ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Mhe. Pandu Ameir Kificho	- SPIKA
1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	- MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	- MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	-MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	-MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	-MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	-MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	-MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	-MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	-MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	-MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	-MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	-MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	-MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	-MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	- Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	-Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	- Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	-Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	-Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	-Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	- Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	- Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	- Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	- Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	- Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	- Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	- Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	- Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	- Nafasi za Wanawake

37.Mhe. Ashura Sharif Ali - Nafasi za Wanawake

38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad - Nafasi za Wanawake

39.Mhe. Farida Amour Mohammed - Nafasi za Wanawake

40.Mhe. Fatma Mbarouk Said - Jimbo la Amani

41.Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Kwamtipura

42.Mhe. Hassan Hamad Omar - Jimbo la Kojani

43.Mhe. Hija Hassan Hija - Jimbo la Kiwani

44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Jimbo la Mji Mkongwe

45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Muyuni

46.Mhe. Kazija Khamis Kona - Nafasi za Wanawake

47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Jimbo la Kikwajuni

48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Jimbo la Kitope

49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Jimbo la Mkwajuni

50.Mhe. Mgeni Hassan Juma - Nafasi za Wanawake

51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma - Jimbo la Bumbwini

52.Mhe. Mohammed Haji Khalid - Jimbo la Mtambile

53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi - Jimbo la Chambani

54.Mhe. Mohammed Said Mohammed - Jimbo la Mpendae

55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - Nafasi za Wanawake

56.Mhe. Mussa Ali Hassan - Jimbo la Koani

57. Mhe. Mussa Khamis Silima - Jimbo la Uzini

58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Rahaleo

61.Mhe. Omar Ali Shehe - Jimbo la Chake-Chake

62.Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Rashid Seif Suleiman - Jimbo la Ziwani

64.Mhe. Raya Suleiman Hamad - Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rufai Said Rufai - Jimbo la Tumbe

66.Mhe. Saleh Nassor Juma - Jimbo la Wawi

67.Mhe. Salim Abdalla Hamad - Jimbo la Mtambwe

68.Mhe. Salma Mohammed Ali - Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Salma Mussa Bilali - Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salmin Awadh Salmin - Jimbo la Magomeni

71.Mhe. Salum Amour Mtondoo - Jimbo la Bububu

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan - Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki - Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai - Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake

79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim - KATIBU

Kikao cha Tisa – Tarehe 29 Juni, 2011

Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi

DUA

Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma dua

TAARIFA

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujaanza mjadala wetu nilikuwa na taarifa ndogo naomba niwajuulishe. Waheshimiwa Wajumbe jana jioni ilisomwa hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Mwenyekiti. Kwa hivyo, Wajumbe hawakupata kuchangia hivyo tumeona leo asubuhi na jioni tutachangia Waheshimiwa Wajumbe na kesho asubuhi watachangia Mawaziri na badala yake tumwite Mhe. Waziri aweze kufanya majumuisho. Waheshimiwa Wajumbe tumezingatia hilo kwa kuwa wizara ni kubwa na ina taasisi nyingi kwa hivyo waheshimiw tukupeni nafasi lakini kila mtu aweke *points* zake vizuri na aende moja kwa moja kwenye hoja.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 200

Kuwepo kwa Ofisi za Ubalozi wa Nchi Za Nje – Zanzibar

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Kabla ya marekebisho ya 10 ya Katiba ya Zanzibar, Zanzibar ndani ya Muungano ilijuilikana kama sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hivyo ilizingatiwa kwa kigezo hicho hata katika upatikanaji wa misaada na ugawaji wa fursa mbali mbali

mfano: Ofisi za Kibalozi na Maafisa wa Kibalozi ndani na nje ya Tanzania. Hivi sasa ibara ya 2 ya Katiba ya Zanzibar ya 1984 Toleo la 2010 inaitambua Zanzibar ni miongoni mwa nchi mbili zinazounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(a) Tanzania ina Ofisi ngapi za Ubalozi nje.

(b) Ni Ofisi ngapi kati ya hizo zinaongozwa na Wazanzibari.

(c) Kwa kuwa Zanzibar ni mdau (*counterpart*) wa Muungano, Idara ya Mambo ya Nje inaishirikisha vipi Zanzibar katika shughuli za uajiri wa Maafisa.

(d) Je, kutokana na marekebisho haya ya Katiba ya Zanzibar, hatuoni haja ya Ofisi za Ubalozi wa nchi mbali mbali sasa kuwepo hapa Zanzibar badala ya utaratibu wa sasa wa kupatiwa Ofisi chache tu za Ubalozi Mdogo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 200 lenye vifungu (a), (b), (c), na (d) kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa kabla ya marekebisho ya 10 ya Katiba ya Zanzibar, Zanzibar ilijulikana kama sehemu ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo hivi sasa ibara ya 2 ya Katiba ya Zanzibar ya 1984 Toleo la 2010 inaitambua Zanzibar kuwa ni miongoni mwa nchi mbili zinazounda Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, pamoja na marekebisho hayo suala la Mambo ya Nchi za Nje bado ni suala la Muungano.

Mhe, Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa nimjibu Mhe. Mwailishi swali lake Nam. 200 lenye vifungu (a), (b), (c) na (d) kama hivi ifuatavyo.

a). Mhe. Naibu Spika, Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania inazo Ofisi za Kibalozi thalathini na mbili (32) na Ofisi ndogo za Kibalozi (*Consulates*) mbili (2). Pia inazo Balozi mbali mbali za heshima yaani *"Honorary Consulates"* katika baadhi ya nchi duniani.

b). Mhe. Naibu Spika, Ofisi za Kibalozi zinazoongozwa na Wazanzibari ni tatu ambazo ni Stocklm – Sweden, Balozi Mohamed Mzale, Cairo –Misri Balozi Ali Haji Shauri na Beijing – China Balozi Omar Ramadhan Mapuri. Aidha, Ofisi ya Ubalozi wa Oman ilikuwa ikiongozwa na Balozi Hussein Said Khatibu na Ofisi ya Ubalozi wa Italy ilikuwa ikiongozwa na Balozi Ali Karume ambao kwa sasa wamestaafu bado kuteuliwa Mabalozi wengine kujaza nafasi hizo.

c). Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa taratibu za uajiri katika Serikali ya Muungano wa Tanzania, ajira za maafisa zinafanywa na Sekretarieti ya Ajira katika Tume ya Utumishi wa Umma ambayo hutoa fursa sawa kwa kila mtu kuomba nafasi za ajira pale zinapotangazwa bila ya kujali sehemu aliyotoka katika Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, utaratibu huu haukutoa nafasi stahili kwa Zanzibar kupata nafasi stahiki katika Taasisi za Muungano na ndio maana suala hili liliamua kuwekwa katika orodha ya kero za Muungano.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumjuilisha Mhe. Mwakilishi kwamba kufuatia mazungumzo yanayoendelea katika Kamati ya Pamoja ya SMZ na SMT ya kushughulikia Kero za Muungano imekubalika kwamba ipo haja ya kwa na utaratibu maalum wa kuona kwamba nafasi za ajira katika Taasisi za Muungano zinatengwa kwa ajili ya Wazanzibari. Utekelezaji wa suala hili unahitaji marekebisho ya Sheria na kanuni za utumishi zilizopo. Mhe. Naibu Spika, kwa kuzingatia muda unaohitajika hadi sheria hizo kurekebishwa, wizara zinazohusika na utumishi za SMZ na SMT zinaendelea na hatua za kuweka utaratibu wa muda wa mgao kwa nafasi za ajira kwa Taasisi za Muungano hadi hapo sheria zitakapofanyiwa marekebisho.

d). Mhe. Naibu Spika, suala la kufungua Ofisi za Kibalozi ni uamuzi wa nchi husika kulingana na maslahi ya nchi hiyo. Kwa utaratibu uliopo hivi sasa, Ofisi za Ubalozi hufunguliwa Dar-es-Salaam na ofisi ndogo za Kibalozi zinaweza kufunguliwa Zanzibar kama nchi itapenda kufanya hivyo. Hata hivyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inapoona umuhimu wa kuiomba nchi husika kufungua ofisi ndogo ya Kibalozi hapa Zanzibar inafanya hivyo. Mhe. Naibu Spika, hata zile nchi zote ambazo hazina Balozi zake hapa Zanzibar zinashirikiana vizuri na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala mbali mbali ya maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, baada ya majibu ya Mhe. Waziri naomba nimuulize maswali matatu ya nyongeza.

a) Kwa kuwa amekiri kwamba Zanzibar ni miongoni mwa nchi mbili zilizounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na amesema kwamba suala hili liko katika suala la Muungano la mambo ya nje. Mimi naomba kujua ni vigezo vipi ambavyo hupelekea kupatikana kwa mabalozi hata Zanzibar wakapatikana 5 katika 32.

b) Mhe. Naibu Spika, utaratibu wa ajira katika Ofisi za Kibalozi amesema huwa unashughulikiwa kwenye Tume ya Utumishi. Naomba kujua kwa sasa ni wafanyakazi wangapi walioko Balozi za nje ambao ni Wazanzibari.

c) Kwa nini hadi sasa Zanzibar hatuna Ofisi ya Ubalozi na badala yake huwa tunatumia ofisi ndogo tu za Ubalozi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, vigezo vinavyotumika katika kuteuwa Mabalozi ziko taratibu kupitia Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje kutokana hatua kwa hatua mpaka kufikia sifa yakuwa Balozi. Lakini hata hivyo haikusababishii kuteuliwa moja kwa moja kuwa Balozi ni uamuzi wa Mhe. Rais anapoona sasa fulani nimteuwe kuwa Balozi akawakilishe nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu ni wafanyakazi wangapi na ni Wazanzibari wangapi wako Balozi za nje. Mhe. Naibu Spika, suala hili ningeomba nimjibu kwa maandishi kwa sababu sina takwimu za kutosha kwa sasa.

Mhe. Naibu Spika, swali lake la tatu Mhe. Mwakilishi ni kwa nini Zanzibar tuwe na ofisi ndogo badala ya kuwa na ofisi kamili za Ubalozi. Mhe. Naibu Spika, ni utaratibu tuliokubaliana katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba Ofisi za Kibalozi zitafunguliwa Dar es Salaam na ofisi ndogo zitafunguliwa hapa

Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, hii inatokana kwamba kwa wakati huo Dar es Salaam ilikuwa ndio Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kwa hivi sasa inavyotakiwa hizo Ofisi za Kibalozi zifunguliwe Dodoma lakini haijaonesha ishara ya Mabalozi wenyewe kuanza kuhamia huko Dodoma.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Waziri swali dogo tu la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mhe. Mwakilishi alielezea namna Mabalozi wanavyochaguliwa na wanavyopatikana na akasema kwamba ni maamuzi zaidi ya Mhe. Rais.

Mhe. Naibu Spika, ni kwamba Tanzania ina Mabalozi wangapi nchi za nje na katika hao Wazanzibari ni wangapi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, katika jibu langu la msingi nilieleza kwamba Balozi za Tanzania zilizoko nje ni 32 na katika hizo kwa sasa Wazanzibari wako 3 huko nyuma walikuwa ni 5 kutokana na wawili kustaafu kazi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kuniruhusu niulize angalau swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mabadiliko ya 10 ya Katiba ya Zanzibar imetangaza Zanzibar kama ni moja kati ya nchi mbili zinazounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kwa kuwa mpaka hivi sasa Dar es Salaam ndio inayobakia kuwa na Balozi zote pale.

a) Je, kuendelea Ofisi za Ubalozi kubakia Dar es Salaam na kuiacha Zanzibar kumalizia mabalozi wadogo utakubaliana na mimi kwamba ni moja kati ya kero za Muungano hizo.

b) Kwa kuwa Zanzibar ni nchi Balozi kuendelea kubakia Dar es Salaam tu pale haitaipotezea Zanzibar ule uwezo wake halafu viongozi wetu wakitaka kuzungumza na Ofisi ya Ubalozi waende Dar es Salaa wakasajili pale mpaka wawapate, lakini zikiweko huku basi nadhani viongozi wetu wangekuwa wanaenda hapa Zanzibar Mjini kuzungumza na Mabalozi wetu. Kwa hivyo, hii si kuidhalilisha Zanzibar Mabalozi kubakia Dar es Salaam.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kuweko Balozi Dar es Salaam sio kero za Muungano ni utaratibu tuliokubaliana na tulikubaliana kwamba Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa wakati ule yatakuwa Dar es Salaam kwa sasa yapo Dodoma, lakini kutokana na *traditional* yetu tumeendelea kuwa na Balozi zile pale Dar es Salaam. Lazima tukubaliane suala la Muungano ni kama ndoa wakati mwengine, kwa kuwa unapunguza sehemu ya uhuru wake, unapokuwa na ndoa yale ambayo uliyafanya kabla ya kuoa huwezi kuyafanya baada ya kuoa. Vile vile unapokuwa na Muungano lazima yako mambo yatakukuta ambayo yatakupunguzia sehemu ya uhuru wako.

Kwa hivyo, kuweko Balozi Dar es Salaam sio kero bali ni utaratibu tuliokubaliana ambao tunautekeleza vizuri. Kwa upande wa kuwa kwa nini Balozi zile zisiwepo hapa Zanzibar na viongozi wetu wanapata tabu kwenda Dar es Salaam, kwa sababu Muungano ni gharama na jambo lolote kulifanya ni gharama kwa hiyo si tatizo kwa viongozi kwenda Dar es Salaam kuzungumzia maslahi ya nchi yetu na Dar es Salaam na Zanzibar sio mbali kwa sasa utaratibu ni huo.

Mhe. Naibu Spika, lakini hivi sasa Serikali zetu zimeanzisha mchakato wa kutoa maoni kuhusu Katiba mpya, mara mchakato huo utakapoanza basi yote hayo kama Wazanzibari wanaona hili

ni tatizo na waeleze kinagaubaga matatizo yao na Serikali zetu zitawasikiliza.

Mhe. Makamo wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, namshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa majibu yake mazuri kuhusu suala hili liloulizwa.

Mhe. Naibu Spika, kufunguliwa Balozi kamili Dar es Salaam inatokana na *Vienna Convention of Diplomatic Practice* kwa Balozi zote kamili zinafunguliwa kwenye *capitals* za nchi. Zanzibar sio *capital* ya *United Republic of Tanzania* na ndio maana Balozi kamili zinafunguliwa Dar es Salaam na Balozi ndogo zinafunguliwa Zanzibar, na Balozi ndogo zinaweza kufunguliwa popote Tanzania kuna Balozi ndogo za nchi Kigoma, tunazo hapa Zanzibar zinaweza kuwa Arusha na kadhalika. Lakini ule Ubalozi wenyewe kwa mujibu wa taratibu za kidiplomasia lazima zifunguliwe kwenye *capital* ya nchi. Mhe. Naibu Spika, sisi Tanzania tunao Ubalozi mdogo mfano Saudia Arabia Jidah, lakini Ubalozi kamili uko Riadh kwa sababu ndio *capital* ya *UAE*, tunao Ubalozi mdogo Mombasa lakini Ubalozi wetu kamili uko Nairobi. Kwa hivyo, hii ni kwa mujibu wa taratibu za kidiplomasia wala sio kwa sababu nyengine zozote.

Nam. 102

Uuzwaji wa Majengo ya Serikali na Maeneo ya Wazi

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) - Aliuliza:-

Kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi juu ya uuzwaji wa baadhi ya majengo ya Serikali na maeneo ya wazi.

(a) Je, ni kweli kwamba jengo la Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali limeuzwa.

(b) Kwanini Serikali iliamua kuuza jengo hilo na kwa kutarajia faida gani.

(c) Je, ni kiasi gani cha fedha ambacho Serikali imepata kutokana na mauzo hayo.

(d) Je, Serikali imechukuwa hatua gani kuwapatia wafanyakazi wa taasisi ambazo zilikuwa kwenye jengo hilo pahala pengine pa kufanyia kazi.

(e) Ni hatua gani madhubuti zilizochukuliwa katika kuhakikisha kuwa nyaraka zetu haziathiriki kutokana na kuhamishwa huko, na ni kiasi gani cha gharama zitakazo tumika kuzihamisha taasisi hizo na kuziweka sehemu nyengine.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 102 lenye kifungu (a), (b), (c), (d) na (e) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, jengo lilokuwa likitumia na Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali Zanzibar pamoja na tasisi nyengine lijuulikanalo kwa jina la Mambomsige halijauzwa.

(b) Mhe. Naibu Spika, kama nilivyo jibu kifungu (a) jengo hilo halijauzwa kwa hivyo hakukuwa na matarajioa ya faida ilotokana na mauzo.

(c) Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa jengo hilo halijauzwa, hakuna fedha iliyopatikana itokanayo na mauzo.

(d) Mhe. Naibu Spika, Serikali imechukua hatua zifuatazo katika kuwapatia watumishi wa taasisi zilizokuwa zikitumia jengo hiolo maeneo mengine ya kufanyiakazi.

(i) Serikali imetumia Tsh. 172 milioni kwa ajili ya kulikarabati jengo la Benki ya Watu wa Zanzibar la Forodhani jengo hilo limehamiwa na watumishi wa Ofisi ya Mrajis Mkuu na watumishi wa Wakfu kuhamia hapo.

(ii) Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali wamehamia katika Jengo lao lilioko Maisara Mjini Zanzibar.

(iii) Shirika la Meli walikuwa wameshakamilisha matengenezo ya jengo lao liliopo Malindi hivyo, wamehamia katika jengo hilo.

(iv) Mhe. Naibu Spika, kabla ya kuhamisha nyaraka mbali mbali Serikali ilipata ushauri wa kitaalamu kutoka kwa Idara ya Nyaraka na Mambo ya Kale ushauri huo ulikuwa juu ya njia bora ya kuzihamisha nyaraka hizo. Ushauri huo ndio uliofuatwa wakati wa kuzihamisha nyaraka hizo, aidha serikali ilitumia Tsh. 8.5 milioni kwa ajili ya kuzihamisha taasisi hizo.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri katika majibu yake ametwambia kwamba jengo hilo halikuuzwa inawezekana sasa atueleze limefanywa nini, limekodishwa au limefanywa kitu gani.

b) Ni utaratibu upi ulotumika katika huko kukodishwa kwenyewe kama limekodishwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, jengo hili kuna makubaliano ya kulikodisha. Pia kuhusu utaratibu unaotumika wa kukodisha jengo lolote la serikali ni kwa mtu muhusika au taasisi husika kuandika barua yake kwa Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi na Majenzi na ikiwa jengo hilo halina matumizi mengine na matumizi yako ambayo umejieleza katika barua yako yanakidhi hoja za serikali, jengo hilo utakodishwa kama halina mtu mwengine. Kwa hivyo, huo ndio utaratibu ambao aliyetia nia ya kutaka kulikodi jengo hilo amefuata utaratibu huo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri katika majibu yake alisema kuwa wizara ambazo kila sehemu walioko katika jengo lile wamehamia katika zao. Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi Shirika la Meli limetoa fedha zake mwenyewe kwa kutengeneza ofisi yake na mpaka leo wizara yake haijawalipa.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mwakilishi swali hili limekwenda nje ya utaratibu naomba ulitafutie utaratibu mwengine wa kuliuliza.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye (a), (b) na (c).

a) Napenda kumuuliza Mhe. Waziri hili jengo kama limekodishwa je, limekodishwa kwa muda wa miaka mingapi.

b) Je, hili jengo hizo fedha zilizokodishwa ni kiasi gani.

c) Je, wale wafanyakazi waliokuwemo mle ndani wamelipwa fidia au wamehamishiwa vipi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, labda nitoe maelezo ili Waheshimiwa Wajumbe wasipate shida ya kufahamu kinachoendelea katika jengo lile. Mhe. Naibu Spika, Mambomsige pana mambo mawili, kuna ardhi na kuna na jengo.

Mhe. Naibu Spika, serikali imetoa *lease* ya ardhi na imekodisha ardhi ile kwa miaka 99 kwa kiwango cha dola 10 kwa mwaka lakini kodi hiyo itakuwa *reviewed* kila baada ya miaka 3. Jengo bado halijakodishwa tutatumia sheria ya *Rant Restriction Act* ambayo imepitishwa na Baraza lako tukufu kukodisha jengo lile, tunachosubiri jengo lile lifanyiwe ukarabati tulione *status* yake halafu serikali ndio tuseme sasa tunakodisha kiasi gani hili jengo. Mhe. Naibu Spika, hayo ndio makubaliano baina ya serikali na mwekezaji.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, katika masuala matatu ya nyongeza yaliyoulizwa na Mhe. Mwakilishi limebakia moja naomba kumuelezea kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, ni kwamba wawekezaji hawa wametupatia dola milioni 1.5 kwa ajili ya kuwahamisha kuwajengea jengo jengine wenzetu waliokuwa wakitumia jengo la Mambomsige, hii ni nje ya kodi.

Nam. 1

Udhibiti wa Wimbi la Walimu
Kukimbilia Skuli za Tanzania Bara

(Mheshimiwa aliyeuliza hili ameliondoa)

Nam. 29

Kuanzishwa Chuo cha Afya – Pemba

Mhe. Salma Mussa Bilali - Aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa kumekuwa na upungufu wa Wataalamu katika fani mbali mbali kwenye Vituo vya Afya zaidi huko Pemba. Tatizo kama hili lilikuwa katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na lilitatuka pale Wizara hiyo ilipofungua Chuo na kutoa mafunzo ya Ualimu huko Wete, Pemba.

Je, Wizara yako haioni kuwa kuna haja ya kuanzisha masomo ya Wakunga na Wauguzi huko Pemba ili vijana hao wabaki kwa idadi kubwa Kisiwani hapo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 29 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, tatizo la upungufu wa wataalamu linaeleweka na ndio maana tukaweka mkakati wakuongeza nguvu kwenye fani ya wataalamu, wakusomesha kada mbali mbali za Afya pamoja na kuongeza madarasa na vifaa vipya huko Chuo cha Afya Mbweni.

Mhe. Naibu Spika, wizara kwa muda mrefu ilikuwa na azma ya kuanzisha Chuo cha Afya Pemba eneo liliopo Gombani (Ustawi

wa Jamii) Chake-Chake lilipendekezwa kwa ajili ya ujenzi huo. Azma hii ulishindikana kutokana na sababu mbali mbali zinazojumuisha gharama za uendeshaji, uhaba wa vifaa vya kufundishia, walimu wa wataalamu mbali mbali wa nadharia na vitendo. Aidha taaluma za sayansi za afya zinahitaji umahiri mkubwa unaokubalika kimataifa kwa viwango mahsusi vilivyowekwa.
Mhe. Naibu Spika, kwa kuliona hilo, wizara iliona ni vyema kuanza kukiimarisha Chuo cha Afya kilichopo Mbweni. Uimarishaji huo umejumuisha upanuzi wa madarasa na ujenzi wa dakhalia za wanafunzi ili kukidhi haja ya kupokea idadi kubwa ya wanafunzi ikiwemo wale wa kutoka Pemba.

Kwa sasa idadi ya wanafunzi wanaochukuliwa kujiunga na chuo imeongezeka sana kutoka 180 hadi 280 sawa asilimia 35. Ni imani ya wizara kuwa ongezeko hilo la wanafunzi litasaidia kupata idadi kubwa ya wafanyakazi watakaopangiwa kufanya kazi na kubaki huko Pemba.

Mhe. Naibu Spika, wizara imeandaa utaratibu maalum wa uteuzi wa wanafunzi watakaojiunga katika Chuo cha Afya Mbweni ambapo nafasi hizo zitatolewa kwa mujibu wa mahitaji ya wafanyakazi Unguja na Pemba. Aidha, mikakati maalum ikiwemo mikataba itazingatiwa na kusimamiwa. Sambamba na hilo wizara imeweka mkazo maalum wa kupeleka wafanyakazi mahala ambapo kuna upungufu zaidi hasa Pemba.

Mhe. Salma Mussa Bilal: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. katika majibu yake amesema kwamba wamewapeleka wafanyakazi kwa miaka miwili Pemba kwa mkataba. Je, hiyo mikataba tayari wameshafungishwa.

Pili, tumepata taarifa kwamba tayari kuna wafanyakazi hao wameshapelekwa Pemba hiyo miaka miwili kwa mkataba, lakini

baadhi ya wafanyakazi hao wamepatiwa makaazi na serikali, kuna baadhi ya wafanyakazi mpaka leo bado hawajapatiwa makaazi na wanaishi katika nyumba za kupanga. Je, wizara yake ina mpango gani wa kuwasaidia hawa wafanyakazi ambao hawajapatiwa makaazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, hayo masuala anayouliza hayana uhusiano kabisa na suala hili wala sikusema mimi kama kuna wafanyakazi tumewapeleka Pemba. Sijasema hilo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa asubuhi hii. Mimi nataka kujua tu vituo vya Unguja na Pemba ni vingapi.

Pili, wataalamu wanaotoka Kituo cha Afya Mbweni ni wangapi kwa mwaka na ni lini chuo hicho kitatoa wataalamu wanaoweza kutosheleza mahitaji yetu kwa vituo vyetu vya afya.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, vituo vya afya vilivyoko Unguja na Pemba ni kwamba Unguja kuna vituo 78 na Pemba vituo 59. idadi ya wataalamu hiyo nitamletea kwa mandishi, kwa sababu kwa hapa sinayo. Lakini kwa mipango ambayo tumeipanga tuna mategemeo labda baada ya miaka mitano tutakuwa na wafanyakazi wa kutosha na kuzidi hata idadi tunayoihitaji.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabla sijamuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza napenda niupongeze uongozi wao kwa kuona ile haja ya kupeleka ma-*nurse* wengi wa vituo mbali mbali. Swali langu ni hili, kwa kuwa usafiri umeimarika baina ya Unguja na Pemba na kwa kuwa Chuo cha Afya, Mbweni kinasomesha wanafunzi kutoka sehemu zote mbili za Unguja na Pemba, kwa nini hawaoni haja angalau ule mwaka wa tatu wale wanaotoka

Pemba kuwamalizia kule ili wakazoeana na ile hali ya hospitali za kule na ikawa ni rahisi kuwapangia kazi katika maeneo yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema katika swali la msingi kwamba, chuo kinafuata utaratibu wa kupeleka wanafunzi katika sehemu zile ambazo zitaweza wao kuwasimamia. Pemba wafanyakazi wa kusimamia wanafunzi ili waweze kufanya hizo shughuli zinazotakiwa hawapo, tuna upungufu wa wafanyakazi katika Chuo cha Afya Mbweni, tunategemea Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa ndio hospitali ambayo inafundisha wanafunzi na pale ndipo penye watu wenye utaalamu wa kutosha kuwasimamia wanafunzi hao.

Kutokana na upungufu ulioko Pemba hata ukimpeleka mtoto yeye mwenyewe atasimama peke yake hana wa kumsimamia. Kwa hivyo, utaratibu uliopo Hospitali ya Mnazi Mmoja ndio hospitali inayofundisha wafanyakazi na ndiko tutakakowapeleka na ndiko watakakopata usimamizi unaostahili ili kuweza kutoa wafanyakazi bora.

Nam. 105

Gharama Kubwa za Kukodisha Trekta

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) – Aliuliza:-

Imebainika kuwa wakulima katika bonde la Makoba wanashindwa kulima kutokana na bei kubwa ya kukodi trekta na hasa ukizingatia kuwa wakulima wetu ni wanyonge mno.

Mhe. Waziri, kwa kuwa kilimo ndio uti wa mgongo, Je, serikali itawasaidiaje wakulima hawa ili waweze kupata unafuu.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 105 kama hivi ifuatavyo:-

Suala la kilimo cha matrekta mabondeni linasimamiwa na Jumuiya za Wakulima wenyewe kwa wale ambao wameamua kununua matrekta kupitia mradi wa *TASAF* ikiwemo kupanga bei. Hata hivyo, serikali katika msimu ujao imekusudia kupunguza bei ya huduma za kilimo kwa wakulima wote ikiwemo huduma za matrekta**.**

Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mhe. Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Moh'd Shein imedhamiria kuleta mageuzi makubwa ya kilimo kupitia programu yake mahsusi ya Mapinduzi ya Kilimo yenye lengo la kuunga mkono kazi kubwa inayofaywa na wakulima wa nchi yetu kwa kuwapatia zana za kisasa za kilimo na pembejeo kwa utaratibu wa ruzuku, programu hiyo inaanza mwaka huu wa fedha.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa hii kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. Waziri katika jibu lake mama alilojibu ni kwamba kuna sehemu ambazo zina matrekta ya mkopo wa *TASAF*. Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba kuna sehemu nyengine hazina matrekta hayo isipokuwa yapo matrekta ya serikali na bei bado kubwa.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, ninakubaliana sana na Mhe. Makame Mshimba kwamba yapo mabonde mengine hakuna matrekta haya niliyoyazungumzia ya *TASAF*, bali yapo matrekta ya serikali ambayo yanatoa huduma kwa wananchi.

Nam. 14

Kuimarisha Mashamba ya Ng'ombe wa Maziwa

Mhe. Salma Mussa Bilali – Aliuliza:-

Chakula cha aina ya *protein* kitokanacho na nyama pamoja na maziwa ni muhimu kwa afya ya mwanaadamu. Mashamba ya Mifugo hasa ya ng'ombe yalitusaidia sana kwa kupata maziwa ya kutosha pamoja na vitoweo. Aidha, yalitoa ajira kwa vijana wetu.

(a) Kwa nini Mashamba ya Ng'ombe wa Maziwa kama ya Makurunge, Kizimbani na Bambi yamesimamishwa kutoa huduma hiyo.

(b) Katika kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa vitoweo vya kutosha na vya bei nafuu ambayo wananchi wa kipato cha chini wataimudu. Je, Wizara yako ina mpango gani madhubuti wa kurejesha na kuimarisha mashamba hayo au kuanzisha mashamba mengine zaidi.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi – Alijibu:-

Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 14 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Lakini kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba nikubaliane naye kwamba, chakula kitokanacho na nyama na maziwa ni muhimu sana kwa afya ya binadamu, na naomba nichukue fursa hii kuwatanabahisha wananchi kwamba badala ya kutumia vinywaji vinavyotengenezwa kwa kemikali ambavyo mara nyengine vinywaji hivyo vinaweza vikaathiri sana siha zetu, ninawashauri zaidi kutumia vinywaji vitokanavyo na maziwa ambayo hujenga zaidi siha za miili yetu na vizazi vyetu.

Baada ya maelezo sasa naomba kujibu swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, mashamba ya ng'ombe wa maziwa ya Makurunge, Kizimbani, Bambi na mengineyo, yamesimamisha huduma za uzalishaji hivi sasa kutokana na mabadiliko ya kisera yaliyoidhinishwa na Baraza lako tukufu, ambapo Wizara ya Mifugo na Uvuvi sasa haijishughulishi moja kwa moja na uzalishaji wa mifugo na mazao yake. Kazi ya uzalishaji imepangiwa na sera kuendeshwa na sekta binafsi na kazi ya wizara na serikali ni kuandaa mazingira mazuri ikiwa ni pamoja na kuweka sheria, kanuni, mafunzo pamoja na udhibiti mbali mbali kwa kuongoza sekta nzima ya mifugo na uwezeshaji wa ufugaji wenyewe.

(b) Mhe. Naibu Spika, katika kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa vitoweo vya kutosha na bei nafuu, wizara yangu inaendelea kushajiisha na kuhamasisha watu mbali mbali wakiwemo wa ndani na nje ya nchi kuwekeza katika uzalishaji wa mifugo na mazao yake, na kwa taaluma inayotolewa hivi sasa sekta binafsi ikiwemo wenye kipato cha chini imeanza kupata maendeleo makubwa ya uzalishaji wa mayai, maziwa, kuku na jitihada zimeanza za usarifu wa mazao hayo. Aidha, Jumuiya za Wafugaji pamoja na wafugaji wadogo wadogo wataendelea kupewa umuhimu katika kuendeleza sekta ya mifugo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Nashukuru sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kuwa uvumi uliopo ni kuwa shamba la Pangeni limeuzwa.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, sikubaliani naye Mheshimiwa kwamba shamba la Pangeni limeuzwa.

Mhe. Asha Abdi Haji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba kuuliza swali la nyongeza kwa Mhe. Waziri. Alipokuwa akijibu swali lake mama nilimsikia kuzungumzia shamba la Makurunge, nilisikia kwamba shamba hili limechukuliwa na limebakia sehemu ndogo. Je, suala hili ni kweli? Ikiwa ni kweli nani aliyechukua na ni nani aliyemiliki na kutumika kwa kazi gani.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, shamba la Makurunge linamilikiwa na Halamshauri ya Wilaya ya Bagamoyo. Ni kweli kwamba katika hekta 30,000 tulizokuwanazo, hekta 24,000 Halmashauri ya Wilaya kama mmiliki wa Bagamoyo wamewapa watu wengine na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imebakiwa na hekta 6.000.

Hivi sasa bado Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo ndiye anayelimiliki, lakini hapa Zanzibar anayelitumia ni Wizara ya Mifugo na Maliasili kupitia chuo chake cha Kizimbani. Chuo cha Kizimbani wanategemea kutumia kwa ajili ya utafiti mbali mbali kwa sababu ndani ya Chuo cha Kizimbani pia kunaendeshwa mitaala ya mambo ya mafunzo ya mifugo. Kwa hivyo, ni eneo ambalo litatumika vibaya kwa ajili ya utafiti wa mifugo kama ni *attachment* ya Chuo cha Kizimbani ambacho serikali ina mpango wa kukiendeleza hadi kutoa dgree ya kwanza na ya pili katika chuo hicho.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipatia fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri anaonekana kwamba wizara yake inawashajiisha wananchi kwa kuweza kujipatia kitoweo cha nyama na maziwa, na kwa kuwa bahari inajitahidi sana katika mambo ya kutoa vitoweo wakiwemo samaki na pweza, lakini

inaonekana wizara yake haikutupia macho na kwa kuwa wananchi hasa wa Kijiji cha Vitongoji na Furaha katika Jimbo la Wawi wameshajitokeza kuanzisha mashamba ya uzalishaji wa samaki. Je, serikali yake ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi wale ili kuendeleza kupata kitoweo wao na wananchi wengine wa Zanzibar. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba wananchi wa Jimbo la Wawi na hasa sehemu ya Vitongoji ambayo Mhe. Mwakilishi ndiko anakotoka wamehamasika sana na kushughulikia ufugaji wa mazao ya baharini. Zamani Mhe. Mwakilishi anajua kwamba hata yeye mwenyewe alikuwa mlaji mkubwa wa kasa, lakini nashukuru kwamba yuko pamoja na wizara yangu kuona kwamba ulaji wa kasa yeye mwenyewe ameacha na wananchi wake anawahamasisha waache, namshukuru kwa hilo.

Kuhusu suala la namna gani tutashirikiana na wananchi wale wa Jimbo lake katika ufugaji wa mazao ya baharini, tayari mimi mwenyewe Mhe. Naibu Spika, tuna *contact* kubwa na wananchi wake na baada ya Baraza hili tumepanga kwamba twende pale na wataalamu wangu kwenda kuendelea kuwafunza namna ya ufugaji wa mazao baharini na wameniomba kuwapatia kijana mmoja au wawili mafunzo ya ndani na nje ya nchi, ahadi hiyo nimeichukua na wakati wowote nafasi ikitokea nawaahidi kwamba na wao watapata.

Nam. 48

Mfuko wa Mkopo Nafuu kwa Wananchi

Mhe. Abdi Mosi Kombo – Aliuliza:-

Katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya sita kulinzishwa mfuko wa mkopo nafuu kwa wananchi wa kipato cha

chini, lakini kwa bahati mbaya, wananchi wa kipato cha chini wa Shehia ya Matemwe hawakufaidika na mkopo huo.

(a) Kama wananchi wa kipato cha chini walio wengi hawakufaidika na mikopo hiyo. Je, ni nani waliofadika na mikopo hiyo.

(b) Tangu kuanza kwa mfuko huo ni kiasi gani cha fedha kimeshatolewa na ni kiasi gani kimebaki.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny: Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika) – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 48 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, watu waliofaidika na mkopo nafuu ni wananchi wa kipato cha chini ambao wamekubaliana kutimiza masharti ya mkopo huo na miongoni mwa waliofaidika na mkopo huo ni wananchi wa Jimbo la Matemwe. Jumla ya wananchi 21 wa Jimbo la Matemwe wamefaidika kama ifuatavyo:

- Shehia ya Matemwe watu 3
- Shehia ya Kandwi watu 18.

Jumla ya fedha zilizotolewa kwa Jimbo la Matemwe ni shilingi **40,400,000/=**

(b) Mhe. Naibu Spika, tangu kuanza kwa Mfuko wa AK na JK fedha zilizotoka ni shilingi Bilioni moja na Milioni mia nne na sitini na tatu laki sita na arubaini elfu (1,463,640,000/=). Na fedha zilizobakia ni shilingi Bilioni mbili milioni mia moja thelathini na sita laki

tatu na sitini elfu (2,136,360,000/=) kati ya shilingi Bilioni tatu na Milioni mia sita (3.6 Bilioni).

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. kwa kuwa hivi sasa bado wananchi wanaendelea kutumia Mfuko wa AK na JK. Je, Mhe. Waziri Mfuko mpya wa JK na AS utaanza lini ili wananchi wafaidike na mifuko hii.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny: Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika): Mhe. Naibu Spika, mpaka sasa hivi tunaendelea kutumia Mfuko wa AK na JK, lakini yapo matumaini makubwa ambayo mwenyewe Mhe. Rais alisema utakuwepo pia Mfuko wa AS.

Nam. 23

Mashirika ya Serikali Kumiliki Mali (*ASSETS*)

Mhe. Ali Salum Haji - Aliuliza:-

Kwa kuwa hadi hivi sasa utaratibu wa mali (*assets*) za Shirika la Meli na Uwakala zinamilikiwa na Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Utaratibu huu unalinyima Shirika uwezo wa kupata mikopo kutoka katika mabenki na hivyo kusababisha Shirika kushindwa kujiimarisha na kujiendeleza kibiashara.

(a) Je, Mhe. Waziri anaweza kueleza kuna sababu gani zilizopelekea Shirika hilo kutomiliki mali zake.

(b) Je, ni Mashirika mangapi ya Serikali yanayomiliki mali zake na kwa sababu zipi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 23 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, Shirika la Meli la Zanzibar limeasisiwa chini ya sheria iliyokuwa ya Mashirika ya Umma ya mwaka 1978 chini ya sheria Nam. 04, ambayo imefutwa mwaka 2002 kwa kuanzishwa sheria nyengine ya Mitaji ya Umma.

Mhe. Naibu Spika, kwa mnasaba huo na kwa mujibu wa sheria hii, hakuna kikwazo chochote kinacholifanya Shirika la Meli la Zanzibar kutokumiliki meli zake wenyewe. Hata hivyo, napenda nikiri kwa muda mrefu kumekuwa na mkanganyiko juu ya umiliki wa mali za shirika hilo kuwepo chini ya Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Ili kuondoa mkanganyiko huo Shirika la Meli limo katika hatua za mwisho za kuandaa rasimu ya sheria, sheria ambayo italipa uwezo shirika kumiliki meli zake wenyewe na rasimu hiyo itawasilishwa Barazani katika vikao vijavyo.

(b) Mashirika ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yanayomiliki mali zake wenyewe yaliyo chini ya Wizara ya Miundombinu ni Shirika la Bandari, hali hiyo inatokana na sheria iliyolianzisha Shirika lenyewe la Bandari sheria Nam. 1 ya mwaka 1997.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. hivi karibuni tulisikia kuwa Meli ya M.V. Mapinduzi imeuzwa. Je,

Mhe. Naibu Waziri imeuzwa kwa kiasi gani na pesa hizo zimekwenda wapi.

Pili, Mhe. Naibu Waziri huoni iko haja ya hivi sasa hizo fedha ambazo zimeuziwa meli hiyo wakapewa wenyewe Shirika la Meli wakanunua meli nyengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, katika majibu mama nimeeleza kwamba hakukuwa na kikwazo kinachoifanya Shirika la Meli kutokumiliki meli zake wenyewe, lakini nikiri kumekuwa na mkanganyiko na mali nyengine kumilikiwa na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Mkanganyiko huu ndio uliopelekea pamoja na sababu za kiufundi meli hiyo ya M.V. Mapinduzi kuuzwa na imeuzwa na Wizara ya Fedha na kiasi kilichouzwa ni Dola laki tatu na tisini na tano. Fedha zipo na imeuzwa kwa mnasaba wa ku-*phase out.*

Mhe. Naibu Spika, nikubaliane na rai aliyoitoa Mhe. Mjumbe, lakini naamini kwamba fedha hizo Wizara ya Fedha watatupatia pale tutakapozihitaji na sisi kama Wizara ya Miundombinu na Shirika la Meli tuko katika harakati na mazungumzo tumeshaanza na wahisani na wafadhili watakaoweza kutusaidia kupata meli.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, Shirika la Meli kwa kumbukumbu zangu lilikabidhiwa meli tatu kwa wakati mmoja zikiwa katika hali nzuri, M.V Ukombozi ya Mafuta, M.V. Maendeleo na M.V Mapinduzi ya abiria na meli zikifanya kazi na kuingiza mapato.

Lakini meli ziliendelea na zikafa zote, zikatengenezwa na hivi sasa hazimo katika mamlaka ya kiuendeshaji wamezikodisha, lakini wakati ule ule tuna Shirika la Bandari la Wizara hii hii ya Miondombinu na Mawasiliano, lina uwezo wa kutengeneza meli zilizoharibika na mfano ni Meli ya Jitihada ambayo ilikuwa katika

hali mbaya na hivi sasa inafanya kazi. Kwa manufaa na maslahi ya nchi hii na uendeshaji wa mashirika yenyewe, kwa nini wizara haioni kuwa iko haja ya Shirika la Meli kupewa kazi nyengine lakini hivi vyombo vya baharini vikapelekwa katika Shirika la Bandari.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, napenda ifahamike kuwa Shirika la Meli lina dhamira nzuri na ya dhati ya kutaka kuzuia matumizi ya fedha za serikali ili zitumike kwa matumizi yenye tija. Matengenezo yanayokwenda kufanywa nje kwa maana kama Mombasa na kutokufanywa katika Shirika la Bandari yanatokana na mahitaji halisi ya matengenezo yenyewe.

Mhe. Naibu Spika, kama tunavyojua meli zetu hizo ni kongwe, katika matengenezo hayo kunahitajika vipuri na baadhi ya zana ambazo hapa petu hazipo. Ili kufanikisha matengenezo hayo yawe vizuri inatulazimu meli hizo kwenda kutengeneza nje ya Zanzibar.

Nam. 81

TV Kutoonekana Pemba

Mhe. Farida Amour: Mhe. Naibu Spika, kwa vile suala la Televisheni Pemba limeshatolewa ufafanuzi wa kutosha kwa heshimia naomba kuondoa swali langu.

Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa.

Nam. 57

Umilikaji wa Ardhi kwa Wananchi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Kwa kuwa anapokuja mwekezaji kwa nia ya kutaka kuwekeza analazimika kulipa fidia kwa wananchi na baadae Serikali humkodisha ardhi hiyo kwa mkataba maalum na endapo mwekezaji atavunja masharti ya mkataba Serikali huufuta mkataba huo.

(a) Je, Serikali baada ya kufuta ardhi ya eneo husika ardhi hiyo inarudi kwa wananchi waliokuwa wakilitumia hapo mwanzo au inarudi chini ya milki ya Serikali.

(b) Kama ardhi hiyo inarudi kwenye milki ya Serikali. Je, Mhe. Waziri unakubaliana na mimi kuwa malalamiko mengi katika ukanda wa pwani yanatokana na wananchi kudhani kuwa ardhi hiyo ni mali yao na wanaweza kuuza tena.

(c) Je, Wizara yako haioni kuwa umefika wakati wa kufanya juhudi za makusudi kuwaelimisha wananchi wa maeneo hayo ili kuepusha malalamiko ambayo msingi wake ni kutokuelewa vizuri sheria.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu**:**

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 57 lenye kifungu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Naibu Spika, Serikali baada ya kufuta Mkataba wa Ukodishaji Ardhi *(Land Lease Agreement)* wa eneo husika ardhi hiyo inarudi katika milki wa Serikali kusubiri mwekezaji mwengine yeyote atakayeomba.

(b) Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba baadhi ya malalamiko yanatokana na kufikiria kuwa ardhi hiyo inarudi katika milki zao. Hii inatokana na baadhi ya koo zenye haki ya kupata fidia kutohusishwa na familia zao wakati wa mchakato wa kugawana fidia hiyo.

(c) Mhe. Spika, Wizara yangu haina pingamizi na ombi la Mhe. Mwakilishi la kufanya juhudi za makusudi za kuwaelimisha wananchi wa maeneo hayo ya pwani na juu ili kuepusha malalamiko ambayo si msingi na baadhi ya wananchi kuepuka sheria.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kipindi hicho kinatoka mara ngapi kwa wiki ili kuwaelimisha wananchi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyotoa. Mhe. Naibu Spika, kimsingi hatuna ratiba maalum ya kutoa taaluma hii lakini taaluma inatolewa kila pale haja inapotokea na tunashirikiana na mikoa na wilaya husika pale ambapo wananchi bado hawajafahamu. Bado tutaendelea kutoa taaluma hii mpaka mgogoro huu umalizike.

Lakini si tatizo kwamba wananchi hawajafahamu, tatizo ni lile alilolisema Mhe. Naibu Waziri alipokuwa anajibu swali mama ni kwamba wakati wa kugawana wananchi zile fidia familia nyengine huwa zinatengwa na baadae hizi familia zilizotengwa ndio hudhani kwamba wao hawakuhusishwa na bado

wanaendelea kudai kwamba lile eneo ni lao. Bado tatizo hilo tutakwamuka kwa kuwapa elimu wananchi hao.

Nam. 107

Serikali kuyapeleka Maoni ya Katiba Mpya ya Wananchi wa Zanzibar katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mhe. Ussi Jecha Simai – Aliuliza**:**

Katika mchakato wa kuanzisha Katiba Mpya na kufuta ile ya zamani ya mwaka 1977, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikusudia kupeleka Mswada wa Kuunda Tume itakayoundwa na Wajumbe kutoka pande zote mbili za Muungano na hatimae kukusanya maoni ya wananchi kuhusiana na muundo wa Katiba hiyo. Hata hivyo, kabla ya mswada huo kujadiliwa Bungeni wananchi wengi wa Tanzania pamoja na Wazanzibari ambao ni wadau wa upande mmoja wa Muungano wa Tanzania wamebahatika kutoa maoni yao.

(a) Je, Mhe. Waziri, hadi sasa Wizara yako imechukua hatua gani za kuyapeleka maoni hayo ya wananchi wa Zanzibar katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(b) Ni upi msimamo wa Wizara yako ikiwa maoni ya Wazanzibari hayatazingatiwa katika uundwaji wa Tume hiyo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria – Alijibu**:**

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 107 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, baada ya Wazanzibari kutoa maoni yao mazuri kuhusiana na mchakato wa rasimu ya Mswada wa Kuunda Tume ya Kukusanya Maoni ya Wananchi kuhusu kuandaa Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mhe. Makamo wa Pili wa Rais aliwasiliana na Mhe. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano kumwelezea mapungufu yaliyoelezwa na wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo Mhe. Makamo wa Pili wa Rais na Mhe. Waziri Mkuu kwa pamoja waliwaagiza Wanasheria Wakuu wa Zanzibar na wa Jamhuri ya Muungano kukaa pamoja na kuyashughulikia yote yale ambayo yalielezwa na kutolewa maoni na Wazanzibari pamoja na Watanzania kwa ujumla. Kazi hiyo ilifanywa kwa pamoja na napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe pamoja na Wazanzibari wote kuwa mswada wa hivi sasa umezingatia maoni yote yaliyoelezwa na Wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, ni nia ya Wizara hii baada ya kumaliza hatua za kisheria zilizobakia na baada ya kuliarifu Baraza la Mapinduzi hatua iliyofikiwa, basi tutafanya utaratibu maalum kwa Waheshimiwa Wawakilishi tuwaelezee yote yaliyoelezwa na Wazanzibari na vipi mambo hayo yamezingatiwa na kuingizwa katika rasimu hii mpya ya mswada kwa utaratibu wa kuanzisha Katiba Mpya.

(b) Mhe. Naibu Spika, Wizara yangu haina msimamo kwa hivi sasa kwa sababu yote yaliyolalamikiwa yameingizwa katika rasimu mpya. Hapa napenda nichukue nafasi hii niishukuru sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kusikia vilio vya Wazanzibari na kwa kupitia kwa Wizara yangu na Afisi ya Mwanasheria Mkuu kukubali kufanya majadiliano ya pamoja kwa vizuri kabisa

na kuyaingiza yote yale maoni yaliyotolewa na wananchi wa Zanzibar.

Lakini napenda nieleze pia kuwa msimamo wa Wizara yangu na wa Serikali kwa ujumla utakuwa ni msimamo wa wananchi kwa kupitia Waheshimiwa Wawakilishi wao ikiwa tu maoni ya Wazanzibari hayatozingatiwa. Kitu ambacho kwa hivi sasa hakitarajiwi kwa sababu maoni yote ya Wazanzibari yameshazingatiwa na yamewekwa katika rasimu hiyo mpya.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwanza tunashukuru baada ya hoja za wananchi wa Zanzibar Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliuondoa mswada ule na kufanya marekebisho sasa hivi tunashukuru kwamba angalau wanashirikiana na Serikali ya Zanzibar katika maandalizi ya rasimu hiyo ya mswada.

Mhe. Naibu Spika, tatizo la Katiba lina mambo mawili. Wenzetu wa upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano wao walitaka Katiba mpya kwa matatizo yao na sisi Zanzibar tulikuwa tunataka Katiba mpya kwa matatizo yetu ambayo yote yanatofautiana. Zanzibar sisi tulitaka Katiba mpya kwa sababu tunahisi hii Katiba ya sasa hivi haitekelezwi au haitekelezeki.

Mhe. Naibu Spika, tatizo lililokuwepo la Katiba ni kutokutekelezwa sio tatizo tunataka Katiba mpya lazima. Je, sasa hivi tunakwenda katika Katiba mpya serikali yetu itatuhakikishiaje kwamba hii Katiba mpya ambayo itaundwa hizi serikali mbili itazitekeleza kama Katiba zinavyotaka.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa kwa kuwa tayari tuna Katiba ambayo bado ni halali na sisi tumekula viapo. Kwa nini kuna baadhi ya

mambo yamo ndani ya Katiba ya Muungano lakini serikali zetu hayatekelezwi kama matakwa ya Katiba yanavyotaka.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, Katiba iliyo nzuri ni Katiba ambayo inaingiza mambo yote yanayohusiana na jamii. Kwa hivyo, kwanza nikitazama kama Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano inaingiza hayo yote, kitu ambacho sifikirii na kitu ambacho hata wewe naamini kwamba hukubaliani na kwamba Katiba hii ya hivi sasa inaingiza hayo.

Kwa hivyo, suala la mwanzo ni kuifanya Katiba ya Jamhuri ya Muungano kuwa nzuri kwa maana ya kwamba uwe ni mnara, iwe ni chombo ambacho kina malengo ya kuwasaidia wananchi wake. Hicho ndio kilio cha mwanzo ambacho kitakuja baada ya wananchi wa Zanzibar na wenzetu wa Tanzania Bara kutoa maoni yao na baada ya kutoa maoni yao ndio Katiba hiyo naamini itakuwa ni nzuri. Lakini suala la pili ni suala la utekelezaji wa Katiba. Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba kitu chochote kile hasa kwa upande wa Sheria na Katiba, Sheria inaweza ikawa ni nzuri lakini ikawa utekelezaji wake ni dhaifu. Kwa maana hiyo, bado tutakuwa tuna matatizo.

Katiba inaweza ikawa ni nzuri wakati huo lakini watekelezaji wake wakawa ni dhaifu. Ninachoomba hapa ni kwa serikali zote mbili lakini zaidi kwa wananchi kwa kupitia Wawakilishi wao na Wabunge kwamba pale ambapo mtu amepewa dhamana kutekeleza jambo katika Katiba au katika Sheria na ikawa hatekelezi ipasavyo, kwa hivyo ni jukumu la Baraza hili na ni jukumu la Wabunge kuhakikisha kwamba mtu yule anachukuliwa hatua zinazofaa kwa mujibu wa hiyo Katiba.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, karibuni tulifanya Marekebisho ya 10 ya Katiba ya Zanzibar. Kwa kuwa sasa hivi kuna rasimu hiyo inakuja

ya kurekebisha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kuwa katika Katiba tuliyopitisha ya Zanzibar Marekebisho ya 10 ndani ya masharti mojawapo ni kwamba masuala yote makubwa yatapigiwa kura ya maoni na wananchi wa Zanzibar na baada ya kupata majibu ya kura ya maoni ndio suala hilo litatolewa uamuzi.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa tunataka kurekebisha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kura ya maoni ina gharama tena kubwa. Je, kwa sababu tunataka kupitisha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania gharama ya kura ya maoni itatolewa na Serikali gani ya Zanzibar au ya Muungano.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, tunachozungumzia hapa ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Kwa hivyo, kwa mantiki hiyo shughuli zote na gharama zote zinazochukuliwa ili kufikia huo uandikaji wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano zitatolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Kwa maana hiyo, hata suala la kura ya maoni litafanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa mujibu wa utaratibu ambao tutakubaliana katika hiyo Rasimu ya Katiba ambayo inajadiliwa hivi sasa.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali alitueleza kwamba rasimu inayotengenezwa sasa hivi imefuata matakwa ya Wazanzibari. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar ndio Wawakilishi wa Wananchi wa Zanzibar.

(a) Je, matakwa haya ambayo yameingizwa katika rasimu hii mpya mawazo ya Wazanzibari yamepatikana vipi.

(b) Je, Serikali haikuona haja ya kuiwakilisha Kamati ya Katiba na Sheria ya Baraza la Wawakilishi kabla ya mswada huo kupelekwa katika Bunge.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, kama alifuata vizuri mtiririko wa majibu yangu kuanzia jibu la jana nilisema kwamba rasimu hii ilipoletwa kwa sababu utaratibu wa sheria yoyote ile kwanza inakwenda katika *public* na maoni ya wadau yanachukuliwa.

Mswada ule wa Katiba ulikuja kupata maoni ya wadau. Kwa maana hiyo, hata wawakilishi kwa wakati huo walikuwa ni wadau na walikuwepo Bwawani. Pale kulikuwa kuna maoni na yale yalikuwa ni maoni ya Wazanzibari na Haile Sellassie palikuwa kuna maoni na yale yalikuwa ni maoni ya Wazanzibari. Maoni hayo kwa pamoja yakatufanya kwamba tuyaingize katika mswada ule.

Mswada ule kama nilivyosema umeyachukua maoni yale yote ya Wazanzibari na jibu la leo nimesema kwamba baada ya kumalizika utaratibu uliobakia wa kisheria ambao ni mdogo mdogo, kwanza kwa mujibu wa utaratibu wetu wa kisheria tulioweka tunapeleka Baraza la Mapinduzi na naamini ni siku mbili tatu hizi hizi ambazo maoni hayo yatapelekwa Baraza la Mapinduzi. Baada ya hapo kama nilivyoahidi ni kwamba Waheshimiwa Wawakilishi ambao ni wawakilishi wa wananchi wa Zanzibar tutawaarifu na wao tutawaambia na hapo ndio jukumu la wawakilishi kwa niaba ya Wazanzibari wetu wote watatoa maoni yao baada ya kurekebisha. Kwa hivyo, napenda nithibitishe tena kwamba baada ya hatua hizo ndogo zilizobakia Baraza la Wawakilishi tukijaaliwa tutaliarifu rasmi.

Hoja za Serikali

Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2011/2012 – Wizara ya Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:

Utaratibu

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, ibara ya 95 ya kanuni yetu imetoa siku 35 za kazi kujadili Bajeti ya Serikali. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa muda uliotengwa hautoshi kama ambavyo imeonekana kwenye Bajeti ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ambayo ilipangiwa siku moja na nusu.

Kwa kuwa Afisi ya Baraza la Wawakilishi tayari imetoa mwongozo kwamba baadhi ya wizara zijadiliwe siku moja na nusu na baadhi ya wizara zijadiliwe siku mbili jambo ambalo halitowezesha ufanisi kwenye Baraza hili.

Kwa kuwa Mhe. Naibu Spika, kanuni ya 57 (6) inamtaka Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kuzungumza kwenye Bajeti ya Serikali kwa zaidi ya dakika ya 30 na Spika anaweza akamuongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwa kutumia kanuni ya 151 ya Baraza la Wawakilishi naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako likubali kuweka kando kanuni ya 95 ili wajumbe wako wapate nafasi ya kujadili hoja hizo za Bajeti ya Serikali kwa kila wizara siku mbili badala ya siku moja na nusu ambazo zimependekezwa na Afisi ya Baraza. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mwakilishi hoja tumeisikia lakini suala la muda serikali ndio inayoweza kutoa maelezo. Kwa hiyo, tunamuomba Mhe. Makamo wa Pili wa Rais suala hili atuwekee

sawa. Lakini kwa Wizara hii ya Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tumeshatoa siku mbili sawa sawa za kujadili. Sasa hayo mengine ya kuongeza muda serikali itatoa uamuzi. Nashauri mimi acha tuchangie halafu hoja hiyo tutakuja kuijibu baadae.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 151 hoja inayotolewa kwa mujibu wa kanuni hii haitotolewa taarifa na itaamuliwa bila ya mabadiliko wala majadiliano. Kwa hivyo, naomba Baraza liamue hoja yangu kama tena kuna msingi tukubaliane na kama hakuna msingi tuendelee mbele.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika na Waheshimiwa Wajumbe, kanuni hii iliwekwa kutokana na hali halisi ambayo serikali itakuwa nayo. Kutokana na mazingira yetu ya kiuchumi kwa sasa fedha ambazo tunazo kwa ajili ya kuendesha shughuli hii ni kwa mujibu wa kanuni kama ilivyo. Tutakapotengua kanuni maana yake tutaongeza gharama ambazo kwa sasa serikali haina.
Kwa hivyo, naomba ushauri Mhe. Naibu Spika, twende nao na tuzidi kushauriana ndani ya serikali halafu tuwe na majibu rasmi baada ya hapo. Kwa hivyo, naomba tuendelee kwa utaratibu huo ambao tunakwenda nao na kama kutakuwa na uwezekano mwengine tutaliarifu Baraza lako tukufu. Lakini kwa sasa tuendelee kwa taratibu za kanuni kama zilivyo ya ibara ya 95 na kama kutatokea jambo lolote lile Mhe. Naibu Spika, kama ulivyoshauri ningeomba tufuate utaratibu ulioshauri.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, maelezo ya Mhe. Waziri nimeyafahamu. Suala la uwezo wa serikali ni jengine na uwezo wa Katiba na Kanuni za Baraza ni jambo jengine. Mhe. Naibu Spika, ninachokuomba kwa busara zako Baraza liamue hoja yangu na uzingatie hoja ya waziri na hoja yangu, ili Baraza liamue kwamba kuna haja ya kuongeza.

Kwa sababu hiyo bajeti huo uchumi ni kwa ajili ya wananchi na wananchi wanahitaji kusikia wawakilishi wao wanasemaje. Kwa hivyo, nia yangu ni kwamba kanuni iwekwe kando ili Baraza lijadili kwa upeo wake. Kwa mujibu wa kanuni hii ya 151 hoja huamuliwa na Baraza, ikijadiliwa ni kwamba tutakuja kanuni hii ya 151 kanuni ya (2) na ya (3).

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, kanuni ya 95 inasema kwamba siku 35 zitatengwa kwa ajili ya shughuli za Bajeti, lakini inaweza ikatolewa hoja ya kuongeza siku 5. Sasa hoja hii inapotolewa Mhe. Spika ndio mwenye mamlaka ya mwisho ya kuamua kwamba ile hoja iliyotolewa ina mantiki au haina uzito.

Lakini katika kifungu cha 151 Mhe. Naibu Spika, hii ni suala la kutenga kando kanuni. Mhe. Naibu Spika, unapoomba siku ziongezwe ni kwa sababu ya mjadala kama ni mkubwa sana na wewe umetumia *wisdom* yako ya kuongeza siku mbili leo.

Lakini napenda Baraza lako tukufu lione kwamba kuna baadhi ya wizara nyengine ambazo hazitohitaji hata siku mbili. Kwa mfano, wizara ambayo tuliipita jana ya Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais.

Sasa mimi ninachopendekeza na ambacho nahisi kitasaidia ni kwamba kwa sababu kuna wizara nyingi ambazo zinakuja mbele yetu na wizara hizi zinatofautiana, basi pale ambapo tutahisi kwamba wizara hii inahitaji zaidi ya siku moja na nusu iliyowekwa pale unaweza kutumia *wisdom* yako na kuongeza siku. Lakini kama kuna wizara ambayo haihitajii siku moja na nusu pale pia tunaweza tukafanya hivyo. Kwa maana hiyo, Mhe. Naibu Spika, si busara kutoa moja kwa moja kauli ya kusema siku 5 ziongezwe kama anavyotaka mjumbe.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, kwenye Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais siku kwamba kulikuwa hakuna wajumbe, wajumbe wengi walikatizwa na tuliombwa. Wajumbe wengi walikuwa na michango kwa ajili ya wananchi wa Zanzibar. Ninachoomba Mhe. Naibu Spika, suala la mapato ni jengine na suala la utaratibu wa kanuni na katiba ni jengine. Naomba busara zako kwamba Baraza liamue hoja yangu kama hakuna msingi nitaridhia maamuzi ya Baraza.

Mhe. Naibu Spika: Mimi nadhani bado mjumbe tusiwe na haraka kanuni haziruhusu, kanuni ya 95 tuendelee kwa siku 35. Tungekwenda kama zitamalizika bado wizara zipo tutatenga kanuni kando ili kumaliza wizara zetu kama tunavyofanya kwenye maswali na sehemu nyengine.

Ningeshauri tuendelee na kama muda utakwisha basi tutatenga kanuni kando tutaongezea ili tumalize majadiliano yetu. Nashauri tufanye hivyo.

Hivi sasa bado mapema ndio kwanza leo wizara ya tatu nashauri tufanye hivyo na wote watakaoletwa kuchangia watachangia. Kama sasa hivi nina watu 12 tu na tuna siku mbili. Kwa hiyo, Mhe. Mjumbe ningeshauri tuendelee kama ilivyo kanuni na kama hatukumaliza tutatenga kanuni kando ili tumalize kilichosalia. Kwa hiyo, naomba tuendelee na uchangiaji na naona waheshimiwa wengi walioleta majina wamekwenda kunywa chai. Sasa naomba tutulie tuchangie ili tuweze kufikia malengo kama alivyochangia Mhe. Hija Hassan Hija.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi asubuhi ya leo kutia baraka katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka 2011/2012.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kutujaalia leo roho zetu zikawa bado zimo katika hali ya kupumua. Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuwa tunapewa muda mchache lakini *inshaallah* tutautumia hivyo hivyo kuendeleza hoja zilizokuwa za msingi kwenye vitabu vya bajeti.

Mhe. Naibu Spika, namsifu sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa bajeti yake nzuri sana yenye mwelekeo wa kuwasaidia wananchi hususan wale wa vijijini na wa mjini.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuanza kuchangia naingia katika ukurasa wa 47 Mkoa wa Mjini Magharibi. Mhe. Naibu Spika, kwanza nimsifu Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi hususan pale anapojitahidi sana kuziondoa zile kero za wananchi ambazo kila siku zinapigiwa kelele na vyombo vya habari. Mhe. Naibu Spika, mimi ni shuhuda kumuona Mhe. Mkuu wa Mkoa akizitafutia ufumbuzi mzuri na kuzitatua lakini pili katika kusimamia miradi.

Mhe. Naibu Spika, nampa hongera sana Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi Mwenyezi Mungu amjaalie kila la kheri kwa kusimamia miradi hii kwa ufanisi kabisa bila ya ubadhirifu wa aina yoyote.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi ni mzee wetu wa miaka mingi ana experience nzuri sana katika utendaji wa Serikali hii ya Mapinduzi Zanzibar tumeona uadilifu wake. Lakini nimpe shukurani kubwa za dhati kabisa pale alipoisaidia Kamati ya Madiwani kuwapa sehemu ya kufanya kazi yao, nampa hongera kubwa sana.

Baada ya kamati ile ya madiwani kuwa hawana pahala pa kufanyia kazi, basi Mhe. Mkuu wa Mkoa walijipiga kifua akasema njooni mimi nitawapeni nafasi ya kufanyia kazi, hapo nampa hongera sana, kwa sababu alijua nini mantiki yake.

Mhe. Naibu Spika, niingie katika ukurasa wa 50, sitokuwa na fadhila, kwa nini na Mkuu wa Mkoa wangu nisimsifu, Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja. Mkuu wa Mkoa huyu nilifanya naye kazi karibu miaka mitano nilipoanza utawala wangu, tulikuwa tunashirikiana sana katika kuleta maendeleo kwenye shehia zetu na yeye nampa hongera kubwa sana ni mfuatiliaji mzuri na yuko tayari kuziondoa tatizo kero za hapa na pale hususan kero za viwanja, yuko karibu sana.

Mhe. Naibu Spika, hivi karibu tu ameanza kupanga programu nzuri na nimeiona. Aliwahi kumtuma Mhe. Mkuu wa Wilaya, tuliposhirikiana naye pamoja katika kulitafuta tatizo la hawa watu wa kule Matemwe Bangaloo kuweza kulitatua na tulishirikiana. Lakini yeye alisema kuwa hakuhudhuria kutokana na tatizo au majukumu ya hapa na pale na hilo nampa hongera kubwa sana, kusema kuwa Mkuu wa Wilaya nenda kwa utekelezaji. Hilo namsifu sana.

Jengine niseme kuwa ni msimamizi mzuri katika miradi. Hata juzi Mhe. Rais Dk. Shein alipotembelea, alifurahika kuona ni jinsi gani Mkoa wa Kaskazini Unguja ulivyokuwa unatumia uwezo wake wa kuviendeleza vikundi vya ushirika. Ushahidi tosha ni pale katika Skuli ya Fujoni. Suala hili nataka nimkumbushe mheshimiwa, wale waliokubali kutoa hapo kwa hapo msaada ule, mpaka leo kwa simu za hapa na pale nasikia bado fedha hazijafika.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mkuu wa Mkoa ajitahidi sana kuzifuatila fedha zile, ili wale waliokuwa hawajalipa basi walipe mara moja, kwa sababu ni aibu leo waziri kujitangaza mbele ya Rais kusema mimi nitatoa, tena pesa yenyewe ni Shs. 200,000/= halafu leo inafika miezi miwili fedha zile hazijafika kwa wahusika. Naomba Mhe. Mkuu wa Mkoa kama ulivyokua jamadari wa kusimamia mambo mengine basin a hayo nakuomba kwa dhati kabisa uweze kuyafuatilia ili kuweza kupata manufaa.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja hongera sana na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atakupa kila la kheri ili kuendeleza gurudumu hili la kuleta maendeleo kwenye mkoa wako.

Mhe. Naibu Spika, niingie kwenye ukurasa wa 58 kuhusu Baraza la Manispaa. *Alhamdulillah Rabil Alamina* tulimshukuru Mwenyezi Mungu kuwa bajeti hii ya Mhe. Dk. Waziri Mwinyihaji ametueleza ni jinsi gani amekusudia mara hii mji wetu kuvitafutia vitendea kazi vya kisasa ili angalau tuwe na asilimia ndogo sana, ya kuwa angalau nchi yetu isinuke. Kwa sababu hali ya uchafu inapelekea nchi kunuka.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri utakapopata fedha unazoziomba kwenye kitabu kiki, basi tuhakikishe kwamba mji wetu unaondokana na kadhia hiyo na fedha zitumike kwa mujibu wa utaratibu unaotakiwa.

Mhe. Naibu Spika, nimsifu sana Mhe. Meya Mstahiki ambaye ni kijana madhubuti kabisa kwa kuliongoza baraza lake kwa uwadilifu na kwa kutumia kanuni. Nampongeza sana pamoja na kamati yake teule aliyeiteuwa yeye kwa kufuatilia masuala ya hapa na pale, kwa kutaka kuliboresha au kulitengeneza baraza lake liwe zuri na liwe katika uadilifu wake unavyotakiwa. Nawapongezeni sana kabisa. Mhe. Naibu Spika, kwa sababu sisi ni viongozi wa *backbencher*, tunatakiwa kila tunaloliona tuishauri serikali, tuisaidie au tumsaidie waziri katika utekelezaji wake ili ufanisi wake uwe mzuri.

Hvi karibuni Mhe. Naibu Spika, kuna kijana wangu mmoja alinipigia simu kule Kitope, akaniambia mheshimiwa nasikia kuna ajira kule manispaa. Mimi nikamwambia sijui, kwa sababu ajira hazipitii Baraza la Wawakilishi. nikamwambia sijui, lakini kwa kuwa ni mwananchi wangu nikasema wacha nimsaidie ili katika kuondoa umaskini, nikasema nihangaike ili kijana yule aweze

kupata kazi Baraza la Manispaa, kwa sababu na yeye ni haki yake na ni Mzanzibari.

Mhe. Naibu Spika, nilihangaika kweli kutafuta. Nikaambiwa kweli ajira zipo, lakini zimo katika njia ya kinyemela, ni watu 40 tu ndio waliosajiliwa. Mhe. Naibu Spika, naomba niinukuu kanuni kidogo. Kanuni hii ni ya Baraza la Manispaa, jinsi ya uwezo wa kumpa Mkurugenzi na kuweza kufanya kazi hizo. Mhe. Naibu Spika, kuna kifungu cha 49(1)(2) cha kanuni ya Baraza la Manispaa, naomba ninukuu;

Kifungu cha 49(1)

> "Bila kuathiri sheria ya Baraza la Manispaa, sheria nyengine swali lolote linalotokana na mkutano wa baraza kuhusu kuajiriwa kazi, mshahara, hali ya utumishi au tabia ya mtumishi yeyote aliyeajiriwa na Baraza la Manispaa, litajadiliwa na baraza katika kamati husika, isipokuwa kama baraza litaagizwa vyenginevyo".

(2)

> "Waajiriwa wote wa baraza kama waajiriwa wapya au wanaitwa kwa uhamisho, ni lazima ipatikane idhini ya kamati ya sheria na utawala wa Baraza".

Mhe. Naibu Spika, twende katika kazi ya mkurugenzi. Kazi ya mkurugenzi. Katika wajibu wake Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa, atakuwa na madaraka yafuatayo.

- Kuangalia uendeshaji bora wa shughuli na kuona kwamba zinafanyika kwa utaratibu wa usawa kwa mujibu wa sheria, kanuni, bajeti na maagizo yanayotolewa na Baraza la Manispaa.

- Kulishauri baraza kwa uwadilifu kuhusu mambo yanayohusika na uajiri wa wafanyakazi, mishahara, upandishwaji wa vyeo na kufukuzwa kazi kwa utumishi.

Sasa Mhe. Waziri utanieleza utaratibu huu wa kanuni. Je, umetumika kuwapata hawa wafanyakazi 40. Kwa sababu inavyosemekana ujanja uliotumika mawaziri wengi ndio mliopata nafasi hizi kuwapeleka watoto wenu sehemu hiyo. Walala hoi hakuna hata mmoja, basi hata wawakilishi angalau kupewa nafasi.

Angenipa na mimi nisingesema hapa leo, ningesema ni sheria tu. Lakini sikupata, ndio huyo kijana nimehangaika naye mpaka nimekosa. Hivi kweli niende pale wakati nasema hivi Baraza la Wawakilishi, mawe, nisingepata hata siku moja Mhe. Naibu Spika.

Kwa hivyo, tuangalie Mhe. Waziri kwa kukupenda kabisa, baraza letu lile la manispaa limekuwa linakwenda tu kinyume na utaratibu, mheshimiwa ni hatari hiyo. Kwa sababu Baraza la Manispaa lile linaongozwa na viongozi wenye taaluma, linaongoza watu ambao maskini ya Mungu wanakwenda pale ili kuweza kupata mwelekeo wa baraza lao kila siku liwe katika hali ya kiuadilifu na utendaji wake. Lakini Mhe. Naibu Spika, kuna vurugu vurugu tu zinafanyika kila leo. Tukisema iwe balaa, lakini tutaendelea kusema, hakuna kuogopa.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri wewe ni shahidi wa sheria hii ndio uliyetia saini kwenye kwenye kitabu hiki, umo humu ulivyokuwa waziri mwenyewe, unanitizama. Mhe. Naibu Spika, tukienda katika ukurasa huu wa 20 jinsi gani Mkurugenzi anayehusika anaweza kutia mikataba yake. Humu kuna maeneo yanasema hivi, mheshimiwa naomba ninukuu kifungu cha 55.

Kifungu cha 55

> “Bila kuathiri masharti ya sheria ya Baraza la Manispaa la mwaka 1995, baraza linaweza kufanya mkataba wa kuzingatia utaratibu ufuatao. Wakati wowote ambao thamani yake ya mali kazi itakayoagizwa, haitazidi milioni 3”.

Mhe. Naibu Spika, mikataba inazidi fedha hizo na mikataba hiyo ina mengine ya milioni 170 ya Kinazini katika ujengaji wa nyumba zile, ina nembo ya karatasi ya manispaa, kuna mikataba ya Kwerekwe ambayo ina milioni kuanzia 63 na kuendelea mbele. Mhe. Naibu Spika, kuna mkataba wa *garden* pale. *Garden* la kuchekesha zaidi yule mtu kaambiwa alipe laki moja tu kwa mwezi, halipi na yeye kapendwa sana. Kwa sababu kuna laki tisa anachukua yeye kwa mujibu wa mkataba, laki tisa anajilipa yeye lakini laki moja tu kashindwa kupeleka. Suala hili Mhe. Waziri chukua hatua mara moja. Kama hawezi yule mtu basi funga ile *garden*, chukua mwenyewe. Kwa sababu hiyo laki moja aliyokubaliwa kwa mujibu wa mkataba na bado hataki kufanya kazi, ana mantiki gani.

Mhe. Waziri hiyo ndio hali ambayo nimetaka kukuambia leo hapa, ili tuangalie kanuni zetu zinavyofanyakazi, kwende na kanuni tusiende na malumbano. Tumefika pahala madiwani sasa hivi wanajigawa ndani ya baraza lao ni kitu cha aibu kwa nchi yetu. Wanachodai ni haki yao, kanuni hizi hapa kwa sababu ajira na wao walipaswa wasikilize wajuwe na waende kwa utaratibu.

Sisi hapa tunaye katibu wetu, akitaka kufanya jambo katibu basi ana kamati yake ya uongozi, mbona anatuita, jamani kuna hili na hili je mnasemaje. Kamati inaliridhia au kulikataa, kama imelikataa analiacha na kama imeliridhia analifanyia kazi, ndio utaratibu ulivyo. Lakini kama vyombo hivyo havikuweza kuhusishwa basi itakuwa kwa mujibu wa sheria itakuwa ni kosa kubwa sana linatendeka.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyokuambia mimi leo sitokuwa mkali sana, lakini tuangalie hali halisi ilivyo, kwa sababu leo natoa *lecture* tu, nafundisha jinsi gani kanuni zinataka zitumiwe kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa 61, sasa tizama hali ya hatari ilivyo. Mhe. Spika, juzi ulisema maneno mazuri sana hapa. Baraza la Manispaa litaanza mazungumzo, huko nyuma tayari mikataba ipo. Mheshimiwa tunapelekwa mahakamani sasa, hawa wenye mikataba mheshimiwa tutafanya vipi. Ulisema kuwa utazungumza moja kwa moja na makampuni yenyewe.

Mhe. Waziri, nakupa siri moja ya Zantel walipelekewa *bill* kubwa sana, ndio maana wakasema wanajiondoa. Kama hili hujalipata Mhe. Waziri basi litafute hilo. Walipelekewa *bill* kubwa sana hawa Zantel na manispaa, wakasema hii! Hali hii hatuwezi kulipa, sijui kama sio milioni 700 kitu kama hichi, ndio wakaona wajiondowe wao wawatafute wafadhili wawaweke kutangaza jina lao.

Lakini Mhe. Naibu Spika, huyu ni mtoto wetu Zantel. Mimi hili neno Tigo nikilizungumza wenyewe wataalamu wakisikia ninazungumza neno Tigo watanipigia makofi, kwa kuwa hata ile kuisema Tigo mimi naona haya. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, Zantel ni ubia wetu, anatusaidia kodi zetu kwa asilimia kubwa sana. Kwa hivyo, ni lazima tuangalie. Mimi ninavyoona hili suala hebu tulitafutie utaratibu wa kuweza kuwasaidia hawa ili tusiingie hatiani kumpa tabu Mwanasheria Mkuu wetu ambaye ni bado mpya, sio mpya wa sheria hapana, ni mpya wa Baraza. Itakuwa kila siku tunampeleka mahakamani tu, haiwezekani.

Naomba kabisa tulizingatie. Fikra zangu ninazokuambia Mhe. Waziri kaa chini tena ulizingatie kwa makini kabisa ili ulitolee ufanisi mzuri. Mhe. Naibu Spika, tusifanye jazba ya kusema kuwa haa! Tuondoshe. Mahakamani tunaelekea na tutalipa pesa nyingi,

pesa zako zote za bajeti utamlipa mtu mmoja mweka mabango. Kwa hivyo, mimi naomba twende vizuri.

Mhe. Naibu Spika, naomba niingie ukurasa wa 65 Halmashauri ya Kaskazini B. Mhe. Waziri nikupe hongera umetuletea kijana mzuri sana, mpenda maendeleo ni muda mchache tu makusanyo yake yameshafika milioni 200 hata ule muda uliomwekea yeye keshapita zamani.

Mhe. Naibu Spika, anatufaa sana yule kijana, aligundua matatizo ya hapa na pale ni jinsi gani uvujaji wa mapato, sasa ameyafunga. Sio vibaya ukaletewa fitna, naamini hivyo, kwa sababu kawaida yetu siku hizi ukisema sana unaambiwa yule siye, unaambiwa yule hivi na hivi na ukiwa mtendaji sana utapewa kila aina yamajungu, kwa sababu anatekeleza kazi yake kwa mujibu wa sheria.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri kijana huyu anatufaa sana, tena sana kabisa. Ningekuwa mimi ndio Dk. Shein basi ningempa Ukurugenzi wa Manispaa, lakini bahati mbaya naitwa Makame Mshimba Mbarouk Mwakilishi wa Jimbo la Kitope, sina mamlaka hayo, sijui mwenzangu Mhe. Makamo wa Pili kama atanisikiliza hii hoja yangu ikoje. Kwa kweli anafanya kazi vizuri sana.

Mhe. Mjumbe fulani: Umepokea pesa nini?

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Sijapokea pesa bwana. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli kijana huyu anafanyakazi vizuri sana. Kwa sababu mimi namsifu mtu ambaye anafanya utekelezaji kabisa. Kwa nini mtu sifa yake asipewe. Dk. Mwinyihaji nimekusifu hapa kutokana na bajeti yako nzuri na inamuelekeo mzuri, ni haki yako hiyo ni lazima nikusifu. Sio vibaya pia kukuambia Mhe. Dk. Mwinyihaji tai yako imekaa upande, ndio wajibu ulivyo ni haki yangu kukuambia, na ndio *backbencher*

ilivyo. Kwa hivyo, na yeye kijana wangu anafanyakazi vizuri kwa mujibu wa utaratibu.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nawaomba Wakuu wa Mikoa hizi halmashauri wasizitie mikono, wawaachie watumie sheria zao walizopewa, tusiwatie maneno kila mara, hapa na yeye ana mamlaka yake huyu. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wakuu wa Mkoa waacheni makatibu wetu wafanye kazi zao kwa uwadilifu kabisa, tusiwabughudhi. Mhe. Waziri ikiwa kama tutaendelea kuwabughudhi hawa, basi si dhani kama utendaji utakwenda vizuri, watakuwa wanaogopa tu.

Sasa mimi naomba Wakuu wa Mikoa tuwaachie wafanye kazi zao kwa mujibu wa utaratibu, tuone jinsi gani halmashauri zetu zitakapofanyakazi na kuweza kuleta maendeleo katika jamii, kwa sababu zinatusaidia na zinatufichia siri sisi wawakilishi na wabunge, pamoja na wizara husika. Kazi za Serikali Kuu wanazifanya wao, kwa sababu wao tayari ni sehemu ya Serikali Kuu.

Mhe. Naibu Spika, niingie katika ukurasa wa 79. Mhe. Waziri juzi ulinijibu swali, kwa kweli niliondoka mnyonge sana sikufurahika nalo. Nini mantiki ya JKU Mhe. Waziri. Mantiki yetu Mhe. Waziri ni Jeshi la Kujenga Uchumi. Dhana kubwa ni kuwakusanya vijana na kuondoa hisia mbaya mitaani na kuwaweka pale na kuwaweka katika hisia mbayo yenye kutafuta njia ya utegemezi, yaani ya kujitegemea.

Juzi mimi nilipiga kelele sana suala la JKT. Mhe. Waziri mimi sijaridhika nalo hili suala la JKT hata kidogo. Uliniambia haya ni wenzetu, kule wanafanyakazi nzuri, wanapata kazi za ukulima, kazi za uchngaji na mambo mengine. Sasa leo naona humu umenionesha wewe njia hii hapa mheshimiwa kuwa JKU inafanya shughuli hizo hizo ni sawa sawa na wale. Nilichogundua Mhe.

Waziri hamtaki kutoa posho, basi hakuna chengine chochote. Kule Bara wenzetu wanatoa posho shilingi hamsini, lakini nyinyi hamuwapi fedha hawa ya kukimu haja, hata ile sabuni sijui kama wanapewa Shs. 5,000/= ni aibu.

Mhe. Naibu Spika, tuna bonde kubwa sana Bambi na hatujalifanyia chochote, tunawachukua tunakwenda kuwapeleka kwa wenzetu. Mhe. Naibu Spika, suala hili mimi bado sijakubaliana, linanikereketa akili.

Juzi nilikwenda pale JKU, nilisema ilivyokuwa mimi ni mwakilishi niende kule nikatafute nafasi, ili wananchi wangu waweze kupata nafasi ya kuweza kwenda huko JKT, ili wanieleze wakirudi kuna nini huko. Lakini hatimaye nilipokwenda pale hizo nafasi zenyewe nimeambiwa chache. Lakini kila unayemuona kaletwa na Waziri Juma au kaletwa na Waziri Asha.

Mhe. Naibu Spika, mimi niliambiwa Mhe. Mjumbe utapata nafasi moja. Sidhani kama ile nafasi itapatikana, kama imepatikana sawa, haikupatikana nimesamehe. Lakini kwa nini Mhe. Waziri iwe hivyo. Jeshi letu lazima hili tulisaidie kwa jitihada zote, tunaomba fungu hili ulilloomba ni kidogo halitoshi kwa JKU tusidanganyane. Vyengine vyovyote vile, ondoa skuli ile, ondoa mashamba yale, ondoa skuli ya ufundi na ondoa kila kitu bora tusiwe nayo kabisa JKU. Ubaya zaidi wanakwenda kule vijana hawarudi tena. Awamu iliyopita wamekwenda sikumuona hata kijana mmoja kurudi, tumeshakuwa na wingi wa watu sasa tunagawa watu. Isitoshe hatuna tahadhari kama wale tunakwenda kuwapa mafunzo ya ujeshi, tunajitayarisha pahala pabaya sana hatujaiangalia ile wizara Mhe. Dk. Mwinyihaji.

Tunawapeleka kule makundi kwa makundi, hatimaye hatuna udhibiti wa kuwapa kazi tunawaachia tu, ujambazi unazidi kuteketea wakishajua silaha hizo unafikiria vipi. Hebu serikali tulizingatie hili, kama hatuna pesa basi mimi niko tayari posho

langu kulipeleka kule. Kama hatuna pesa Mhe. Waziri niko tayari posho langu la hii *sitting allowance* hapa kulipeleka kule. Hii ni hatari, tusifanye masihara kwa sababu ni vijana wengi sana huko wanatembea tu hivi hivi, wengi wamesharudi huko lakini hawana fedha ya aina yoyote, hawana kazi ya aina yoyote. Karudi ana ufundi wa umeme, basi mpeni vifaa

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe dakika zao 20 zimekwisha, nakuongeza dakika tano ili umalizie.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: sawa. Nakwenda katika sehemu ya KMKM. Mhe. Naibu Spika, KMKM ni kikosi chetu kizuri sana. Tunaomba Mhe. Waziri uwape zana za kisasa ili waweze kujisaidia na kuweza kuondoa ugaidi wa baharini wa uvuvi haramu.

Vile vile hapa kuna tatizo la mfanyakazi mmoja anaitwa Said baba yake mimi simjui, anakaa Mfenesini amefukuzwa kazi na aliomba mwenendo wa ufukuzaji kazi kwa mujibu wa barua mpaka leo hajapewa. Naomba Mhe. Waziri na hili uje kunijibu vizuri, hata onyo lile anasema hajapewa, lakini kajishtukia kafukuzwa kazi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri suala hili tunaomba usaidie, amepeleka tume na kila pahala barua lakini hakuna jibu lolote.
Kwa kumalizia Mhe. Naibu Spika, usinisimamishe naingia Chuo cha Mafunzo. Mhe. Naibu Spika, ilikuwa hapa tunapewa muda wa dakika 30, unanipa dakika 20. Mhe. Naibu Spika, mwenzangu wewe nimekupigia debe.

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa 82 Chuo cha Mafunzo, nimsifu sana Kamishna ambaye hajawa moja kwa moja Kamishna. Ana mtandao mzuri sana wa utekelezaji wa kazi, hususan mbali ya wafanyakazi wake na mpaka wale wa nje ambao wananchi raia wema wa Zanzibar. Ametafuta kitu kimoja kizuri sana hata mimi nimekinukuu na nimefurahi. Ana mradi wa

kuwajengea watu nyumba kwa njia ya mkopo, ni suala zuri sana, mimi sijapata kuona suala hilo, hongera sana Mhe. Mwinyihaji.

Nilikwenda siku moja kwenye sehemu moja, nikasikia mtu mmoja anaambiwa, wewe vipi mama. Akasema mimi nashukuru Alhamdulillah Kamishna aliyekuwepo sasa hivi, nimepata mkopo wa kujengewa nyumba. Nikasema hii neema kwa Zanzibar, ile Afisi ya Majenzi yenyewe haijapanga *plan* hiyo, lakini idara hii imeweka. Kwa kweli mimi namsifu sana Mhe. Waziri. Tena wewe unajua vya kufanya, neema kama hiyo sidhani kama hutomwambia kuwa apate Ukamishna moja kwa moja, sidhani kama Mhe. Waziri hutompigia debe mtu kama huyo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nashukuru sana na japo nimepewa muda mdogo, lakini nilikuwa nina mengi Mhe. Waziri, lakini wakati, nataka niwape wenzangu na hasa leo ilivyokuwa sijanywa chai.

Kwa kumalizia niseme Mhe. Naibu Spika, naunga mkono kwa asilimia 50, baada ya kuja kunijibu suala la ajira la hao vijana. Sitaki nizuie, nasema kuwa zitowe ziende zipite kwenye *channel* ambazo zinahusika kwa mujibu wa kanuni hii inavyoeleza, tufuate kanuni hii, kwa hapo mimi Mhe. Waziri niko pamoja na wewe. Kwa hayo machache, wananchi wangu wa Jimbo la Kitope tunaunga mkono kwa asilimia 50, ahsante sana Mhe. Naibu Spika.
Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii kuweza kutoa mchango wangu kuhusiana na makadirio na mapato na matumizi ya Wizara hii ya Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Kwanza namshukuru Allah kwa kutupa uhai, uzima na *tawfiq* ya kuweza kuzungumza katika kikao hiki. Vile vile napenda nimpongeze Mhe. Waziri kwa uvumilivu wake wa kuweza kusoma kwa muda wa masaa mawili na robo bila ya kuvuta pumzi. Kwa kweli kwa umri wake na alivyosoma anastahiki pongezi, labda ana mazowezi mwenzetu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda nianze na mada ya Chuo cha Mafunzo. Nilikuwa nikisema katika miaka mingi iliyopita, nashukuru kwamba Mhe. Waziri katika kitabu chake hiki ametumia kurasa nyingi za kueleza jinsi Zanzibar inavyoshirikiana kikanda na kimataifa na mataifa mbali mbali. Kuanzia ukurasa wa 65 mpaka 79, Mhe. Waziri anazungumza juu ya namna gani Zanzibar inavyojishirikisha katika shughuli za kikanda na shughuli za kimataifa.

Mhe. Naibu Spika, katika kujishirikisha huku ni lazima tubadilike, tusiende kujishirikisha katika mataifa mengine ya kikanda na ya kimataifa, lakini sisi wenyewe tukabaki pale pale. Madhumuni makubwa ya kwenda katika mikutano hii na majadiliano na nchi mbali mbali na kuwemo katika mashirika ni kutufanya tubadilike.

Katika kitabu chake hiki Mhe. Waziri kifungu wa 71 alikuwa amesisitiza sana umuhimu wa mashirikiano haya. Anasema;

Kifungu cha 71

> "Mhe. Spika, naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba makubaliano hayo ni muhimu sana kwa manufaa ya Zanzibar".

Sasa Mhe. Naibu Spika, siku moja sisi tulialikwa katika kikao, nilipata mualiko katika Baraza hili kuhudhuria kikao cha wadau wa afya, watengenezaji wa madawa ya binadamu, yaani *pharmaceuticals units* au *industry.* Wenzetu katika mabunge mbali mbali ya Afrika Mashariki walikuja Wabunge ambao wamo katika Kamati za Afya. Kwa hivyo, kulikuwa na *common thing* katika ule ujaji wao, yaani kila aliyekuja pale anatoka kwenye Kamati inayoshughulikia Masuala ya Afya, yaani *Public Health Committees* za Mabunge yale yaliyokuja.

Mhe. Naibu Spika, kwa bahati nzuri sisi tulikwenda ikiwa tunao ujuzi kidogo, lakini ikitokezea wakati kunataka kufanywa mabadiliko au kufanywa maamuzi, basi maamuzi haya yaende kwa mujibu wa yale mashirikiano yetu.

Kwa kweli mimi binafsi nilikuwa nikichangia sana kwamba tufikie wakati hiki Chuo cha Mafunzo tukiite kama kilivyo, yaani ni jela, kwa sababu hizi zifuatazo:-

Kwanza kila aliyepelekwa jela hakwenda kuandikishwa skuli, isipokuwa alipelekwa Mahakamani na Jaji akamuhukumu kwamba huyu ni mkosa. Kwa hivyo, akeshahukumiwa na Jaji kuwa huyu ni mkosa au anatuhumiwa kuwa ni mkosa apelekwe rumande, basi anapelekwa kule jela.

Pili katika vitabu vyetu vya sheria kila ambaye amefikishwa Mahakamani imeandikwa *by conviction to imprisonment* na *imprisonment* imo katika neno linaloitwa *prison*, yaani ni jela. Kwa hivyo, nadhani kuendelea kukiita Chuo cha Mafunzo, itakuwa tunakwenda kwenye mikutano pamoja na kushirikiana na wenzetu, lakini itafika wakati tubadilishe haraka mambo haya wakati hatupo tena.

Mhe. Naibu Spika, madhumuni ya kuanzisha Mhe. Marehemu Mzee Abeid Amani Karume ilikuwa sio jina, mimi naamini ilikuwa sio jina. Kwa kweli alianzisha utaratibu wa kwamba wale vijana au watu ambao ni wakosa wakenda kule, basi watakaporudi wawe na utaalamu fulani na wala wasijekurudia tena makosa yale. *(Makofi)*

Kwa hivyo, sisi tushughulikie na vile vitendo vya kuwafanya wale wanaokwenda kule waweze kusoma taaluma mbali mbali za kiufundi pamoja na za kiamali. Lakini tukumbuke kwamba hatuko katika ulimwengu uliojitenga peke yetu, isipokuwa ni lazima twende na wenzetu.

Vile vile suala jengine katika miaka ya 1960 hapa Zanzibar zaidi kulikuwa na skuli mpaka za sekondari. Kwa hiyo, vyuo havikuwepo na hivi sasa tunapotezana malengo, maana yake ukimwita huyu ambaye ametoka skuli, chuo pamoja na anayetoka jela wote ni mwanafunzi, kwa kweli tunababaishana.

Mhe. Naibu Spika, nadhani kwamba wakati tunakwenda katika Kongamano za Kikanda na Kiulimwengu, basi na hili tulibadilishe na tuliite vile vile ni jela. Sasa ikiwa hatukubali basi mimi siwalazimishi, lakini isijefika wakati humu tukaletewa mswada huu kwa njia ya dharura tukaambiwa upesi tubadilishe, kwa sababu kuna mambo yanatokea, basi nitajulikana siku hiyo kwamba ah! Alisema fulani hapa. Hilo la kwanza.

Pili huko unakuita Chuo cha Mafunzo ambako mimi sikubaliani nako na mimi nakuita jela. Mhe. Naibu Spika, wazungu wanasema "*call a spade a spade"*, yaani ikiwa pauro basi liite pauro na ukiliita jembe itakuwa hufahamiki. Mhe. Naibu Spika, tumeambiwa na watu waliokaa pamoja na waliokwenda kwenye kamati kwamba kuna matatizo kuhusu watoto wadogo wanaoingizwa jela au Chuo cha Mafunzo. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Waziri katika maelezo yake alitaja mpaka kumalizika kwa majengo hayo inategemewa mwaka 2014. Mhe. Naibu Spika, watu wa zamani walisema kwa Kiswahili "Mngoja maiti hungoja akilia". Kwa hivyo, watoto wale watakaokaa katika mazingira kama hayo mpaka mwaka 2014, watakapotoka ni watoto tena na kila atakayetoka atakwenda kumuambukiza mwenzake.

Mhe. Naibu Spika, nadhani kwa suala la watoto hususan ile Sheria tuliyoipitisha hivi karibuni ya Kulinda Haki za Watoto, asijekufikia wakati Mhe. Waziri akafikishwa Mahakamani kwa kuvunja Haki za Watoto. Kutokana na hali hiyo, isijekufika

wakati ikawa yule aliyefikishwa Mahakamani mwanzo kwa kuvunja zile Haki za Watoto ni Mhe. Waziri wa wizara hii.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, aliangalie suala hili kwa mamepa mno, ili wale watoto wanapelekwa jela wapate sehemu yao na waweze kwenda kama watoto walivyo katika dunia. Hilo la pili.

Suala la tatu Mhe. Naibu Spika, nataka niingie katika utendaji wa Baraza la Manispaa kidogo tu. Mhe. Mjumbe wa mwanzo aliyeanza kwa kweli Mhe. Naibu Spika, Baraza la Manispaa kuna tatizo na kwenye kitabu chake Mhe. Waziri kifungu cha 116 ukurasa wa 61 Mhe. Naibu Spika, naomba kunukuu.

Ukurasa wa 61 kifungu cha 116 kinasema hivi:-

> "Baraza la Manispaa limeanza mazungumzo na Makampuni ya simu ya *Zantel* na *TIGO,* ili kujadili utata uliojitokeza katika Mikataba iliyofungwa baina ya Baraza la Manispaa na Kampuni za matangazo ya biashara ambazo zinaifanyia kazi Kampuni hizo pamoja na mabadiliko ya Sera za utakelezaji wa mradi wa ZUSP katika utekelezaji na uwekaji taa za barabarani.
>
> Baraza la Manispaa linakusudia kufanya mikataba moja kwa moja na Kampuni hizo mama za simu badala ya kupitia Kampuni za Matangazo. Hatua hii itajenga uhusiano mzuri wa kibiashara na Kampuni hizo. Hivi sasa uwekaji wa mabango ya biashara utajadiliwa kupitia Kamati husika za Baraza la Manispaa".

Mhe. Naibu Spika, kuonesha kwamba ina maana huko nyuma zilikuwa hazijadiliwi, yaani hii inaonesha wazi wazi. Lakini

niseme sisi au mimi nilikuwemo kwenye kikao cha Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi tuliowataka hawa watu wa Manispaa kutueleza nini kilichotokea baina yao na *Zantel* hata ikawa kuna matatizo hayo.

Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, fikra hii ndio iliyokuwa mwanzo, lakini kupitia kwa Mkurugenzi wa Mipango Sera na Utafiti hivi sasa ambaye yupo Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na yeye ni mjumbe wa Bodi ya *Zantel* kutoka serikalini. Hivyo, alisema kwamba *Zantel* walipeleka ombi lao na wakatakiwa watoe zaidi ya shilingi milioni 700 kwa mwaka kwa kupachika mabango, wakati walipoajiri kampuni walitakiwa watoe shilingi milioni 5.

Sasa namuuliza Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, hivi kurejea tena kwenye makampuni moja kwa moja watatozwa zile shilingi milioni 700 au watatozwa kiwango ambacho kinakubalika na Baraza la Manispaa kikawaida.

Mhe. Naibu Spika, mwanzo walipeleka ombi lao wenyewe, lakini hawakukubaliwa, maana yake waliambiwa watoe shilingi milioni 700 kwa mwaka. Kwa hivyo, Mhe. Waziri namuomba sana kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba Baraza la Manispaa lina matatizo, kwa sababu sisi wametuletea barua mbili tofauti tena kwa sehemu hiyo, yaani barua moja wanawapa *Zantel* na nyengine *TIGO* na eneo hilo hilo na sisi barua hizo tunazo kama kamati. Sasa kwa sababu kuna tatizo, basi lichunguzwe na wale ambao wataonekana na hatia waadhibiwe ndio uwajibikaji, lakini kukiwa na tatizo tunalinda tu, basi litakuwa lako Mhe. Waziri kama unawalinda hao wengine.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho atueleze baada ya mkasa huo, pia yeye mwenyewe alitueleza hapa katika Baraza kwamba ameunda tume yake na taarifa tulizonazo Mawidani

kupitia vyombo vya habari waliunda tume yao. Mhe. Naibu Spika, watueleze nini kilichoonekana na hatua gani zilizochukuliwa.

Mhe. Naibu Spika, katika Bajeti ya Serikali tuliletewa miradi ya Manispaa za Unguja na Pemba pamoja na ile ya Mabaraza ya Miji ya Wete na Chake Chake na Mkoani. Kwa kweli aliyekaa kitako na kugawa hajulikani ni nani, lakini kwenye miongozo ya utaratibu wa kibajeti ni kugawa rasilimali kwa uwiano mzuri.

Sasa itakuwaje bilioni 39 zitolewe kwa Mji wa Unguja na bilioni 3 tu zitolewe kwa Miji yote ya Pemba na wala si hivyo tu hizo bilioni 3 ziko za ziada zinaambiwa za uendeshaji, yaani *administrative costs* za Manispaa ya Unguja.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, aje atueleze ni kigezo gani kilichotumika kwa ajili ya kugawa bajeti hii katika uwiano huu.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu tayari zimeshagaiwa basi Mhe. Waziri anaweza kujitetea. Sasa je, kitakachokuja mwaka 2012/2013 kitaanza wapi, yaani tukubaliane hapa, kwamba mara hii tumegawa hivi, lakini kitakachokuja tunaanza huko ambako hakukugaiwa, kwa sababu na ile Miji inahitaji fursa kama inazopata miji mingine.

Hivi sasa kuna matatizo ya uhamaji wa watu, tunaambiwa wanavamia Mji wa Unguja. Lakini ikiwa fursa huwapelekei watakaa, hawatokaa na watakimbilia pale kwenye fursa. Kwa hiyo, wakati wa kugawa hizi rasilimali basi tuangalie uwiano baina ya mji kwa mji au kisiwa na kisiwa ama mkoa kwa mkoa, ili zile fursa zikienea watu hawawezi kufanya *Town Migration*, ambayo ikasababisha matatizo makubwa ya uendeshaji wa miji.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwa Madiwani. Mhe. Naibu Spika, Madiwani wamepiga kelele siku nyingi sana, mimi

tokea niingie katika Baraza hiki ni kipindi cha pili. Kwa kweli serikali bado haijawatamkia madiwani wamewaweka nafasi gani, nadhani mara hii Mhe. Waziri aje atueleze hawa Madiwani kwa mujibu wa Utawala Bora hawa ndio waliochanguliwa na wananchi na wangepata stahiki nzuri zaidi, kwa sababu ni wachaguliwa na wananchi.

Kwa nini hawapati stahiki zao kutoka serikali hii na ule wasi wasi uliokuwepo hivi sasa umeshaondoka na tunayo Serikali ya Umoja wa Kitaifa, ambayo imeondoa kila aina ya kuoneana na tunashukuru sana, kwa nini wabakishwe Madiwani tu, basi keki hiyo ndogo ambayo tunayo basi tukatiane na wao, ili waweze kujisikia. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe dakika 20 zimekwisha nakupa dakika 5 za kumalizia.

Mhe. Rashid Seif Suleima: Ahsante Mhe. Naibu Spika, namalizia. Kwa kweli mimi sina *interest* au sina kitu ndani ya Kikosi cha Zimamoto, yaani hamna ndugu yangu wala mwanangu, lakini naona huyu Mhe. Waziri anakichukia hiki kikosi sijui kwa nini hakipendi. Sasa ametueleza mwenyewe hapa majanga zaidi ya mia moja ambayo yametokea. Kwa mfano, tukiangalia ukurasa wa 85 kuna majanga mbali mbali ambayo yametokea naomba kunukuu Mhe. Naibu Spika.

Ukurasa wa 85 kifungu cha 189 kinasema hivi:-

> “Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, kikosi kimeripotiwa jumla ya matukio 258. Matukio 129 ni ya moto wa majumbani na mahoteli ya kitalii, matokeo 55 ni ya moto wa misitu na mashamba, matukio 30 ni ya moto wa *transformer* za umeme, matukio 12 ni ya moto wa gari, matukio matatu ni ya moto wa uongo pamoja

na matukio 29 iliyohusisha uokozi wa watu na wanyama walioingi katika visima na mashimo".

Lakini tukiangalia bajeti yake mwaka jana ilikuwa kama hivi na pia nilisema. Kwa kweli bajeti yake shilingi bilioni 1,883/-, lakini KVZ ni bilioni 2,453/-. Sasa kile Kikosi cha Zimamoto na Uokozi ambacho kinashughulikia matukio yote haya bajeti yake ni ndogo kuliko KVZ, hivi kuna nini. Mhe. Naibu Spika, huku KVZ pamoja na mambo yote kama kweli mnaipenda basi hamuifanyi angalau ikawa sawa, yaani KVZ pamoja na Kikosi cha Zimamoto na Uokozi zikapewa bajeti sawa.

Sasa Kikosi hiki cha Zimamoto na Uokozi pamoja na majukumu yake yote basi bajeti yake ni hii ambayo ni ndogo. Lakini jambo la kustaajabisha zaidi haitakiwi hata inunue *spanner*, yaani haikutiliwa hata *zero* shilingi kwa ajili ya maendeleo, wakati KVZ imepewa shilingi milioni 100/- kwa ajili ya maendeleo.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba atueleze kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba hiki Kikosi cha Zimamoto na Uokozi hapa Zanzibar ni mtaji kwamba majumba yaungue moto yamalize, mahoteli yaungue moto yamalize, yaani ni mtaji wa watu wengine.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana na naomba niunge mkono bajeti hii iwapo masuala yangu yatajibiwa vizuri na ninamhakikishia Mhe. Waziri utamsaidia. *(Makofi)*

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Naibu Spika, na mimi kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametiwezesha kuwa katika hali ya uzima na kuja hapa kwa mantarafu ya kutathmini na kujenga mazingira ya taifa hili. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spiak, pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa hotuba yake mwanana ambayo kwa kweli imejieleza vizuri sana. Vile vile niwapongeze watendaji wake ambao wamemsaidia katika shughuli hii ya uandaaji wa hotuba hii. *(Makofi)*

Lakini kwenye mame na mabaya hayakosi na dhamira hasa ya vikao vyetu hivi ni kuisaidia serikali Mhe. Naibu Spika, si kumkomoa mtu na wala kumsema mtu au kumjadili mtu kwa madhumuni mabaya. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwanza nizungumzie kuhusu Vikosi vyetu vya SMZ. Kwa kweli nichukue nafasi hii kwa kuvipongeza Vikosi vyetu vya SMZ na hasa KMKM kwa jinsi inavyofanya shughuli zake kikamilifu, kwa sababu mtu anapofanya vizuri basi mpe sifa yake. Mhe. Naibu Spika, nakipongeza kikosi hiki na nakitakia kila la kheri. *(Makofi)*

Pamoja na hayo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba awapatie mahitaji ambayo kwa kweli ndiyo yatakayowawezesha kukamilisha majukumu yao. Mhe. Naibu Spika, nawaombea kikosi hiki kwa kweli kionewe huruma kwa sababu kinafanyakazi katika mazingira magumu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sasa nije katika Vikosi vyetu vyengine kama vile JKU, Chuo cha Mafunzo navyo pia niviponge. Hapa nataka kutoa ushauri Mhe. Naibu Spika, kwa sababu Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tunataka kuleta mageuzi ya kilimo, basi ni vyema vikosi hivi viwili na wao kugeuziwa mageuzi ya kilimo ndani ya taasisi zao na uwezo huo upo, kwa sababu wanayo maeneo makubwa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naomba sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, itakapohakikisha kwamba bajeti hii imekaa vizuri, basi vikosi hivi vya JKU pamoja na Chuo cha Mafunzo vionewe imani. Kwa kweli vikosi hivi vina majukumu

mbali mbali katika taasisi zao. Hivyo, navipongeza vikosi hivi kwa nia moja kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sasa nije kwa mtoto ambaye hana baba wala mama Kikosi cha Zimamoto na Uokozi. Kwa kweli mimi naweza kusema kuwa kikosi hiki hakina baba wala mama na wenzangu wameelezea hapa kuwa tunaiona kikosi hiki ni kidogo sana.

Lakini hiki ni kikosi muhimu katika nchi na hapa liliulizwa swali na mimi niliuliza swali la nyongeza na nilisema jamani hivi sasa imefika wakati kwamba kila mkoa angalau kuwa gari ya zimamoto. Kwa mfano, linalotokezea janga na kutoka gari ya zimamoto kutoka Mkoa wa Mjini hata itakapofika kule basi hilo janga tayari limeshamaliza kila kitu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naiomba sana serikali kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba tubadilike twende na wakati. Mhe. Naibu Spika, lazima tukubali kuingia harara kwa mambo ambayo ni muhimu kwa jamii kwa jumla. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu Mhe. Naibu Spika, nimesema kwamba tunavyo vikosi vyetu, taasisi ambazo kwa kweli zinatufanyia kazi vizuri tu na nitazitaja. Kwa hivyo, naiomba serikali kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwa moyo mkunjufu kabisa tuache kununua *furniture* kutoka Dar-es-Salaam na sehemu nyengine, ili tuweze kuokoa fedha za serikali. Kwa kweli vikosi vyetu vinafanyakazi nzuri sana za *furniture*. Hivyo, naiomba serikali kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwa udhati kabisa, ili tuvipe vikosi vyetu pamoja na vijana wetu waweze kupata ajira Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, samani za bei kubwa wakati tunao uwezo wa kutengeneza samani ambazo ni nzuri, miti yake pia ni mizuri kuliko kwenda kuchukua nyumba za panya na kuzitia katika maofisi.

Kwa kweli hili naiomba serikali kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kama tunavyofanya mawasiliano kwa Karakana na kutoa maelekezo hapa kwamba gari zote za serikali zipelekwe kwenye Karakana ya Serikali ingawa haijachukuliwa hatua kiasi hicho.

Sasa naiomba serikali kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba samani za mawizara zote tutoe *order* katika Vikosi vyetu ambavyo vinatengeneza samani nzuri na hata majenzi tunaona jinsi wanavyojenga vizuri tena kwa nia safi kabisa ya kuisaidia serikali. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo sasa niende Baraza la Manispaa na wenzangu wamezungumza waliotangulia na mimi ninayo haki ya kuzungumza. Kwa kweli namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba ajikaze na Baraza la Manispaa si hivyo litamuweka upande, kwa sababu sisi lazima tumwambie Waziri husika. Hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, akae na Baraza la Manispaa kwa ajili ya kupanga mipango ya kuuweka mji huu katika hali ya mazingira mazuri. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nimetembelea masoko yote. Kwa mfano, katika Soko la Malindi na wengine watakuwa mashahidi hapa, mazingira ya soko hilo kwa kweli hayaeleweki, yaani ukipinda tu pale basi yule samaki atakuchukia tena ni sehemu ndogo sana na watu wanalipa Mhe. Naibu Spika. Hivi kuna kikwazo gani cha kuweka watu maalum kwa ajili ya kusafisha pale, pia soko hili ni dogo na wala halitoshelezi. *(Makofi)*

Lakini kubwa zaidi watu wanatoka sehemu mbali mbali kwa ajili ya kukusanyika nje, sasa wale wanaolipa kodi wanapata shida, kwa sababu watu wanauza nje na Manispaa ipo inaona. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu

Spika, hebu tubadilike katika mambo ambayo uwezo tunao. *(Makofi)*

Tukija Soko la Darajani kwa kweli hili ndio halisemeki. Mhe. Naibu Spika, katika soko hili ukienda sehemu ya kuuzia kuku *Wallahi* Mwenyezi Mungu anatulinda kwa mengi. Lakini kuna uchafu ambao umekithiri na Manispaa wanajaribu kujenga, isipokuwa nina wasi wasi Mhe. Naibu Spika, wale watu ambao ni Wazalendo tokea lilipoanza soko lile sijui hayo majenzi au hivyo vibanda vinavyojengwa kama watapewa wao. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba ahakikishe suala hili linasimamia kwa udhati kabisa, si hivyo kipindi kinachokuja tutazungumza vyengine katika kikao cha Baraza hili. Kwa maana hiyo, lazima tuwape haki watu ambao wamehamia tokea mimi mdogo niko hapa na leo kwa kuwa mtu anazo fedha zake na tayari limeshatengenezwa, ndio anapewa na kuachwa yule ambaye aliyeanzilisha na kuweza kuhangaika kwa mvua na jua akakoseshwa nafasi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nimetoa wito kwenye Kamati yangu kwamba nitakuwa mkali kwa hili na nitalifuatilia kwa karibu zaidi. *(Makofi)*

.
Mhe. Naibu Spika, nije soko la Mombasa kwanza tuwashukuru sana wenzetu wa China ambao walitujengea soko lile kwa dhamira nzuri sana, lakini niseme kwamba lile soko limekufa madhumuni hasa ya soko lile haipo na zamani ilikuwa vyakula vyote vya nafaka vinakwenda kwenye soko lile, lakini leo Mwanakwerekwe imekuwa imebeba mambo yote.

Namuomba Mhe. Waziri kwanza soko lile kuna tangi la maji ambalo linasaidia mpaka mitaa yote pale pampu tu imeachwa na

kisima kipo, namuomba Mhe. Waziri alifuatilie suala hili na pale sio pa kuuzwa mitumba Mhe. Naibu Spika, soko lile kwa ajili ya mboga mboga na nafaka nyengine kama Michele, njugumawe, kunde na vyenginevyo, watu walikuwa wanatoka bara *centre* yao ni pale tumeliua soko kwa mitarafu ya kuwa kule hakuna chochote watu wote wako Mwanakwerekwe. Naliomba na namuomba Mhe. Waziri suala hili alifuatilie ili lile soko lifufuke tusibeze misaada tunayoipata.

Mhe. Naibu Spika, nije Mwanakwerekwe ndio huko majaa yote yako huko, siku tuliyosema tunakwenda palisafishwa pale nje pakawa safi nenda sasa hivi ukaangalie kila kitu kipo nje pale, kule ndani kuna maturubali mengine yamechanika mengine yamewekewa miti yanafyatuka, maana yake hakuna mpangilio wa aina yoyote kuhakikisha kuwa lile soko liko katika hali nzuri.

Mhe. Naibu Spika, kumewekwa sehemu ya nyama lakini kuna tajiri mmoja ametoa pesa amejenga nje pale ameshatia kila kitu, namuomba Mhe. Waziri pale pasiuzwe nyama kwa sababu anawadhulumu wenzake ambao wamehamia miaka na miaka ndani kule kuuza nyama, yeye kaja kaonyesha pale na mambo yake yote na mafriza, mafeni, ma *air condition* tusifanye mambo kwa kuwadhalilisha wale wengine waliokuwa hawana uwezo.

Mhe. Naibu Spika, soko la Mwanakwerekwe kwanza nimpongeze sana pamoja na mambo yote lakini nimpongeze sana Mkuu wa soko la Mwanakwerekwe pale ambae anashughulikia ni mtu wa Manispaa huyu, kwa kweli anasikilizana sana na wafanyakazi wa pale na wafanya biashara wa pale, naiomba Wizara kupitia kwa Mhe. Waziri kamati yangu imekwenda imeshajihisha ili watu wajiunge katika ushirika, wako tayari na Wizara husika ya uwezeshaji imeshafanya baadhi ya mambo kukamilisha pale.

Sasa naomba sana Mhe. Waziri na yeye alifuatilie hili kwa karibu ili lile soko likae kama soko na uchafu, nje pale Mhe. Naibu

Spika, hebu tufuatilie haya mambo kwa karibu tutoe madhumuni hasa ya soko lile, ukenda pale *packing* hamna, uchafu moja kwa moja mabaskeli yamekaa ndivyo sivyo na ile ni njia kuu ambayo ni hatari tupu. Namuomba Mhe. Waziri hilo alifuatilie.

Mhe. Naibu Spika, nije katika mambo ya *maintenance* tatizo tulilokuwa nalo Mhe. Naibu Spika, tulirithi majengo mengi na sasa hivi tuna majengo yetu wenyewe baadhi, lakini tatizo tulilonalo ni matengeneo tunaacha mambo mpaka yanamalizika badala ya kujenga ufa tunakuja kujenga ukuta. Namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwake kuwe na utaratibu maalum wa kupitia majengo yetu yote ya serikali tuangalie wapi panahitaji matengenezo makubwa na wapi panahitaji matengenezo madogo ili kuokoa fedha za serikali.

Nimeshazungumza vya kutosha lakini la mwisho Mhe. Naibu Spika, nina wivu lakini wa kimaendeleo sio wa husda, Mhe. Ismail Jussa Ladhu juzi aliuliza suala kuhusu habari ya mataa kwamba Mji Mkongwe utatiwa mataa, mimi nasema sio Mji Mkongwe tu taa za njiani ni muhimu hata ukienda *Air Port* ukenda wapi, taa za njiani ni muhimu Mhe. Naibu Spika, hili mimi kabla sijaingia katika Baraza hili nilikuwa nalisikia linapigiwa kelele lakini itatengenezwa taa moja itapwesa siku ya pili imekwisha, naomba nifanyiwe utafiti maalum kujua ni chanzo gani ambacho taa zetu hizi za njiani hazifanyi kazi zake.

Nakuomba Mhe. Waziri kwa heshima na taadhima tufufue mambo yetu ambayo kwa kweli tulikuwa tumeyazoea huko nyuma.

Mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, bustani za barabarani hizi hazijulikani mwanzo wala mwisho, hapa utaona maua mekundu kule utaona kiduge kimekaa vipi sijui naomba tuige mifano ya wenzetu kama hatuwezi tupande mipopoo mule ambayo kulima kwake ni mara moa mipopoo ina fadia Mhe. Naibu spika, na

mbegu zipo, tupande mipopoo kuanzia *Air port* mpaka mule mote ambamo tunahisi kwamba hatuhitaji ulimaji wa kutwa na mtu kuchimba mashimo, mipopoo tu namuomba Mhe. Waziri.

Baada ya kusema hayo nitoe shukurani zangu za dhati kabisa kwa kumuunga mkono hotuba hii Mhe. Waziri mia na hamsini. Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambae ametujaalia kukutana hapa sasa hivi katika Baraza lako tukufu, tukiwa hatujambo .

Lakini pili nikushukuru wewe kwa kunipatina nafasi hii na mimi nipate kuchangia japokuwa mchango mdogo lakini niweze kuchangia hotuba hii. Lakini tatu nimshukuru sana Mhe. Waziri jinsi ya uwasilishaji wake alivyoweza kuiwasilisha hotuba hii ya bajeti na niungane na Mhe. Rashid alisema anampongeza na kumshukuru kwa ile stamina aliyokuwa nayo kwa kusimama kwa masaa mawili na robo akaweza kuiwasilisha vizuri kwetu namshukuru na namuombea na Mwenyezi Mungu amzidishie kuwa na afya njema azidi kulitumikia taifa hili.

Mhe. Naibu Spika, na mimi nianze mchango wangu kuanzia na mazingira, mazingira ni kitu muhimu sana ambacho kinaizunguruka jamii yetu, hivyo nimuombe, nataka kusema hili la mazingira kwa kuisemea serikali sisi wananchi ambao tunatendewa na serikali yetu. Kuna usemi unasema mjenzi na mjengewa, mjenzi ni serikali yetu ambayo tayari inatujengea wananchi wake mahitaji mbali mbali ambayo tunayahitaji hivyo ni lazima na sisi tunaofanyiwa basi tuweze kushukuru na kupongeza kwa lile ambalo tumefanikiwa kulipata.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa serikali inajitahidi kwa juhudi zake zote kuwaletea mahitaji muhimu wananchi wake lakini sisi

wananchi tunayabeza sana, hivyo nitoe wito kwa wananchi kuwaomba serikali hii inapotuletea mahitaji sisi basi tuwe na moyo wa kupongeza juhudi za serikali yetu na kuenzi yale matunda ambayo tunaletewe, nasema hilo kwa sababu mazingira pamoja na juhudi zote utakazozichukua Mhe. Waziri na wizara yake nzima na watendaji wake wote kama sisi wananchi ambao tunafanyiwa hatukuyapokea kwa moyo mmoja na kuyaenzi basi itakuwa kazi bure.

Mhe. Naibu Spika, usafi wa mji ambapo ndio kitovu chetu kikuu tunachoringia mjini hapa, hata huo utalii basi tunasema utapendeza zaidi au utakuwa mzuri zaidi kama ule mji wetu utaonekana katika hali nzuri, lakini Mhe. Naibu Spika, cha kushangaza mji wetu ni mchafu kupita kiasi na ndiopo ninaposema tujitahidi na sisi.

Wizara kwa kuwa tayari imeandaa mpango wake huu naamini na sisi tukiongeza nguvu zetu pale basi tutaweza kufanikiwa. Nimuombe Mhe. Waziri kama sheria ipo au haipo basi iletwe na tuweze kuipitisha lakini baadae nimuombe aisimamie kwa juhudi zake zote, kwa sababu sisi wenyewe tunachafua mazingira kwa makusudi tunatupa hata viboksi ovyo ovyo, maganda ya muhindi kila kitu sisi tunatupa tupa tu kwa kutegemea Manispaa itakuja kusafirisha sisi wenyewe hatujali basi box hata chini ya mlango wako kweli ije kuzoa Manispaa, lazima na sisi tuwe na utaratibu wa kuweza kuthamini.
Mhe. Waziri ametueleza hapa jinsi atakavyotusaidia kusafisha Mji huu lakini na mimi nasema tuongeze juhudi sisi wenyewe lile linalohitajika kulifanya na sisi basi tufanye kwa kuipa nguvu serikali yetu.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo niende katika vikosi kama wenzangu walivyovipongeza vikosi vyetu vya SMZ kwa kweli vikosi hivi vinajitahidi san asana, na pale inapohitajika kupongezwa basi kweli tuvipongeze na tuvipe motisha. Maana ya

kusema hayo nataka nianze na kikosi cha KMKM kikosi hiki kinafanya kazi zake vizuri lakini katika mazingira magumu sana, nayasema haya kwa ushahidi tosha kwa sababu mimi ninapoishi naishi karibu sana na kikosi cha KMKM Mkokotoni. Inawezekana kwa kuwa hiki ni kikosi shida zikawa ziko nyingi lakini mimi nitasema zile ambazo naziona mbele ya macho yangu.

Mhe. Naibu Spika, kikosi hiki pale kilipo kina boti chakavu lakini hata mashine haina, hapana mashine na hiki ni kikosi ambacho tunategemea wakati wowote kisaidie kuokoa mali ambazo zinasafirishwa kimagendo, lakini pia kiweze kuokoa wananchi wanapopatwa na ajali za baharini. Lakini cha kushangaza sana pale Mkokotoni shida zikitokea basi utaona KMKM wanavyohangaika wanamtafuta mwenye mashine wamuazime ili wende kuokoa tatizo lililotokea.

Hawana mashine, hawana hata mafuta ya akiba yaliyokaa pale kama angalau ikitokea shida wakaweza kui-*serve* mara moja, lakini jengine hata ile nyumba ambayo wanaishi pale hivi sasa basi sio ya kwao. Kwa hivyo nimuombe sana Mhe. Waziri kuweza kuangalia askari wetu hawa kwa jicho la imani waweze kupata makazi ambayo ni ya kwao, lakini pia waweze kupata vitendea kazi muhimu. Katika kitabu hiki kimeeleza kwamba zitafanyiwa ukarabati vyombo vya baharini, lakini pia nimuombe ukarabati ufanywe lakini pia kupatikana vyombo vipya ni muhimu zaidi.

Sasa niende na Kikosi cha Mafunzo kama walivyotangulia wenzangu waliosema kwamba hiki kikosi ni muhimu sana, kikosi hiki kinashughulika na wanafunzi na mahaburu ambao wanapelekwa pale lakini cha kushangaza bajeti inayowekewa inakuwa ni ndogo sana na hali ya kuwa wana mzigo mkubwa, nimuombe Mhe. Waziri kuviangalia vikosi hivi kwa jicho la imani sana hasa ikizingatia kikosi hiki kinajishgulisha na uzalishaji mali. Mimi nasema nyongeza iende kwenye fungu kwa kuwa na wao

wanajitahidi kuzalisha basi na sisi ni vizuri kuwapa motisha wa kuongezea ili wakaweza kupata moyo na kuweza kufanya vizuri.

Mhe. Naibu Spika, vikosi hivi vinajishughulisha na kilimo ambacho juzi tu Mhe. waziri wa Kilimo ametuleta mswada wake ambao tunahitaji kuwa na chakula cha kutosha, leo vikosi hivi tukivipa motisha vikaweza kufanya vizuri tunaweza kupata chakula cha hakiba, mimi nimuombe Mhe. Waziri vikosi aviangalie kwa jicho la imani kama kile cha Zimamoto mama Asha Bakari ameshakisemea sana kuwa ni mtoto yatima hasa hana baba wala mama.

Kwali Zimamoto haijawahi kuzima labda majivu kila inapofika katika tukio tayari moto umeshazimwa, basi nimuombe Mhe. Waziri zile sehemu ambazo muhimu tunaogopa yasitokee majanga na sehemu za kazi angalau basi pawa na mahodhi makubwa makubwa, angalau ikitokea tatizo la moto angalau wale watu waliokuwepo pale wawahi kuchukua ndoo na kuzima, kwa sababu hata ikija zimamoto unakuwa umeshazimika moto.

Mhe. Naibu Spika, kuna kikosi cha JKU ambacho kikosi hiki kinafanana sana na kikosi cha Mafunzo nacho ni kikosi cha uzalishaji, hapa hivi sasa tunakitegemea kutuzalishia mbegu kwa ajili ya wakulima, jamani nasema vikosi hivi tuvipe motisha vinajitahidi kadiri ya uwezo wao, lakini sisi bado tunaona kazi wanazozifanya hatujazipa kipaumbele. Mhe. Waziri wa fedha alipokuwa anawasilisha bajeti yake hapa ameonyesha vipaumbele ambavyo amezipa Wizara zake, kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri na yeye kuvipa kipaumbele zile Idara ambazo zitaonekana zina mahitaji muhimu sana kwa wananchi wetu ili tuweze kuokoa tatizo likitokea.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo nije kwenye habari ya ujenzi wa nyumba za viongozi au ukarabati, hivyo mimi kwa upande wangu nianza na ujenzi wa nyumba ya Rais pale Kibweni, Rais

wetu ni kiongozi mkuu ana majukumu makubwa na anaporudi hutaka pahala pa kupumzika penye utulivu, hivyo mimi nimuombe Mhe. Waziri waliangalie hili kwamba Rais anahitajika kupata pahala pa utulivu zaidi na sio pale barabarani ambapo pana mazogo ya kila wakati. Itafutwe sehemu nzuri ambayo itakuwa na utulivu kwa kiongozi baada ya majukumu yake na tunamuona Mhe. Ali Mohammed Sheni na harakati zake anajitahidi anafanya kazi usiku na mchana zege hailali, kikao hata saa ngapi lakini atahakikisha kimefikia muafaka kwa hivyo na sisi lazima tuige mifano ya viongozi wetu hawa.

Mhe. Naibu Spika, niendelee katika sehemu ya ujenzi kwa kuomba kuongezewa fedha katika ujenzi wa nyumba ya Mhe. Mkuu wa Mkoa Mkokotoni ambapo na mimi ni mdau katika nyumba hiyo, naomba sana wasaidiwe jengo lao ni chakavu linahatarisha usalama na kufanya kazi kwa utulivu, hivyo waongezwe pesa ili kuweza kukamilisha ujenzi wao ule ili wahamie na kufanya kazi zao kwavizuri,

Lakini pia imetajwa ukarabati wa nyumba ya Mkuu wa MKoa wa Kaskazini Mheshimi vile vile mimi niseme ndio mdau naishi mule, naomba Mhe. Waziri akija hapa anipe moyo wa kuona ni lini ukarabati huo utaanza nimehamia katika nyuma kama gofu lile, najitahidi tu kukaa lakini ni nyumba ambayo imechakaa vibaya sana haistahiki. Hili nalisema kwa upande wangu lanini vile vile nasema kwa niaba ya nyumba zote za serikali kuzienzi, kuzitunza na kuona kila inapohitajika kufanywa ukarabati tunafanya mapema, mwenzangu amesema hapa jamani tuzibe ufa ili tusije kujenga ukuta tunaweza kuokoa pesa nyingi za serikali kama tutafuatilia vitu vyetu haraka haraka.

Mhe. Naibu Spika, nyumba hii ni chakavu sana naomba Mhe. Waziri akija hapa mimi aniambie ni lini itaanza kufanyiwa ukarabati kwa sababu mimi niko pale na nyumba mbovu sana, haina hadhi na pale Nyumba ya Mkuu wa Mkoa ni Ikulu ndogo

wakati wowote anaweza kuja kiongozi wa juu pale wa kitaifa, namuweka wapi nyumba haina fanicha wala haina chochote ndani ya nyumba ile. Nakuomba sana Mhe. Waziri na mimi unipe matumaini.

Mhe. Naibu Spika, niendelee na mimi kuligusa Baraza la Manispaa ambalo nimuombe sana Mhe. Waziri tunapokuwa na mambo yetu, tunapojadili au tunapopanga mipango yetu basi tukipanga ikawa ya muda mfupi, iwe ni mipango endelevu ambayo inakuwa inaendelea kwa muda mrefu nalisema hili kwa ababu ya kuona wafanya biashara wanatanga tanga haijulikani wapo wapi, mara wako huku mara huku na wakati sisi tunapata kodi kutokana na wao wale. Mhe. Waziri naomba atuboreshe wafanya biashara wetu hawa ambao wanatuingizia kipato basin a sisi tuweze kuwathamini, waweze kuwekwa katika mazingira mazuri na tukiamua kuwaondosha badi wapate sehemu nyengine ambapo wataendesha biashara ile vizuri.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo na mimi nikushukuru sana na nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ambaye ndio Rais wetu na sisi nasema tuige na tufuate nyendo zake ili tuweze kwenda vizuri. Siku zote Baraza hili linapitisha sheria na mimi naomba sheria zisimamiwe na ziweze kutekelezwa, siku zote hapa tunapanga na ikichakaa kidogo tunairekebisha lakini utakuta hazitumiki. Kama sheria hatukuzisimamia vizuri kila kitu chetu kitadorora.
Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache kwa niaba yangu na kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, naunga mkono hoja hii mia juu ya mia. *(Makofi)*

Mhe. Moh'd Haji Khalid: Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru wewe kunipatia nafasi hii asubuhi ya leo baada ya wakalia viti wenyeviti wawili katika Wizara mbili zilizopita

kunikosesha nafasi na kunitia katika kapu kubwa. Kwa hivyo nakushukuru leo kwa kunipa nafasi hii.

Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha asubuhi hii kukutana hapa kujadili maendeleo na matatizo ya nchi yetu katika bajeti hii ya mwaka huu, katika Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, kwa hivyo kutokana na sauti yangu ya usemaji mimi sitaki nitoe shukurani nyingi kwa sababu muda wangu mwingi nitakuja kutumia kwa shukurani nije nikose kusema, kwa sababu ati yangu ya kusema ni ndogo ndogo kwa hivyo sitaki nitoe shukurani sana nianze moja kwa moja na yale niliyokusudia kuyazungumza.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitanza kwenye ukurasa wa 21 kifungu cha 39 mwisho huku kifungu hiki kina sentensi moja ndogo inasema, wananchi wameweza kuishi pamoja na kushirikiana katika kujenga nchi bila ya kujali itikadi zao za kisiasa ndani ya muundo mpya wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kukaa huko kwa pamoja bila ya kujali itikadi zao kisiasa ni matokeo maalum yaliyotokea katika mwaka uliopita wa 2010, tukio hilo ni kwa kuja kura ya maoni na hatimae baada ya uchaguzi ikaanzishwa serikali ya Umoja wa Kitaifa na Serikali ya Mapinduzi chini ya Umoja wa Kitaifa.

Hili ndilo lililotuweka katika hali hiyo ningeomba hali hii tuiendeleze na tusiipuuze kwani ndio ngao yetu ya kuijenga nchi yetu kwa sababu tumeshakaa pamoja bila ya kujali hizo itikadi zetu za kisiasa.
Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi baada ya kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar aliinama na akafikiri sana na akateua Makamo wake wawili wenye jina moja kwa lugha mbili tofauti kuna lugha moja majina haya ya Sefu ni upanga, kuna lugha nyengine ni amani au utulivu. Kwa hivyo naomba Makamo hawa wawili wawe upanga pale atakapotokea mtu kujaribu kuchafua umoja wetu huu. Na kwa lugha nyengine

kwa amani pale ambapo amani hii itaendelea na wao waendelee kuilea ili isije kuchafuka. Watu hawa ni wenye busara, hekma na mawazo mapana ambayo naamini wataweza kujituma kuendeleza hali hii isitenguke kwa sababu ndio msingi wa umoja wetu.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo nije katika ukurasa wa 24 kifungu cha 46 kwenye sentensi moja ndogo iliyoanzia aidha.

Kifungu cha 46 "Aidha wananchi wametakiwa kuacha uharibifu wa mazingira kufuatia uchimbaji wa matofali unaofanyika Kangagani, Mwambe na Micheweni Kisiwani Pemba."

Hapa imekuja katika kuacha uharibifu wa mazingira. Mimi nipo karibu sana na Mwambe,

Jimbo langu limepakana sana na jimbo la Kiwani ambalo ni Mwambe. Uharibifu huu uliokuwepo eneo la Mwambe kama haukudhibitiwa iko siku Mwambe itazama na ikizama na mimi nitakuwa nipo ukingoni mwa kuzama, kwa sababu tumepakana. Kwa hivyo ikizama Mwambe na jimbo la Mtambile sehemu ya Kengeja sehemu ninayoishi mimi nayo itakwenda. Hapa kwa sababu pametajwa mazingira ni lazima pamoja na kuwa Idara ya Mazingira haimo katika ofisi hii lakini utendaji wetu wa kazi ni lazima tushirikiane ili gurudumu liweze kuzunguka. Hapa iko haja kubwa ya kutunza mazingira ya sehemu zile ili kisiwa kile kisije kuzama.

Uchimbaji wa matofali mchanga na fusi, ni jambo la lazima kwa sababu kifusi tunajengea barabara zetu, matofali tunajengea nyumba zetu. Wachimbaji waelimishwe kitaalamu na watu wa mazingira jinsi ya kina cha kuchimba hayo matofali na hicho kifusi. Mpaka sasa hatujakuwa na nyenzo mbadala ya kutumia katika ujenzi, ama tutumie miti ambayo tayari imeshapitwa na wakati, ama tutumie matofali yale ya saruji. Pia tunahitaji kupata

mchanga, bado utumizi wa mchanga utakuwa upo. Lazima wataalamu wa mazingira wafanye kazi ya ziada ili kunusuru uharibifu wa mazingira ambao kila kiongozi anapozungumza anaugusia.

Mhe. Naibu Spika, niende katika ukurasa wa 27 kifungu cha 52 kuna pahala imetajwa tu kutekeleza ahadi za Rais. Hapa naomba waratibu wanaohusika na kuratibu shughuli za viongozi wetu wa Kitaifa hususan Rais. Pale anapotoa ahadi tuhakikishe kuwa ahadi zile zinatekelezwa. Hivi sasa kuna viporo vingi vya ahadi zilizotolewa na viongozi na hatimaye zikaachwa bila ya kuchughulikiwa.

Hali hii ikiendelea wananchi wetu watakuja kuwaona viongozi wao wanawadanganya. Kumbe kiongozi akishasema yeye kwake kazi imemalizika, mtekelezaji ni mtendaji. Zamani watu walikuwa wakisema neno la Rais ni sheria. Leo marais wetu wanaweka ahadi lakini watendaji wanazibeza na hatimaye kuna misururu ya viporo vya ahadi zilizotolewa na viongozi kadha waliostaafu bila ya kutekelezwa. Ningemuomba Waziri ahakikishe katika awamu hii ya saba ahadi zote ambazo viongozi wetu wa Kitaifa wataziweka zitekelezwe kama vile walivyoahidi.

Mhe. Naibu Spika, niende katika ukurasa wa 30 nambari 58 inayohusiana na vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi. Mimi binafsi hili jina silipendi kwa mimi kuanzia babu yangu, baba, mimi mwenyewe, napewa kitambulisho naambiwa ni mkaazi. Huyu mwenye Zanzibar ni nani? Ikiwa sote sisi ni wakaazi hao wenyewe ni nani? Wakati wa awamu ya kwanza Mzee Abeid Amani Karume kulikuwa kuna kadi ya uraia ya Zanzibar na wale ambao si raia wao ndio walikuwa wanapewa kadi za ukaazi. Lakini leo mimi raia napewa kadi ya ukaazi aliyekuja kuhamia anapewa ya ukaazi. Nahisi jina hili ningeomba mimi kwa upande wangu lirekebishwe. Linamfanya Mzanzibari awe hana kwao yeye ni mkaazi tu. Kuonesha kuwa si pao hiyo kadi anayopewa

anapewa kwa muda maalum, ambapo uraia mtu unakuwa wa kudumu vyenginevyo abadilishe. Sisi tunapewa uraia wetu kwa awamu, kuonesha kuwa si petu hapa, sijui pa nani. Mimi hapa ndio petu, kwa hivyo nitajiita Mzanzibar wala sitojiita Mzanzibari mkaazi.

Ukurasa wa 43 kifungu cha 84. Mhe. Naibu Spika, hapa kuna kisehemu kinachosema hasa Wakuu wa Mikoa. Mikoa mitatu mmoja wa Mjini/Magharibi na miwili ya Kaskazini na Kusini Pemba hayana bajeti za maendeleo. Ina maana mikoa hii imeambiwa ipige mguu shoto kulia, shoto kulia, shoto kulia, bila ya kutembea. Hii shoto kulia ina namna mbili. Kuna moja shoto kulia unakwenda mbele, nyengine unabakia pale pale ulipo. Hii inachosha. Je, Mikoa hii imeendelea vipi hata ikafika kuwa isipangiwe bajeti ya maendeleo na ikapangiwa mikoa miwili tu. Ina maana hii Mikoa mitatu imeshaendelea sana sasa waingojee hii ifike pahali walipo wao.

Mkoa wangu mimi wa Kusini Pemba bado upo nyuma wala hauhitaji kuingojea hii Mikoa miwili ya Kusini na Kaskazini Pemba. Kwa sababu nao haujafika hatua yoyote. Nimeshangaa kuona kuwa haina hata shilingi moja ya maendeleo. Mkuu wa Mkoa mwenyewe Afisi yake ni koridoo, Afisi ya Mkuu wa Wilaya ni mbovu na nadhani wanahamishwa, sina hakika. Halafu hizi Wilaya kwa nini hazina bajeti, taasisi zote. Hizi Wilaya zinabebwa tu. Kwa nini Afisi za Wakuu wa Wilaya zisiwe na bajeti zao za kujitegemea.

Tulipotembelea kwenye Kamati Afisi mbovu kuliko zote nilizoziona ni Afisi mbili, moja ya Mkuu wa Wilaya wa Chake-Chake, ambayo sisi tuliogopa kuingia tuliikagua nje tu, tukamwambia sawa sawa. Nyengine ya Mkuu wa Wilaya Mjini hapa. Ni Afisi mbovu sana tena mbaya, hata haikuelekea kuwa ni Afisi. Kama tungeliambiwa kuwa hili ni jengo watu wa madawa ya kulevya wamejihifadhi tungeliamini. Tumekwenda kuna Mhe.

Mkuu wa Wilaya na watendaji wake, baadhi ya Afisi wanakaa Idara mbili tofauti kijiofsi kimoja, hii ni hali mbaya sana.

Halafu Mkoa huu kwenye Afisi ya Wilaya iliyo hivyo zaidi yale matumizi ya kawaida hawana hata shilingi moja ya maendeleo. Mhe. Waziri tungeomba utupe ufafanuzi kwa nini Mikoa mitatu hii isipewe chochote. Hii ya Pemba imetoa ruzuku ambayo inakwenda katika Mabaraza ya miji husika. Nichukue Mkoa wa Kusini Pemba, ruzuku iliyotiwa inakwenda katika Baraza la Mji la Chakechake na Mkoani. Imetiwa katika ujumla wake, ruzuku hii haina ugavi. Sijui Baraza la Mji la Mkoa katika ruzuku ile itapata kiasi gani, wala Baraza la Mji la Chake-Chake litapata kiasi gani. Nilitaka Waziri anieleze nijue Baraza la Mji la Mkoani katika ruzuku ile kama itapatikana kifungu chao ni kipi. Isiwe ujumla jumla vile kama ilivyotolewa, kwa sababu hawa kila mtu ana kwake.

Mhe. Naibu Spika, sasa nije katika Kikosi cha Zimamoto. Kikosi hichi kina kazi kubwa na muhimu, bajeti yake ni finyu mno. Kama walivyotangulia wengine waliosema zaidi ya zile kazi za kawaida hakuna hata senti ya kazi za maendeleo. Tulipokuwa tukitembelea vikosi hivi walivyotueleza namna walivyofanya kazi lile gari la umoja mafuta wanayotumia kwa siku pengine Mhe. Waziri anatumia kwa mwezi mzima, miye hata miezi miwili.

Kikosi ambacho kina kazi kama kile lakini bado tunakibana katika kukipa matumizi. Sijui Mhe. Waziri kuna mantiki gani ya kikosi hichi muhimu kupewa bajeti finyu aina ile. Halafu wanafanya kazi katika mazingira magumu na mazito. Tulipokwenda uwanja wa ndege wa Chake-Chake kwenye kukagua tuliwakuta wafanyakazi hawa pale uwanjani na ilikuwa ni siku za mvua. Wamesimama kama waliokuwa wapo katika nyumba ya makuti inayovuja, kwa ufupi walikuwa hawana ofisi. Yale maji ya mvua yanaingia katika kijichumba kidogo wamesimama, kama waliofiliwa na wazazi wao.

Kikosi kama kile kinachofanya kazi ngumu kuwaacha katika hali kama ile ni kuwasononesha. Mhe. Naibu Spika, nimuombe Mhe. Waziri ajipige pige ili wale askari wetu au kile kikosi chetu kilichokuwepo kule Uwanja wa Ndege wapate pahala pazuri pa kukaa ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, katika ziara zetu za kamati tumekitembelea Kikosi cha JKU zaidi tulikwenda katika sehemu zao za uzalishaji. Wana vitu vingi vya thamani, vitanda, meza, lakini hawana soko pa kuuza. Ningewaomba au ningeziomba taasisi za serikali kabla hawajanunua fanicha hizi kutoka nje kwanza waende wakatizame zile za vikosi vyetu tuone namna gani ubora wake zilivyo ili tuweze kuwasaidia. Tutumie msemo unaosema *"charity begin at home"* tusiende katika viwanja vya nje kumbe mali kama ile petu ipo na pengine ni bora zaidi kuliko ile tuliyoifatilia huko.

Mhe. Naibu Spika, hapa imetajwa kidogo zaidi kwenye Mikoa juu ya mizozo na migogoro ya ardhi. Visiwa vyetu vya Unguja na Pemba kila inchi moja ya ardhi basi ina mmiliki wake kama anajulikana au hajulikani, lakini ina mwenyewe. Kinyume na kule Bara. Bara ardhi haina mwenyewe na ndio maana unapokatiwa pande unatakiwa tu uchukue hati miliki kwa kipindi hicho ndio itakuwa imeshakuwa yako. Lakini ingia popote Unguja na Pemba hata uwe ni msituni, ukijidai kulima ukate kate, siku ya pili atazuka mwenyewe akuulize Mheshimiwa ilikuwaje, au mzee ilikuwaje.

Ningeiomba serikali pale ambapo inataka kujenga taasisi yake yoyote kwanza ihakikishe uhalali wa sehemu ile wanayotaka kuijenga. Kabla hatujajenga tuwe tuna hakika kuwa hii sehemu tayari tumeimiliki kisheria. Ili isijekuwa panda shuka mahakamani. Kuna watu wana nyaraka zao toka Sayyid Baraghash. Umiliki wa ardhi una matatizo na serikali imerudisha kwa Mikoa wenyewe kutatua matatizo ya ardhi. Ningewaomba

Wakuu wa Mikoa wajitahidi kutatua matatizo haya ili haki iweze kutendeka katika ardhi.

Mhe. Naibu Spika: Dakika 20 zimekwisha nakupa dakika mbili za kumalizia.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Naibu Spika, mimi kutokana na hali yangu ya usemaji nadhani ungeniona ni mtu wa pekee kunipa hata hizo zote thalathini. Lakini kwa kuwa dakika mbili hazitoshi ningeomba hizo 20 za awali nimalizie. Niseme naunga mkono hoja hii, ahsante.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Nikushukuru Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipatia nafasi ya kusema machache juu ya hotuba ya aliyoisoma sana swahiba wangu, ndugu yangu, Daktari Mwinyi Haji Makame.

Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima na kufika asubuhi hii kwa kuanza shughuli tulizotakiwa kuzifanya na wananchi wa nchi hii ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nilifarijika sana jana baada ya kusikia Mhe. Waziri anazungumzia kuanzishwa kwa eneo huru la biashara la utatu ikiwemo *COMESA* Jumuia ya Afrika Mashariki na *SADC*. Lakini bado furaha yangu ilifika mahala ikasita kwa wasi wasi ambao bado upo ni vipi Zanzibar pamoja na sifa yetu tuliorithi ya kuwa ni *center* ya biashara. Urithi ule leo unafutika kwa kasi kubwa na bado wenyewe sijui niseme hatujaliona hilo ama nguvu zetu timesinyaa au bado kuna usemi tuliouzoea ah! wenzetu wanaliona hilo. Wanaoliona naona wanatupeleka huko.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri alisema naomba ninukuu hapa

> "Naomba kuliarifu kwa ruhusa yako Baraza lako Tukufu kwamba Makubaliano hayo ni muhimu sana kwa manufaa ya Zanzibar, wataalamu wa Zanzibar watashiriki kikamilifu katika majadiliano hayo"

Mhe. Naibu Spika, kauli hizi tumezizowea lakini bado suali linarudi pale pale. Ni vipi Zanzibar kama Zanzibar, wataalamu wanakwenda wanashiriki lakini wana kikomo chao. Yanayobaki yanabaki kwa wanasiasa. Wanasiasa ndio wanaotoa maamuzi ya mwisho. Zanzibar kama nchi ya Zanzibar hizi itifaki za Jumuia za Kanda hivi haiwezekani Zanzibar kupata nafasi yake masuala kama haya. Mikataba hii inatuzuia, Mhe. Waziri hebu tusaidie na hili. Bado Wazanzibari wanajenga hofu pamoja na yote uliyoyasema. Kwa sababu wanachojiuliza kama hivi sasa mfanyabiashara huyu wa Zanzibar anapata vikwazo Tanzania Bara, vipi ndani ya Afrika Mashariki atafaidika.

Sasa tunakwenda zaidi kwenye utatu, *COMESA*, Afrika Mashariki na SADC atatuona nani, atatutetea nani. Haya ndio masuali ambayo wenzetu wanatuuliza kama Afrika ya Mashariki yaliyotajwa Zanzibar kufaidika ni Bandari na Uwanja wa Ndege hata kwenye vitabu haya hayakuzungumzwa mara hii kwamba yamefika wapi. Afrika Mashariki tumeambiwa tutapata Bandari Zanzibar hapa, watatujengea Jumuia ya Afrika Mashariki. Ukatajwa Uwanja wa Ndege wa Karume Pemba haya yote ambayo kwa Zanzibar ndio masuala ya kujivunia kwenye suala hili lililotajwa la biashara hivi sasa halimo. Mhe. Waziri ndugu yangu nitataka hapa uje utuwekee sawa kusudi Wazanzibari na wao wajenge matumaini mema.

Halikadhalika suala la viwanda mfaidiko wa biashara Mhe. Spika, Zanzibar kama Zanzibar lazima tukubali viwanda ndio safari yetu ya kufikia maendeleo. Ni viwanda vipi, hilo ni chaguo letu kufuatana na hali tutakayokuwa nayo wakati huo. Lakini kwa kutaja tu viwanda, viwanda bado na viwanda vyetu nilitangulia

kusema nilipokuwa nachangia hotuba ya Mhe. Waziri mwenye dhamana ya fedha.

Viwanda ni lazima viowane na kilimo, uvuvi na mifugo. Tutaweza kuagiza lakini hatutokuwa na uwezo mkubwa wa kuagiza mali ghafi na kusafirisha. Tutegemee zaidi mali ghafi tutakazoweza kuzalisha kwenye kilimo, uvuvi. Uvuvi kuna eneo kubwa la kujivunia na kuna mazao mengi ya baharini tunayoweza kufanya kazi. Ndani ya masoko haya ya kikanda ni lazima tujipange kwenye viwanda hivi.

Mhe. Naibu Spika, naomba nije kwenye mji wetu wa Zanzibar. Mji wetu tuna utalii, tunauita lakini mazingira yetu hayaridhishi na hali tuliyonayo hususan jimbo la ndugu yangu Mhe. Ismail Jussab, Mji Mkongwe unanuka, lakini mji wa Zanzibar unanuka, sifa ile ya kunukia imepotea. Pamoja na kwamba wananchi wetu wamepoteza sifa yao na utamaduni huu wa usafi. Haya ni mambo ya kusimamiwa na pale inapobidi, sheria angalau za muda kuona kwamba ni za dharura ziweze kujengwa kuweka hadi na haiba ya mji huu.

Mhe. Naibu Spika, nataka niseme kwamba Baraza la Mji la Zanzibar limepoteza dira yake. Wala sio kwa usafi tu. Humo mwengine tutalaumu watu watupa taka ovyo. Tupite kwenye barabara zetu kuu ambapo humo hiyo ni kazi ya Baraza la Mji. Mhe. Spika, kwa idhini yako ninukuu kipande kidogo. “Baraza la Manispaa limeundwa kwa Sheria Na. 3 ya 1995 kwa ajili ya kufanikisha majukumu na kusimamia kazi mbali mbali. Kati ya hayo ni kusimamia michirizi, maji taka, usafi wa barabarani, taa na kadhalika. Hivyo, tujiulize ni lipi kati ya hayo angalau limefikia asilimia 50.

Mhe. Naibu Spika, Baraza la Mji la Manispaa ya Zanzibar limezungumzwa masokoni kwamba kamati zako za kudumu za Baraza hili tukufu limepita tumeliona. Mhe. Naibu Spika, huko

kuna vituko kwani mengine mengi yameshasemwa lakini hali nzima ya ukusanyaji wa mapato na utoaji wa kodi hazifanani na hali halisi kuna ukiukwaji mbaya sana wa ukusanyaji wa fedha hizi, utoaji wa stakbadhi za asubuhi ni tofauti na jioni.

Mhe. Naibu Spika, ni dhahiri kwamba kuna vitabu vya mtu ama watu vinavyotumika kwa kukusanyia kodi. Hali hii Mhe. Waziri hatukuridhika nayo na haturidhiki kwa sababu Wazanzibari wote wanastahili heshima kama na huduma yao kwa usawa wao bila ya kubagua, bila ya kutizama jengine lolote lile, lakini usimamizi ama yanayotekelezwa huko ni kugumu mno kufuatana na hali nzima tunayoihitaji sasa hivi.

Mhe. Naibu Spika, ndani ya Manispaa ya Zanzibar sasa hivi kuna hali kutisha, hali ambayo Mtanzania yeyote akiisikia ama yule mpenda amani na maendeleo yetu atashituka kwani kuna ubaguzi mkubwa wa watu kwa maeneo yao wanayotoka. Mhe. Naibu Spika, hapa kuna sentensi inazungumzia maombi ya fedha kwa wafanyakazi hawa kupelekwa masomoni.

Mhe. Naibu Spika, Manispaa sasa hivi ina wasomi ambao wameshahitimu na wapo lakini hawakupangia kazi wanazostahiki na kwa sababu tu kuna mtu hataki, wamewekwa watu kwenye maeneo ambayo kwa maslahi ya mtu huyo hata kuandika barua anaiandika bosi, anapewa yule kuhalalisha hayo yako ndani ya Manispaa ya Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, hali ya namna hii Baraza hili nadhani si kazi yetu kuidhinisha fedha za umma zikatumiwa katika hali isiyokuwa sahihi.

Mhe. Naibu Spika, ili tu nisaidie Wajumbe wa Baraza lako kazi zetu sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi majukumu ya jumla ya Baraza la Wawakilishi kifungu cha 5(a) (2) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kimeweka mgawanyo wa madaraka kati ya mamlaka 3 za nchi na kimeweka majukumu ya jumla ya mamlaka hizo. Na kinatamka kwamba mamlaka ya utendaji ni

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma ni Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, hili ni miongoni mwa dondoo za karibuni alizotupa Katibu wetu tulisema hizi ndio dondoo kama tunasimamia utekelezaji wa shughuli za umma, hivyo fedha iliyoombwa na Baraza hili Mhe. Naibu Spika, hatupasi kuziidhinisha hadi pale tutakapopata maelezo ni kwa nini kuna wasomi wamehitimu wapo hawajapangia shughuli zao, na waliopangiwa hawana sifa na leo panaomba fedha nyengine wapelekwe. Mhe. Naibu Spika, hawa waliopo kwa nini wasiwekwe kwenye shughuli hizo.

Mhe. Naibu Spika, ni mengi yaliyopo kuna gazeti la Zanzibar Leo la tarehe 5 Juni, 2011 Kamati maalum ya Baraza la Manispaa sina muda wa kulisoma nikielelezo kwamba huko kuna vituko. Lakini Mhe. Naibu Spika, pale wajumbe wako wa Baraza lako tukufu kupitia kamati zako maalum tunapokuja tukaomba kuundwe Tume Teule mahali fulani, ni kwa sababu tumeshaona ama tumeshasikia harufu hapo mahali ni pachafu hapafai lazima pakachungunzwe.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia nataka pia niunganishe maneno yangu kwamba Baraza la Manispaa ni mtihani aliyeko huko na vituko hivyo mimi simjui lakini ni kazi ya serikali sasa hivi.

Mhe. Naibu Spika, kuna ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kuhusu malipo yasiyo na stakbadhi ya shilingi 500,000 kutoambatanisha stakbadhi katika hati za malipo ni kuend kinyume na kanuni 95(4) ya Kanuni za Fedha za Zanzibar kwa mwaka 2005. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, stakbadhi hizo hazikuonekana lakini kuna matengenezo ya Soko la Mwanakwerekwe milioni kumi na moja, laki saba sabiini na nne

na mia tisa na hizi nazo ukaguzi umebaini kwamba kuna malipo yamefanyika kwa ajili ya matengenezo ya soko.

Mhe. Naibu Spika, lakini sheria na kanuni za manunuzi hazikufuatwa tunasimamia sheria Baraza hili, tunatunga sheria lakini pale zisipofuatwa hatuna sababu ya kufumba macho. Mhe. Naibu Spika tunaiambia serikali fedha hizi ni za umma zinatumika lakini hatuwezi kuthibitisha zinatumika vipi na hatuwezi kuidhinisha nyengine zitumike.

Mhe. Naibu Spika, kuna malipo yasiyo na vielelezo *supporting document* hizi ni milioni nne na laki tano ni mtindo huo huo. Mhe. Naibu Spika, samahani hali ya namna hii, hii fedha kuchezewa kiasi hiki ni kwamba tuna mahitaji, tuna matumizi makubwa na mengi, skuli zetu ni matatizo, zahanati ni za tabu leo panapohitaji zitumike kwa maslahi na faida ya watu wote kuna wenzetu wanafanya watakavyo.

Mhe. Naibu Spika, nataka nimalizie kwa kusema kwamba ndani ya Manispaa ya Zanzibar naiomba serikali tena sana bahati nzuri Makamo wa Pili wa Rais yupo kunahitaji jicho la karibu sana kwani kazi nzuri iliyofanywa na Wazanzibari na ikapitishwa na Baraza lako tukufu ni kwamba walipitisha kwa kauli moja kuwa wanataka Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Kura zaidi ya asilimia 60 leo serikali hii imepata sifa kubwa, viongozi hawa Seif wawili chini ya uongozi wa Dk. Ali Moh'd Shein leo Wazanzibari wanatembea kifua mbele.

Mhe. Naibu Spika, ni kwamba mshikamano, maelewano, maridhiano yamefikiwa tunafanya kazi vyema kwa pamoja leo akatokea mtu ama kikundi kukebehi Mhe. Naibu Spika hali hii hatuwezi kuivumilia kwa sababu hasara yake ni kubwa mno. Mhe. Naibu Spika, hili liko Baraza la Mji tunamuomba ndugu yetu Mhe. Waziri hatuna nia yoyote mbaya kwako, lakini kwa sababu tunataka kukusafishia tunaomba ukaifanye kazi hii. Mhe. Naibu

Spika, huyu aliyeko ni mteuliwa wa Rais sisi sio wasemaji wa Mhe. Rais lakini ni wasemaji wa wananchi wa Zanzibar tunasema mwenzetu ana matatizo kwa hivyo vipi vya kufanya nyinyi mtajua serikali, tunataka wananchi wetu wafanye shughuli zao bila ya ubaguzi wenye haki zao wapewe, heshima zao zieleweke na wasomi wapewe nafasi zao kwani ripoti zote zimeshinda, hesabu zimepindukia mwaka.

Mhe. Naibu Spika, watendaji wa shughuli hizo wape lakini hawapewi dhamana zao kwa nini iwe hivyo sisi hatutonyamaza tunataka wawepo wale wafanye shughuli zao na wengine waende lakini kwa heshima zote. Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja hii asilimia 50 mpaka pale Mhe. Waziri atakaponipa maelezo na Baraza hili lenye dhamana kubwa ya kusimamia shughuli za serikali na kuwatumikia umma wa Zanzibar nipate maelezo juu ya fedha ambazo zimekwenda bila ya mfumo unaostahiki. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, naomba nianze kwa kushukuru kupata nafasi hii ya kuchangia bajeti hii muhimu kabisa ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na mimi niungane na wenzangu kwa kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuiwasilisha kwa staili ya aina yake bajeti hii. Na mimi naungana na wanaosema kwamba stamina yake ni kubwa sana. Mhe. Naibu Spika, kwa sababu stamina yake ni kubwa naamini stamina hiyo hiyo atakuja kuitumia kututosheleza hoja zetu wajumbe wakati wa kuja kufanya majumuisho ya wizara hii ili tusipate matatizo kama tulivyopitisha ofisi nyengine na hii iweze kupita vizuri.
Mhe. Naibu Spika, katika mlolongo huo wa pongezi naomba kwa namna ya pekee nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Mhe. Dk. Ali Moh'd Shein).

Mhe. Naibu Spika, Dk. Shein katika kipindi kifupi cha uongozi wake ameonesha kweli kwamba ni kiongozi ambaye Wazanzibari wanaweza kumtegemea kuitoa nchi yetu hapa ilipo na kuipeleka katika hatua kubwa zaidi na maendeleo. Ni mchapakazi habakii ofisini anakutana na wananchi wake na anatoa miongozo ambayo wananchi wanaifurahia sana, sisi tunaokaa na wananchi huko mitaani tunajua hisia zao walizonazo kwa Rais wao mpenzi.

Pia hapo hapo Mhe. Naibu Spika, kwa sababu tunazungumzia Ofisi ya Rais nataka pia nitumie fursa hii kumpongeza na kumshukuru kwa dhati kabisa Mhe. Rais wa awamu ya Sita Mhe. Dk. Amani Abeid Karume kama Zanzibar leo inashuhudia utulivu na tunajisifia hali hii tuliyonayo, basi kama kuna mtu anayestahiki pongezi za aina yake na shukurani za Wazanzibari wote ni Rais mstaafu Dk. Karume.

Hata sote Mhe. Naibu Spika, tungetaka maridhiano yawe angekuwa yule mwenye dhamana ya uongozi katika nchi hataki isingekuwa na hili tumeliona huko nyuma tumejaribu mara kadhaa halikufanikiwa, lakini Dk. Karume ameweka historia mpya ya Zanzibar tunafaa kumuenzi na kumkumbuka milele na milele kwa kazi hii nzuri ambayo ameifanya. Mhe. Naibu Spika, mimi naamini historia itamuandika vyema katika kusimamia suala hili la maridhiano na kuleta umoja wa kitaifa ambao umeisumbua Zanzibar kwa takriban miaka 50 ya misuko suko ya historia ya kisiasa katika visiwa vyetu.

Mhe. Naibu Spika, pia katika pongezi nimalizie kuipongeza sana sekreterieti ya Baraza la Mapinduzi. Mhe. Naibu Spika, tulikuwa tukifanya kazi kwa mazoea sana lakini katika kipindi kifupi hiki tumeshuhudia sekreterieti ya Baraza la Mapinduzi ikimsaidia Mhe. Rais kuandaa mafunzo ya aina yake na stamina zile ambazo zimetoa muelekeo mpya wa utendaji kazi katika serikali yetu. Bila shaka kama zimefanikiwa kuna watendaji waliofanya kazi kubwa

basi wanastahiki pongezi zetu chini ya Katibu Mkuu Kiongozi Dk. Abdulhamid Yahya Mzee naomba niwapongeze wote.

Mhe. Naibu Spika, baada ya pongezi hizo naomba nije katika yale ambayo yamo katika hotuba hiyo.

Mhe. Naibu Spika, kule kwa wenzetu upande wa pili wa bahari kumekuwa na hoja moja inaibuka mara kwa mara siku hizi ya gharama kubwa za matengenezo ya jengo la Ikulu. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, na mimi napata wasi wasi na Zanzibar tusije tukaingia katika mkumbo huo. Kwa hivyo, nilikuwa naomba kidogo kupewa maelezo kwamba pamoja na maelezo mazuri yaliyokuwemo katika kitabu yanaonesha matengenezo makubwa yaliyofanyika kwa hivyo kuweza kuhalalisha kabisa matumizi haya ya takriban bilioni moja mia moja tisini na mbili milioni kwa mwaka uliopita katika matengezo yaliyoko chini ya Ofisi ya Rais Ikulu.

Lakini naona na mwaka huu tena vile vile kuna matengenezo haya yanaendelea na kima kikubwa sana cha fedha takriban zimeomba chini ya fungu la jumla la Idara ya Mipango Sera na Utafiti ni milioni mia tano na hamsini. Kwa hivyo, hapa hatukufafanuliwa hatujui ngapi zinakwenda huku na ngapi zinakwenda kwengine.

Mhe. Naibu Spika, katika hili nikitizama kitabu hiki ukurasa wa 647 cha *estimate* naona kwamba kuna zile milioni mia tatu zilizotengwa kwa ajili ya ukarabati wa majengo na nyumba za viongozi. Lakini papo hapo nikiangalia katika ofisi ya faragha tena katika ukurasa wa 131 nakuta katika voti ya matengenezo ya ofisi na nyumba pana mia moja na sabiini na nne milioni mia tisa na sitini na saba. Kwa hivyo, nilikuwa naomba kusaidia, huku katika shughuli za maendeleo kuna mia tatu milioni, lakini hapa katika matumizi ya kawaida kuna hizi mia moja sabiini na nne milioni nilikuwa naomba kupatiwa maelezo Mhe. Waziri akija

atueleze isiji na sisi tusije tukaingia ule mkumbo ambao wenzetu umewaingia na umewafikisha pabaya sana.

Mhe. Naibu Spika, jambo la pili kuna fungu nimeliona hapa katika kitabu hiki cha makisio, lakini katika hotuba nzima ya Mhe. Waziri hakukiombea ridhaa ya Baraza la Wawakilishi. Hiki ni kifungu ambacho kiko katika ukurasa wa 134 wa kitabu hiki cha mswada inayozungumzia Idara ya Kazi Maalum na kwa mtazamo wangu wa haraka haraka sina hakika naona kama ni mpya ni vile kwa sababu ukitizama huku nyuma kote kuna ziro imenza kuombewa na inamalizikia pale ukurasa wa 136 imeombewa mia moja na arubaini na tano milioni. Mhe. Naibu Spika, huko mwanzo nilidhani labda hii ndio *GSO* lakini nikaona *GSO* ina fungu lake, sasa hili halikuombewa hapa idhini ya Baraza fungu hili la matumizi naomba Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie maelezo.

Mhe. Naibu Spika, niondoke hapo nije katika ukurasa wa 26 wa hotuba ya Mhe. Waziri alipozungumzia suala zima la huduma za mawasiliano Ikulu katika ofisi ya faragha. Mhe. Naibu Spika, serikali hii katika kipindi kifupi kabisa imefanya mambo mengi sana, lakini bahati mbaya wananchi wetu wengi hawayajui na matokeo yake unakuta kuna malalamiko mengi sana ya wananchi kwamba hawana wanachokiona, wakati kuna mambo mengi sana yamefanyika, lakini kama hatujakieleza hakiwezi kusikika.

Kwa hivyo, mimi nafurahi kwamba tumeambiwa kutakuwa na mikutano ya waandishi wa habari kila miezi mitatu. Lakini mimi nataka kupendekeza hapa kwamba kule kwa wenzetu kuna ule utaratibu ambao umeigwa nadhani kutoka Marekani wa kuwa na ile hotuba ya Mhe. Rais ya kila mwisho wa mwenzi.

Mhe. Naibu Spika, sioni ubaya kwa hapa kwetu na sidhani kama ina gharama kubwa kwa Mhe. Rais wetu kila mwisho wa mwezi kutoa hotuba kupitia vyombo vya habari, televisheni na redio yetu

akielezea yale ambayo yamefanyika katika mwezi ule na pia yale ambayo yanatarajiwa kufanyika kwa mwezi unaokuja. Nadhani hili litasaidia wananchi kujua mengi ambayo yanafanyika.

Mhe. Naibu Spika, hapo hapo naomba nisogee katika ukurasa wa 28 na 29 wa kitabu. Mhe. Naibu Spika, hapa naomba maelezo tu kuna hiki kitengo cha *GSO* lakini katika idara zilizokaguliwa hapa nimeona kuwa Baraza la Wawakilishi pia lilikaguliwa.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninavyofahamu Baraza la Wawakilishi sio sehemu ya serikali na hata nikiitizama Katiba kifungu cha 5A ya Zanzibar kinachozungumzia mgawanyo wa madaraka kinataja mamlaka hizi tatu mbali mbali. Kinasema kwamba mamlaka ya utendaji ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mamlaka ya Kutunga Sheria na Kusimamia Utekelezaji wa Shughuli za Umma ni Baraza la Wawakilishi na Mamlaka ya Kutekeleza Utoaji Haki ni Mahakama.

Mhe. Naibu Spika, kifungu kidogo cha 3 kinasema hakuna mamlaka itakayoingilia mamlaka nyengine isipokuwa kama na kwa kadiri ilivyoelezwa katika Katiba hii. Kwa hivyo, mimi napata wasi wasi kidogo ninapoona kwamba Baraza la Wawakilishi linakaguliwa na Kitengo cha Usalama cha Serikali hivyo namuomba Mhe. Waziri akija atusaidie je hatukiuki Katiba hapo katika muingiliano wa majukumu ya taasisi hizi za serikali.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo naomba kuja kupatiwa maelezo ni Idara hii inayohusika na Usajili wa Wazanzibari. Nikiangalia kumekuwa na *trend* ya bajeti ya ofisi hii kubwa sana. Kwa hivyo, huko nyuma ilikuwa kuna utaratibu wa kuianzisha na kutoa hivi vitambulisho, labda ingeeleweka lakini katika mwaka huu wa fedha tayari tunakuta idara hii imeombewa bilioni moja mia mbili arubaini na nne milioni. Wakati mwaka uliopita ambapo kulikuwa kuna pirika za uchaguzi na ilihusika sana hii na kutoa vitambulisho zilitumika shilingi mia tisa na kumi milioni. Kwa

hivyo, hii bajeti ambayo kila mwaka inavimba ya ofisi hii hebu naomba tusaidiwe kuna nini kinafanyika pale. Mhe. Naibu Spika, isije ikawa ofisi hii ni kichaka cha watu kutafuta fedha za walipa kodi, naomba Mhe. Naibu Spika, nipewe maelezo ya kutosha juu ya suala hilo.

Mhe. Naibu Spika, naomba nije katika suala ushirikiano wa kimataifa ukurasa wa 33 Diaspora hadi 43 wa hotuba ya Mhe. Waziri kumezungumzia jinsi Zanzibar inavyoshirikishwa katika maeneo hayo. Naomba nisisitize sitaki kutumia maneno marefu kwa sababu yameshazungumzwa ile hoja ambayo pia ameizungumza kaka yangu hapa Mhe. Asaa tuelezwe Zanzibar inanufaika vipi katika ushirikiano huu. Mhe. Naibu Spika, huko nyuma kwa mfano kunapotokezea mgongano wa kimaslahi Zanzibar inaathirika.

Nakumbuka palipokuwa na mvutano mkubwa wa Tanzania kuwa mwanachama wa *COMESA* au *SADC* palikuwa na mvutano mkubwa na Baraza hili lilichukua nafasi yake wakati ule.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu Zanzibar katika hali yake ya kutanua biashara ilikuwa inanufaika zaidi na *COMESA* kuliko *SADC*, lakini kwa sababu Serikali ya Muungano ilikazania kujitoa *COMESA* na kubakia *SADC* Zanzibar nayo ikaathirika.

Kwa hivyo, inapotokezea mambo kama haya sisi tunafidiwa vipi na Serikali ya Muungano kwa kuendekeza zaidi maslahi yao na kuyaacha maslahi ya Zanzibar ambayo uchumi wake wa kisiwa una mazingira tofauti kidogo. Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa naomba kupatiwa maelezo katika huu utatu unaoambiwa *tripartite* ya *SADC*, *COMESA* na Afrika ya Mashariki Zanzibar itafaidika vipi.
Mhe. Naibu Spika, lakini hapo hapo niseme bahati mbaya suala la ushirikiano wa kimataifa umewekwa chini ya Wizara ya Mambo ya Nje, ingawa ushirikiano wa Kimataifa wenyewe sio suala la

Muungano na hadi hii leo ukiangalia Katiba ya Muungano halimo suala hilo. Lakini kwa kuunda wizara inayoshughulikia mambo haya limewekwa pamoja.

Mhe. Naibu Spika, nasikitika kuwa ushirikiano wa kimataifa na hata kwa mambo ya nje Zanzibar hatuonekani kufaidika, hivyo tunamuomba Mhe. Waziri akija hapa hebu atusaidie huu utaratibu mpya uloanzishwa wa viongozi wa kimataifa unapotembelea Tanzania hawafiki Zanzibar una lengo gani kwa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, huko nyuma ilikuwa ni kawaida kabisa kila kiongozi anayekuja anatembelea nchi zote mbili zinazounda Jamhuri ya Muungano, lakini hivi sasa kuna viongozi wanne mashuhuri amekuja hapa Rais George Bush alomaliza muda wake Marekani, amekuja Rais Abdul Gull wa Uturuki, amekuja Rais Hujin Tao wa China na hivi karibuni amekuja Waziri Mkuu Dr. Manmohan wa India wote hao hawakufika Zanzibar. Lakini mwisho kabisa hapa tulimpata Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani Bibi Hilary Clinton nae hakufika Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, tunataka kuelezwa kuna utaratibu gani unaofanywa hapa wa kutaka kuifanya Zanzibar isitambulike kabisa kimataifa kwa wageni hawa kuishia upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano na kutofika Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, hili linagusa maslahi ya kiuchumi India imetengeka kwa mwaka huu dola bilioni tano kusaidia nchi za Kiafrika. Lakini kwa sababu viongozi hao hawafiki hapa hatupati fursa ya kujitosheleza ya kuwasilisha miradi yetu.

Mhe. Naibu Spika, leo mama Clinton alipokuja ikabidi Mhe. Mansour aende Bara kwenda kuelezea suala la kilimo kwa upande wa Zanzibar na kuna mpango ule ambao unafadhiliwa. Kwa hivyo, kwa nini viongozi hawa wasiletwe Zanzibar kama utaratibu ulivyokuwa ukitumika miaka yote tokea Muungano ulipoasisiwa mwaka 1964 hadi leo. Mhe. Naibu Spika, tukifika pahala

tukisema Wazanzibari wanachoshwa na Muungano ni kutokana na adha kama hizi ambazo hazitamalizika.

Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani utafika pahala Wazanzibari wataamua kwa sababu wanachoshwa na vitimbi hivi vinavyofanywa na upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mhe. Naibu Spika, tumtake Mhe. Waziri wetu amtake maelezo Mhe. Waziri Membe kwa sababu yeye ndie mhusika katika suala hili ana lengo gani dhidi ya Zanzibar kuendeleza utaratibu huu ambao hauwezi kukubalika kabisa.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa Baraza la Manispaa ni kwamba hili limezungumzwa na wengi na kama alivyosema Mhe. Asaa naomba Mhe. Naibu Spika, kidogo uniongeze dakika tano ili kusoma nukuu ndogo tu katika gazeti la Zanzibar Leo ili tuelewe tunachokizungumza hapa.

Mhe. Naibu Spika, Baraza hili lilisimama na wajumbe kwa kauli moja wakadai kuundwa kwa Kamati Teule ya kwenda kuchunguza uoza ulioko Baraza la Manispaa. Mhe. Naibu Spika, yakapita yalopita hatuna haja ya kuyarejea, lakini bahati nzuri Baraza la Madiwani likaonekana liko makini na mahiri zaidi kuliko Baraza hili.

Bahati mbaya sana wao wakaunda Kamati na ikachunguza na gazeti la Zanzibar Leo ni la serikali la tarehe 5 Juni, 2011 likatoa taarifa ya Manispaa Zanzibar kwa waka moto, kamati maalum yaibua madudu lukuki, yapendekeza serikali imng'oe Mkurugenzi, mikataba, matumizi mabovu yaanikwa. Mhe. Naibu Spika, sitaki kulisoma lote nataka kulisoma kidogo tu ambapo diwani huyu wa viti maalum CCM Salma Abdi nanukuu.

"Matatizo yanayolikumbwa Baraza hayakuchomoza kama uyoga, bali yametokana na kanuni na sheria kuburuzwa na utendaji mkuu wa Manispaa. Miongoni mwa kadhia ambazo zimeibuliwa katika

ripoti hiyo ni pamoja na kuwepo kwa mikataba hewa kwa baadhi ya makampuni huku pia ikiwemo mikataba ambayo imefungwa ikiwa hakuna taarifa za wazi. Mikataba hiyo ni pamoja na ule wa wafanyabiashara wa Saateni, Soko la Mwanakwerekwe, Soko la Darajani, Bustani ya Jamhuri, ujenzi wa barabara ambapo mbali ya kuwa haiko wazi lakini pia Baraza limekuwa likivuna fedha kidogo ambazo hazina maslahi. Aidha, kamati hiyo maalumu ilibainisha kuwa Baraza hilo limeingia mikataba kwa baadhi ya Kampuni za Simu kwa uwekaji mabango huku pia sehemu hizo zikiwa zimeshapewa kampuni nyengine.

Diwani Salma pia alisema Mkurugenzi huyu amekuwa akitumia amri za nguvu ambazo zimekuwa zikisababisha mivutano baina ya Manispaa na taasisi nyengine hali iliyosababisha taasisi hiyo kueleweka vibaya.

Akizungumzia juu ya usafi, Diwani huyo alisema kamati imebaini kuwa hakuna mikakati ya kuendeleza usafi huku Mkurugenzi aking'ang'ania ukusanyaji wa mapato zaidi. Aidha, ripoti hiyo imebainisha kutokuwepo kwa kumbukumbu za fedha pamoja na ofisi ya manunuzi hali inayofanya pawepo na kinyang'anyiro wakati Manispaa inapohitaji ununuzi. Sambamba na hayo pia ripoti imebainisha kutokuwepo kwa mkaguzi wa ndani wa fedha kwa kipindi kirefu, pamoja na baadhi ya maofisa kufanya kazi chini ya shindikizo la Mkurugenzi huyo na kutofuata taratibu za kiutendaji".

Mhe. Naibu Spika, nimeomba nilinukuu hili kwa sababu nadhani ni muhimu Wajumbe wa Baraza lako wakalifahamu hili. Mhe. Naibu Spika, tunaomba tupatiwe maelezo miminadhani majibu aliyotupa Mhe. Waziri katika hotuba yake kwamba tutegemee tu kwamba sijui Baraza la Manispaa lita-*deal* na Kampuni za Simu moja kwa moja hiyo haifuniki haya yaliyokuwa yamefanyika, haya mheshimiwa hayafunukiki. Kwa hivyo, nilikuwa naomba tupewe maelezo ya kina na kwa nini serikali kupitia waziri isili-

commend kwa Rais kwamba Mkurugenzi huyu astaafishwe kwa manufaa ya umma kwa sababu anaonekana anatutia hasara kubwa katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, nataka niliunganishe hilo na hili ninalotaka kulizungumza kwamba katika hili Baraza la Manispaa tunashuhudia kila mwaka inaombewa ruzuku hapa, lakini nikitizama kwa mfano mwaka ulopita imeombewa ruzuku ya bilioni moja mia mbili na nane milioni.

Lakini mapato yake yenyewe inayotegemewa ikusanye ilikuwa ni bilioni moja na milioni nne na mpaka kufikia Machi tayari ilikuwa ishakusanya mia nane na kumi na tano miliono. Mwaka huu vile vile imeombewa ruzuku bilioni moja na tisini na nne milioni, lakini inategemewa itakusanya bilioni moja na arubaini na moja milioni. Kwa hivyo, Baraza ambalo linakusanya mapato yanayolingana kabisa na mahitaji yake kwa nini liendelee kupewa ruzuku na serikali wakati pesa hizi zingekwenda kwengine zikaimarisha huduma katika nchi.

Mhe. Naibu Spika, hata tukizingatia huduma zenyewe zinazotolewa na Baraza la Manispaa hazionekani kuridhisha kwa sababu tungekuwa tunaipelekea fedha hizi na hizi zinazokusanya halafu tukaona huduma katika mji zinakuwa na Manispaa yetu inapendeza.

Lakini pamezungumzwa hapa kwamba uchafu umekithiri Mhe. Asaa watu wa Mji Mkongwe sio wachafu wanapenda mji wao unukie mawardi na asumini zinazopandwa nyengine zinatoka Kikwajuni, lakini bahati mbaya sana ni kwamba wanauliza hawa wanatozwa fedha kila duka katika Mji Mkongwe linatozwa shilingi elfu sita za uzoaji taka na haitizamwi kima cha duka lile kama kina thamani ya milioni 40 au kina mtaji wa milioni tano. Mhe. Naibu Spika, halafu inapokuwa taka hazikusanywi

mtawalaumu vipi wananchi kweli tunaweka usafi lakini inapotoka nje kazi ya kukusanya taki ni Baraza la Manispaa.

Mhe. Naibu Spika, pia kumetajwa maeneo hapa moja ni suala la ujenzi katika soko la Darajani kuna ujenzi unafanyika pale hauna maelezo yakutosheleza, wanaondolewa watu ambao ni masikini za Mungu wanapata rizki pale halafu pakishajengwa wanatafutwa watu wengine wakapewa maduka yale. Kwa hivyo, tunaomba tuje tupewe maelezo.

Mhe. Naibu Spika, vile vile pamezungumzwa hapa kuwa hata vyoo katika eneo zima la Manispaa huvipati vyoo vya umma, vyoo vyote vimeuzwa katika Baraza hili vimegeuzwa maofisi. Kwa hivyo, nasema tunakusanya mapesa yote haya lakini baadae hatuoni lolote.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba Mhe. Naibu Spika, tupewe maelezo ya kina katika hilo na ndio maana nasema hii dhana inayotaka kusema sasa ya usafi shirikishi. Mhe. Naibu Spika, kwa hali ilivyo sasa wananchi wamepoteza imani na Baraza la Manispaa hakuna dhana yoyote ya ushirikishi itakayofanikiwa, kwa sababu wananchi wanataka kuona kwanza serikali inawajibisha wale ambao wamekuwa wakiifikisha pabaya nchi yao na huduma wanazohitaji halafu tupate ushirikiano kwa serikali.

Mhe. Naibu Spika, nimepata matatizo naomba Mhe. Waziri akija anipe kidogo maelezo kuna huu Mradi wa *ZUSP* nimeusoma katika kitabu chake nadhani katika ukurasa wa 45 kama sikosei naona yale maelezo yamchanganuo wa mradi ule ukurasa wa 45-46 yameingiza mambo mapya, ambayo katika hotuba ya bajeti aliyotusomea Mhe. Waziri aliutaja mradi huu katika ukurasa wa 61-62 wa hotuba hii ya bajeti yalikuwa tofauti. Sasa nataka kuona kuna mambo mengine huku yako na huku hayako na kuna mengine yameongezwa huku na huku yameachwa. Hebu tupewe maelezo hasa ni maeneo gani kwa sababu nimeuliza hili naogopa

kwanini kuwe na historia mbaya Baraza la Manispaa kwamba isijekuwa watu wameshaingiza mambo yao mengine yale ambayo yaliidhinishwa yakaondolewa yakawekwa yao kwa maslahi yao.

Mhe. Naibu Spika, namalizia kusema naiunga mkono bajeti hii na nitaipitisha lakini baada ya kupatiwa maelezo ya kina na ya kutosheleza kutoka kwa Mhe. Waziri, nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi kuweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri. Kwanza kabisa nampongeza Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa ujumla, nampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa juhudi zake anazozichukua katika kutekeleza majukumu yake ya kazi.

Mhe. Naibu Spika, niipongeze Halmashauri za Wilaya ya Wete na Micheweni kuweza kuingiza mapato kwa kipindi hiki kidogo cha awamu ya saba kwa ufanisi na kupiga hatua ya maendeleo kwa Mkoa wa Kaskazini Pemba. Mhe. Naibu Spika, kwa kushirikiana na serikali na wananchi kuweza kupata viingizio vya mapato na kushirikiana na wananchi hilo linaleta faraja kwa Mkoa wa Kaskazini Pemba na Serikali kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, mimi nielekee kwenye mazingira, katika hotuba hii ya Mhe. Waziri amegusia uharibifu wa mazingira ikiwemo Kangagani, Mwambe pamoja na Micheweni.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kabisa usiofichika kama Kangagani wameshiriki katika uchafuzi wa mazingira kutokanana tatizo kubwa la ajira, kwani vijana wetu wengi wa Jimbo la Ole kwa sababu Kangagani iko kwenye Jimbo la Ole, Kiuyu Minungwini na Kangagani vijana hawa hawana ajira kutokanana kuwa wengine wamesomea uwalimu na uwalimu kipindi kikubwa

hawajaajiriwa. Kwa hivyo, wameona wao wajiajiri kwenye upigaji wa matofali.

Mhe. Naibu Spika, mimi namuomba Mhe. Waziri naomba awaangalie vijana wa Jimbo la Ole hawana ajira kwa hiyo hapo utakapowaondosha sijui wataelekea wapi. Mhe. Waziri kabla ya kuondoshwa pale vijana hao naomba kwanza uwawezeshe kwa miradi na halafu hili linawezekana kwa sababu katika ziara ya Mhe. Rais aliyoifanya katika Mkoa wa Kaskazini Pemba tulitembelea Wilaya ya Micheweni na Wilaya hii na wao wanashiriki katika huo upigaji wa matofali. Mhe. Naibu Spika, lakini wao Wilaya ya Micheweni walipata elimu nzuri baada ya kuchimba yale matofali huwa wanafukia halafu wanapanda miti.

Kwa hivyo, katika majumuisho yake Mhe. Rais alimtaka Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba awachukue wale vijana walioko Kangagani awapeleke Micheweni kwa ajili ya kwenda kusoma. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri kwa moyo wa huruma na upendo uwaangalie vijana wanaochimba matofali walioko Kangagani.

Mhe. Naibu Spika, sasa nije kwenye Baraza la Mji Wete wameahidi katika bajeti hii kuwekea kifusi standi ya magari iliyoko Wete. Lakini Mhe. Waziri mimi siioni standi ya Wete kwa sasa yote imezungukwa na nyumba, gari zile zinakaa mpaka barabarani. Hivyo, Mhe. Waziri hili uliangalie tena linatakiwa lifanyiwe kazi ya kutosha ili ipatikane standi ya uhakika na ya kudumu.

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha mwezi mmoja uliopita Kamati yetu ya Habari, Mifugo, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ilitembelea masoko yote ya Zanzibar. Katika kutembelea Soko la Darajani tulikwenda mpaka soko la kuku la Darajani haliridhishi hata kidogo. Mhe. Naibu Spika, soko lile ni chafu tena sana wale kuku wanaouzwa pale kwa mimi mtu wa hapa Zanzibar

siwanunui. Mhe. Naibu Spika, kuku wamewekwa kwenye mabeseni baadae wanawafunika magazeti, mimi namuomba Mhe. Waziri uwajengee wafanyabiashara wanaouza kuku katika soko la Darajani sehemu yao maalum ya kuuzia kuku.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja asilimia kwa mia. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujaakhirisha kikao chetu mpaka jioni pana matangazo mawili. Tangazo la kwanza kaleta Mhe. Waziri wa Kilimo anatupa taarifa kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi atafanya uzinduzi wa uvunaji wa mbegu mpya ya mpunga katika Bonde la Bambi tarehe 2 Julai, 2011 saa 3:00 asubuhi. Kwa hivyo, Mheshimiwa yeyote anayetaka kwenda atupe taarifa gari ipo atapelekwa na atarejeshwa Mjini.

Tangazo la pili ameleta Katibu wa Kamati ya Wawakilishi ya CCM anaomba wajumbe wote wa Kamati hiyo ya CCM wabakie hapa baada ya kuakhirisha kikao pana mambo muhimu. Ahsanteni kwa kunisikiliza.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 Baraza lilirudia)
(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Ndugu wajumbe orodha tuliyonayo ni kubwa na yote Waheshimiwa mna hamu ya kuchangia wizara hii kwa sababu ndiyo inayotugusa kwenye majimbo, wilaya, mikoa; lakini ningeliomba wale ninaowapa nafasi basi yale yaliyokuwa yameshazungumzwa ya msingi yaachwe na mtu aweze kuzungumza mengine. La kama anasisitiza basi asichukue muda mrefu kwa sababu kila mtu nitampa dakika 20.

Juzi Mhe. Spika, alitoa ufafanuzi juu ya kushangilia, bado watu wanapiga meza kwa nguvu sana. Sasa wenzetu wengine wana *pressure* mtu anaweza kuja kuanguka aikajakuwa matatizo. Kwa hivyo, tushangilie kwa kiasi.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii kuwa mtu wa mwanzo kuchangia mada iliyopo mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi ningeanza katika kipengele cha Diaspora. Nashukuru kwa mara ya mwanzo serikali yetu imeona kuna umuhimu wa wananchi Wazanzibari walioko nje ya nchi hii kuwapa fursa na wao kuchangia katika maendeleo ya nchi yao. Suala hili ni muhimu sana na ukienda katika nchi za wenzetu unawakuta wamejipanga vizuri sana katika suala hili.

Naishukuru serikali kwamba hivi karibuni nasikia imeandaa utaratibu wa kupeleka vijana wetu nchini Qattar ambao watakwenda kufanya kazi katika nchi hizo. Kwa hivyo, ningeomba hawa wakaanza kufahamishwa kuanzia hii leo nini hasa maana ya Diaspora ili wakaelewa na watakapotakiwa kutoa mchango wao katika suala hili wakawa wako tayari.

Mhe. Naibu Spika, suala hili ni muhimu lakini kabla ya kulifikia linan hatua tofauti ambazo zinahitajika zizingatiwe. Hivi sasa kuna wananchi wetu walioko katika nchi tofauti ulimwenguni na wengi pengine wana nia ya kuchangia katika uchumi wa nchi hii.

Lakini hivi sasa hapa katika nchi yetu ninachokihisi ni kwamba bado hatujakuwa tayari katika kuwakaribisha wananchi hawa kuja kuwekeza katika nchi yao. Kwa nini nasema hivyo? Kwa sababu miundombinu yetu bado haijakuwa tayari. Hivi sasa tuna tatizo la umeme ambalo linasuasua, tuna tatizo la maji ambayo hayana uhakika, hata utawala bora nahisi bado hatujafikia kiwango cha kuwa tumshawishi mwananchi aje kuwekeza katika nchi hii. Kwa

hivyo, ili tuwashawishi vizuri na ili tuwape fursa ya kuja hapa kwanza tunatakiwa masuala haya tuyape kipaumbele, si hivyo nafikiri wengi watakuwa hawako tayari kuja hapa kuingiza pesa zao katika uchumi wa nchi yetu.

Jengine katika hilo Mhe. Naibu Spika, ni kwamba wengi kati ya wananchi waliohama nchi hii wakenda nchi nyengine waliondoka kwa sababu tofauti, kuna walioyoondoka kutokana na siasa za nchi hii ziliwachosha, kuna waliyoondoka kuwa walitiwa mahkamani, kuna na waliyoondoka katika nchi hii kwa kupokonywa mali zao. Sasa ili wananchi hawa wawe na hamu ya kurudi katika nchi yao itabidi tuzingatie masuala ya kisiasa zaidi ili tuwashawishi wapate hamu, wapate imani na serikali yetu, kwamba tutakapokwenda kuwekeza katika nchi yetu tutapata usalama wa mali zetu.

Hivi sasa Mhe. Naibu Spika, wengi katika watendaji wetu hasa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya ni wale wale ambao walikuwepo katika awamu zilizopita. Kama tunavyojua awamu zilizopita tulikuwa tunaishi katika hali gani. Sasa ili tumshawishi huyu mtu aje hapa asema mimi niko tayari kuingiza pesa zangu katika mradi fulani basi itabidi tujenge mazingira bora ya kisiasa na ya kijamii, si hivyo wananchi hao nafikiri tutakuwa tunasema tu tuna Diaspora, tuna Diaspora.

Mimi nilibahatika kutembea nchi ya Bangladesh, ni katika nchi moja ambazo zimejenga utamaduni wa kuwapeleka raia wao nchi za Ghuba. Wao wameandaa jumuiya fulani ambazo zinakuja nchini Ghuba, Falme za Kiarabu na kuwatafutia wananchi wao ajira na baadae pato lile linarudi katika nchi hizo. Hivi sasa wale wanaokwenda kutembelea nchi za Ghuba hasa Mascat wanaona wafanyakazi wengi wa majumbani wanatoka eidha Bangladesh au Philipins. Kwa hivyo, na serikali nayo ingejipanga katika hilo, kuna wajane wengi huko mitaani ambao wangepata fursa kama hii wangeiunga mkono sana serikali yao na kuiona imewajali zaidi.

Mhe. Naibu Spika, sasa nakuja kidogo katika Baraza la Manispaa. Watu wengi sana wamepiga kelele hapa kwamba Baraza la Manispaa wee, Baraza la Manispaa. Baraza la Manispaa Mhe. Naibu Spika, lina mchango mkubwa sana katika aidha kuwakimbiza au kuwavutia watalii. Kuna watalii wa aina nyingi

Mhe. Naibu Spika, kuna wengine wakipita barabarani akiona kwamba anaziba pua siku ya pili hutompata tena, akienda barabarani akiwa anataka kujisaidia haja ndogo au kubwa hapati choo siku ya pili atakwambia mimi nchi ile siendi tena. Kwa hiyo, Baraza la Mji walikuwa wana wajibu mkubwa kwanza wa kuangalia mambo hayo muhimu. Leo ukienda katika Soko Kuu unakuta ndio pahala pa mwanzo pwenye uchafu. Sasa kama ni mtalii anataka kuingia pale kwenda kununua keroti au kabeji inakuwa kidogo anapata usumbufu na siku ya pili sijui kama atashawishika kuja tena.

Miaka miwili iliyopita Mhe. Naibu Spika, Baraza la Mji lilikuwa na mradi kama ilivyokuwa na lengo kwa awamu inayokuja ya kujenga au kukarabati michirizi. Niliona kampuni sijui ya wapi lakini wengi waliokuwa wakishughulikia kampuni ile walikuwa ni wenye sura za Kihindi, waliendelea kufukua mashimo, kusafisha mitaro, lakini mara tu walipoondoka watu wale barabara inayoelekea eneo la Mchangani na Mbuyuni kupitia Duka la Vioo zamani tulilokuwa tukiliita hivyo ikawa haipitiki.

Sasa mimi nikawa najiuliza je, hawa wamekuja kuchukua pesa zetu tu na kuondoka wavuja jasho hawana maana yoyote, lakini mvua iliponyesha tu barabara zote zikaziba. Kwa hivyo, naomba kuwapa tahadhari serikali kwamba wakati wanapotoa *contract* za kujenga michirizi kama hii basi wawe makini sana na makampuni ambayo hayana maana.

Hivi sasa Baraza la Mji lina mpango mzuri sana na limetwambia linataka kujenga bustani katika eneo ambalo kuna wananchi

wengi wanaopata ajira zao. Sehemu hii Mhe. Naibu Spika, imekuwa ni mvutano hivi sasa ni kama ule mchezo wa Mbwa na Tumbili, leo ondoka, leo bakia; leo sikutaki, leo hivi, kiasi kwamba katika mchezo huo kuna wengi ambao wameathirika. Miezi miwili au mitatu iliyopita kadhia hiyo iliwakuta vijana wale waliopo Darajani.

Sasa mimi ningemuomba Mhe. Waziri akanifahamisha kidogo je, bado serikali ina mpango wa kuliendeleza eneo lile? Je, wale wananchi ambao wamekaa miezi mitatu bila ya kuendeleza zile biashara zao watapata fidia yoyote au basi serikali haina tena mpango ule wa kuendeleza ile bustani pamoja na maegesho ya magari?

Mhe. Naibu Spika, sitaki nichukue muda wako mwingi, narukia kidogo katika sehemu ya vikosi vya huduma vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mara nyingi Mhe. Naibu Spika, inapofika wakati wa sherehe au maadhimisho ya kitaifa tunawaweka askari wetu katika milango mikuu ya kuingilia nchi hii, *air port* pamoja na bandarini. Sasa wale ambao wanakuwepo katika maeneo yale ya kulinda huo usalama wa nchi yetu wanajisahau, wanadhalilisha wananchi kiasi cha kuondoa utu wao.

Unapopita bandarini Mhe. Naibu Spika, kama unasafiri una kibegi chako huna kitu chengine chochote unaweza kujikuta unaambiwa vua nguo, garagara, hujui sababu yoyote ile uliyoifanya. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri hili aliangalie kwa macho mawili. Nimeshuhudia bandari ya Mkoani kijana mmoja ambaye naye alikuwa ni askari ikimkuta kadhia kama hiyo na wengine na wengine.

Katika hili pia nataka niseme kwamba, unapofika msimu wa karafuu kama tuanvyojua wengi huwa wanatafuta njia za kupitisha mali zao kwenda kuuza kwa bei iliyojuu na ndio imani yao na hapa panatokea mchezo ambao unahatarisha maisha ya

watu. Mara nyingi askari wa KMKM wanajisahau na kuna matokeo ambayo yamesababisha watu kuuwawa. Sasa ningemtaka Mhe. Waziri akanieleza je, kuna shieria inayomruhusu askari kumkutia mtuhumiwa akampiga risasi? Na je, wale ambao wamefanya matukio kama hayo wamechukuliwa hatua yoyote?

Naondoka hapo kidogo niende kwenye vitambulisho. Mhe. Naibu Spika, hili ni zoezi la kufanya kwamba kila mmooja awe na *ID*, huko kwa wenzetu ukienda ni vitu vinavyotumika mara kwa mara. Hapa petu mpaka hivi sasa kuna watu ambao wanasumbuka kwa asilimia mia moja kuipata hii *ID*, utakuta mzee ambaye kazaliwa ana miaka 60 anaambiwa wewe bwana huna cheti cha kuzaliwa, wewe huwezi kupata hiki; unamkutia kijana anaambiwa wewe sijui hivi.

Kwa hivyo, imekuwa ni kero kubwa kama vile zilivyo kero za Muungano. Sasa ningemuomba Mhe. Waziri hili akalitafakari kwa kina, kwa sababu wananchi wengi hivi sasa wamekosa imani na nchi yao na ndio unakuta wanaipa serikali hii majina tofauti kwa sababu yeye anajiona haamini kuwa kwa muda wa miaka 60 hajaondoka hata kwenda Tanzania Bara lakini leo atakapokwenda kuchukua kitambulisho anawekewa vigezo kama vile anayekwenda kuomba *VISA* ya Umarekani, mara lete hiki, mara hiki.

Sambamba na hilo Mhe. Naibu Spika, hivi sasa tumekuwa tuna vitambulisho vingi sana, kuna vitambulisho vinavyotokana na kadi za upigaji kura, kuna vitambulisho wengine tunavyo vya *passport*, wengine tuna vitambulivyo vya leseni kuna na hivyo vinavyoitwa vya ukaazi, lakini sijui vinavyotumika. Kuna mwanafunzi anataka kuingia Chuo Kikuu anaambiwa baba yako mwambie alete kadi ya kupigia kura, sasa je, rasmi kabisa ili mwananchi atambulike kwamba hiki ndicho kitambulisho chake ni kipi kitambulisho cha taifa hapa Zanzibar? Ambapo mimi kama

nimedaiwa kitambulisho cha upigaji kura naweza nikauliza kwa nini niulizwe hiki? Naomba tupate tamko rasmi hapa kwamba kitambulisho rasmi ni hiki hapa. Mimi kwa hayo machache na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu linalozalisha karafuu kwa wingi la Mkoani naunga mkono hoja.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando): Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wa wizara yake kwa hotuba nzuri kabisa ambayo mimi sina tatizo nayo sana, naiunga mkono kwanza kwa asilimia mia moja hii.

Lakini nina mambo mawili matatu kidogo nataka niyapitie ambayo nimeona ni mchango wangu huu nahisi ni ushauri zaidi, kwa sababu wenzangu wameshaogelea sana kwenye hizi mada na umeshatupa tahadhari Mhe. Naibu Spika, tusirejee rejee, basi nipitie tu kwa haraka haraka ili niweze kutoa maoni yangu mawili matatu kwenye hotuba hii.

Mimi nianze na huu mradi wa marekebisho ya Serikali za Mitaa. Ningemuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze hasa mradi huu utakamilika lini. Kwa sababu kwa kweli imekuwa ni hadithi ndefu sana hii, kila siku ukienda marekebisho ya Serikali za Mitaa, marekebisho wenyewe wan ajina lao wanaliita la kitaalamu mimi huwa silijui lakini najua kwa kiswahili tu marekebisho, wenzangu wananambia kuwa ni *reform.* Kwa hivyo, ningeomba Mhe. Waziri akija atueleze hasa hii *reform* ya Serikali za Mitaa lini itakuwa tayari ambapo sheria hii iweze kutumika ili haya matatizo tunayoyaona yamo kwenye serikali hizi yaweze kutatuliwa.

Nikiondoka hapo niende kwenye Idara ya Mawasiliano, Ikulu. Hiki ni kitengo muhimu sana kwa shughuli za pale

palipokusudiwa. Ni kitengo ambacho kinamuunganisha baina ya rais na wananchi wake kwa kupata mawasiliano, lakini mimi nimeona tatizo moja kidogo ambapo Mhe. Rais hivi karibuni alipofanya ziara nililiona katika ziara ya Mkoa wa Kaskazini pale, anafika Mhe. Rais anataka kuhutubia lakini hata mabomba hamna pale, ile gari ya kuweza kuhutubia na kuweza kusikilikana sauti yake hakuna.

Mimi ningemshauri Mhe. Waziri afanye bidii zake zote katika makadirio yake haya tuone angalau basi kuna gari moja pale ambalo linaweza kumsaidia Mhe. Rais anapofika mahala popote pale kuweza kuhutubia kwa wakati, isiwe rais kafika anasubiri gari la mabomba ndio linakuja baada ya rais kufika. Kwa kweli mimi naona ni kitendo cha aibu hiki na kimeshafanyika katika Mkoa wetu katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, tumefika pale rais anataka kuhutubia anasubiri mabomba.

Vile vile tulikwenda kwenye ufunguzi wa Skuli ya Potoa pale kamaliza kufungua rais anataka kuzungumza na wananchi mabomba hayapo linasubiriwa gari zaidi ya dakika 10 mpaka 15. Mimi nafikiri hii Mhe. Waziri si sahihi. Kwa hivyo, ningeshauri kitengo hiki kikawa kina mabomba au gari lake kabisa la mawasiliano ambalo litakuwa na uhakika wa kwamba kila anapokwenda Mhe. Rais gari hili litakuwa limetangulia na linatoa huduma hizo.

Nikiondoka hapo nije kwenye Halmashauri za Wilaya. Kwanza niwapongeze watendaji wa Halmashauri ya Wilaya yangu ya Kaskazini ‘A’ kwa kazi nzuri ya kuvuka malengo. Wamevuka malengo kabisa yale ambayo wamepangiwa na hii inaonesha ni bidii gani wanazozichukua wafanyakazi wa Halmashauri katika kutekeleza majukumu yao.

Hivyo basi, ningemshauri Mhe. Waziri azisaidie hizi Halmashauri kuziwezesha ili ziweze kufanya kazi yake vizuri zaidi. Nina

hakika ikiwa hivi sasa wameweza kufika pahala mpaka wanavuka malengo kama watawezeshwa vizuri basi nahakika makusanyo yatakuwa maradufu zaidi ya haya ambayo wameyafikia. Kwa sababu ukiwawezesha wataweza kutanua wigo wa kuweza kupata makusanyo zaidi.

Lakini vile vile nizungumzie suala la vitambulisho. Kumekuwa na malalamiko kidogo hasa katika Wilaya ya Kati nafikiri sote tumesikiai haya, malalamiko ya wananchi wa Wilaya ya Kati juu ya kuondoshwa ofisi yao ya vitambulisho pale ilipokuwepo kwenye ofisi ya Mkuu wa Wilaya nafikiria imehamishiwa Tunguu. Malalamiko yamekuwa mengi masheha wamekuwa wanalalamika sana wa wilaya ile, lakini masheha wale wanalalamika kwa niaba ya wananchi kwa sababu wao wanapata malalamiko kwa wananchi. Mimi nafikiri serikali iangalie tena kukihamisha kituo kile pale na ikirejeshe katika kituo kile kile cha mwanzo.

Kwa sababu ukiangalia ile jografia ya Wilaya ya Kati hapo kilipowekwa kweli ni Wilaya ya Kati, lakini ile jografia inakataa mtu kufikiria atoke Tunduni aende Tunguu kutafuta kitambulisho wakati alikuwa akitoka Tunduni anapita pale Wilayani anateremka gari anakwenda kwenye vitambulisho.

Lakini sasa hivi inambidi apande gari mbili, kwa mazingira ya watu wa kwetu inakuwa ni ngumu kidogo na serikali inahimiza muda wa kubadilisha ukifika watu wakachukue vitambulisho, lakini kama hatukuwajengea mazingira mazuri ya kuhakikisha kwamba wanakwenda kuvichukua kule hawatokwenda na itakuwa ni tatizo hili, siku ya siku inafika mtu unamdai kitambulisho kule kimeshatoka lakini hafiki. Mimi ningeshauri suala hili lingeangaliwa vizuri ili ofisi ile irudi pahala pake ilipokuwepo zamani na wananchi waweze kwenda kuchukua vitambulisho vyao pasina tatizo lolote.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea mbele nigusie Baraza la Manispaa kidogo juu ya kituo cha Saateni. Mimi nazungumzia kituo cha Saateni yale mazingira ya kile kituo pale kilipo. Kwa kweli hali ya mazingira pale hairidhishi hasa ikiwa imenyesha mvua pale ukipita pale pananyekenya tope, pametiwa fusi lakini inaonekana halikushindiliwa wala halijawekwa sawa. Kwa hivyo, mazingira ya pale ni mabaya sana, ningemuomba sana Mhe. Waziri ajitahidi katika hili atuombee huko kwa watu wa Manispaa pafanyiwe marekebisho angalau kama kile kituo cha daladala cha Darajani, pawekwe lami pale ili yale mazingira yaweze kubadilika.

Lakini vile vile tuangalie na wale watu wa daladala pale, wanasimama kwenye njia badala ya kuingia kule ndani, wanasababisha msongamano usi wa lazima, daladala inatoka Bububu inasimama barabarani, inayotoka mjini inasimama barabarani na sisi wengine tunaotaka kupita pale hatuwezi kupita kwa sababu ile njia yenyewe sio pana.

Sasa mimi ningelishauri Baraza la Manispaa likaandaa utaratibu mzuri wa kuweza kuwa zile daladala zisisimame kwenye njia, inayotoka mjini iingie kule ndani kwenye kituo kabisa, na inayotoka bububu huku iingie kituoni kipo kimetengenezwa pale kidogo, basi watengeneze mazingira kuwa zisikae barabarani ziwe zinaingia kwa ndani ili kutoa nafasi kwa zile gari ambazo hazisimami zinapita tu ziweze kuendelea. Kama sio hivyo, kesho na keshokutwa kila siku pale tutakuwa tunapokea ajali kutoka kwenye eneo lile.

Mhe. Naibu Spika, niguse kidogo kwenye suala la Mahkama katika Manispaa. Manispaa wanayo Mhakama yao pale, lakini imekuwa na manung'uniko makubwa kutoka kwa wananchi kwamba ukisogea kwenye Mahkama ile basi tena wewe huna hata cha kujitetea, ukifika wewe ni kifungo au faini hujitetei. Kwa hivyo, wanachosema pale ukifika anayekuhukumu sijui chui hivyo ukienda kondoo wewe hupati hata ya kujitetea. Kwa hivyo,

ukienda pale katika mahakama ile unaonekana wewe unakwenda ndani tu, utakwenda ndani au utalipa faini hata kama kuna jambo ambalo linatakiwa maelezo basi kutoa maelezo kwako kwanza kitisho unapigwa wiki mbili ndani, siku unayokuja unaambiwa ukubali yaishe au unarudi tena kwa hivyo mtu anakubali haraka haraka ili yaishe.

Sasa mimi nafikiri Mhe. Waziri aangalie vizuri hii Mahkama hasa kwa hawa watendaji, sifikirii kama sheria ndio yenye tatizo, lakini nafikiri wale watendaji. Kwa sababu inaonekana kama wengine wanawabambikizia kesi watu, kavuta huku kakataliwa basi wewe utakwenda tu na mkikubaliana huku yanakwisha. Sasa mimi nafikiri Mhe. Waziri hili kidogo tuliangalie kwa sababu wananchi wetu wamekuwa na malalamiko sana juu ya jambo hili.

Bado niko kwenye Baraza la Manispaa sasa nizungumzie kidogo juu ya hawa watendaji hasa hawa wa chini wafagiaji, mama zetu huwaona sana watu wazima wale ndio wanaofagia barabara, mara wanakata majani, unamkuta mama kakata kidog kakaa kitako kachoka anasubiri apumzike kidogo ili aweze kuendelea na kazi. Hawa mimi nahisi Baraza la Manispaa haliwaangalii kwa sababu siwaoni kukaa na vitendea kazi, utamkuta mtu anazoa taka hana hata *gloves* mkononi, wanazishika hivi hivi wanatia kwenye magari.

Sasa hili Mhe. Waziri uliangalie vizuri, vitendea kazi kwa ajili ya wale kinamama au wale wafanyakazi wa ngazi zile za chini. Wanaonekana wanafanya kazi kama kwa kulazimishwa, hakuna vitendea kazi, sifikirii kama hata afya mnawapima, maana mngekuwa mnawapima afya vizuri ninahakika wale wengine mngekuwa mmeshawapumzisha kwa sababu hata afya zao inaonekana si barabara lakini tena ndio yanakwenda tu.

Mhe. Naibu Spika, jambo hili kwa kweli si zuri wala halileti picha nzuri katika jamii yetu. Ndugu zetu wale wanaofanya kazi katika

sehemu zile ni wafanyakazi kama wafanyakazi wengine, lakini wanakuwa wanafanya kazi kwa hali ya unyonge. Mhe. Naibu Spika, ningeomba sana watu hawa wakapatiwa vitendea kazi kwa sababu wakipatiwa tutaviona tunakutana nao humu.

Lakini pia tuangalie juu ya usafishaji wa mji. Mhe. Naibu Spika, mimi nafikiri huu mji tusisafishe asubuhi, tuusafishe wakati watu wameshapumzika ili watakapoamka asubuhi waukute mji uko safi. Lakini ikiwa saa moja na nusu tunakwenda makazini ndio mji unasafishwa unapita pale mtu ana fyagio hata hicho kiatu kama umetia kiwi unakikuta kimejaa vumbi.

Sasa mimi ningeshauri usafi wa mji huu unafanywa wakati wa usiku ili asubuhi watu wapite mji huu ukiwa uko safi. Kama si hivyo tutaendelea kuwa tunalaumiana. Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Waziri alisimamie hili katika taasisi yako hii ili mji wetu nao ulingane na miji mingine.

Mhe. Naibu Spika, huu mji wetu ni mzuri sana lakini uchafu nao ndio umetuzidi ingawa wachafuzi ndio sisi. Maana manispaa wapo kidogo sana pale kama tutawahesabu lakini tuliokuwepo huku mitaani ndio wengi. Tnauchafua sisi lakini mnatuchaji katika kuuchafua ule mji ili nyinyi muusafishe. Kwa hivyo, chukueni bidii vizuri ya kusafisha ule mji angalau na sisi mji wetu ukipita asubuhi useme napita katika mji wa Zanzibar. Lakini unapita katika mji wa Zanzibar inakuwa kama sijui umepita wapi. Mhe. Naibu Spika, hili linasikitisha sana namuomba Mhe. Waziri tujitahidi.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninahakika watu wale kama watapewa zana za kutosha za kufanyia kazi za uhakika basi mji utabadilika na utang'ara. Tuangalie maeneo ambayo mmewapa watu katika kufanya kazi zao kama pale *Jamhuri Garden* Kisiwandui, mmempa mtu lakini kapaboresha pamekuwa pazuri sasa sisi tunashindwa nini, basi hata kuweka bustani humu.

Mhe. Naibu Spika, ukiitazama hii barabara ya Michenzani ina maeneo yamewekwa makusudi kwa ajili ya bustani lakini bustani zile hazipandwi matokeo yake sasa hivi mchanga unaoanguka barabarani ndio unachukuliwa unawekwa pale juu, kila siku unakuwa rundo pale unaongezeka tu. Sasa kesho na kesho kutwa unakuwa mchanga mwingi ikinyesha mvua unaletwa barabarani, ikipita mvua unaurejesha pale juu itakuwa tunafanya kazi ya zeze. Mhe. Naibu Spika, ningeomba tufanye utaratibu mzuri ili michanga ile iondoke tupande bustani mji wetu uweze kupendeza zaidi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mimi nafikiri niwapishe wenzangu nao waendelee kwa sababu mada nyingi zimeshazungumzwa nisirudi huko tuendelee na mengine. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana na mimi kupata nafasi hii ya kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nianze na Ofisi ya Usajili na Kadi za Vitambulisho. Mhe. Naibu Spika, vitambulisho vya Mzanzibari vina umuhimu wa peke yake kwa Wazanzibari na ndio tulikuwa tukizungumza sana nashukuru Mwenyezi Mungu akatujaalia vitambulisho hivi viko.

Mhe. Naibu Spika, vitambulisho hivi ndivyo vielelezo vya Mzanzibari katika shughuli zake kadhaa za maisha. Kwa mfano, kuwa mpiga kura, *passport*, leseni ya duka na mengineyo. Kwa mujibu wa Katiba ya Nchi Mzanzibari yeyote anayetimiza masharti na ikiwa umri wake haupungui miaka 18 anastahiki kupatiwa kitambulisho hichi.

Sasa Mhe. Naibu Spika, vitambulisho hivi pamoja na kuwa wenzangu wameshaeleza na tumeambiwa tusirudie lakini kila mtu

kwa muono wake vinasababisha kufikwa na matatizo mengi ambayo kwa kweli ni ukiukaji wa haki ya Mzanzibari. Mmoja katika mfano ulio hai ni katika shughuli za kuandikisha wapiga kura.

Mhe. Naibu Spika, wapiga kura wetu wengi safari hii tuliwakosa na hakuna nchi yoyote ambayo siku zikiendelea mbele idadi inapungua isipokuwa safari hii kwa sababu ya kutotimiza masharti kwa wale wahusika katika kuwapatia watu vitambulisho vyao vya kupigia kura kwa kupitia masharti ya kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi.

Mhe. Naibu Spika, kwa vile wizara hii inahusika na mambo haya na itaendelea na shughuli hizi kwa sababu ni haki ya kila Mzanzibari, naomba kueleza matatizo yaliyokuwepo hapo mwanzo na ambayo yalikuwa si ya msingi ili iweze kuondoka hali hii mbaya tuliyonayo ya kuwakosesha watu haki zao iondoke.

Mhe. Naibu Spika, sijui ni kwa sababu gani lakini ni kawaida kuwa panapokuwa na jambo lolote ni lazima tunaanza katika ngazi ya chini kabisa ya utawala na huku ni kwa ndugu zetu masheha. Matatizo yaliyotufika ni kwamba kulikuwa na sheria ambayo haimo katika Katiba na sheria ile ilitumika na tukajitahidi kupiga makelele mpaka kwa ngazi za juu za utawala lakini kwa baadhi ya maeneo ilibakia katika hali ile ile na kwa hivyo tukawakosesha watu haki yao bure.

Sheria ya umri. Kwa mujibu wa Katiba Mhe. Naibu Spika, ni kwamba yapo mambo yanayomfanya Mzanzibari asitumie haki yake ya kujiandikisha kupiga kura na moja ni kukosa au kushindwa kuthibitisha au kutoa kitambulisho cha umri, uraia au uandikishwaji kama mpiga kura.

Mhe. Naibu Spika, ulipokuja uchaguzi huu uliopita kulikuwa na watu wa aina nyingi, kulikuwa na watu ambao walipiga kura huko

nyuma bila ya kuwa na vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi lakini vitambulisho vya kupigia kura walikuwanavyo.

Kuna watu walikwishatimia umri na ilikuwa ni haki yao kuwa wapiga kura lakini hawakuwa na kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi. Kwa bahati moja katika masharti ni umri, pamoja na kuwa ni umri lakini haikueleza sheria kuwa hiyo aliyoitumia sheha ilikuwa sahihi kuwa ni lazima kipatikane cheti cha kuzaliwa cha *register* cha mtu huyo japokuwa ana umri unaopindukia miaka 60. Hichi ni kichekesho.

Kwa hivyo, aliyekosa haki ile ni Mzanzibari mwenye haki sawa sawa na mwengine. Kwa sababu daftari linaendelea na hata juzi tulipokuwa na hotuba ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ni kuwa tutahakikisha kwamba wote wale ambao hawakupata na wengine waliokuwa wameshatimiza masharti ya kupata watapewa haki yao.

Kwa hivyo, naomba hili suala la kuwa ni lazima uwe na cheti cha kuzaliwa *register* isiwe ni sababu ya kuwakosesha watu haki yao. Umri humu ulivyoelezwa ni kuwa na kitambulisho chochote kinachoainisha kuwa wewe umeshafikia umri ule.

Halafu jambo jengine kwa Pemba vyeti vya kuzaliwa *register* havipatikani na wazee wetu hawakuwa na uzoefu huo wa kutafuta vyeti vya *register*. Kwa hivyo, hulazimika kuja Unguja na kwa sababu ni vya miaka mingi wale watendaji hupata kazi sana ya kuvitafuta mpaka kuviona. Siku zinakwenda ratiba zinamalizika halafu tunawaacha watu wanakosa haki yao.

Mhe. Naibu Spika, naomba kwa vile tuna Serikali ya Umoja wa Kitaifa, tuna serikali iliyokuwa ni tulivu, amani na tunakwenda vizuri *Alhamdulillah.* Haya matatizo ambayo yalisababishwa na serikali yenyewe kwa kuwa kuwatumia masheha kwa sababu

ambazo zisielewi hebu tuyaondoe tuone kweli Wazanzibari tumebadilika. Hilo la kwanza.

Mhe. Naibu Spika, sitaki nizungumze mengi lakini la pili katika shughuli zangu za kamati moja katika kazi tunayoifanya ni kutembelea masoko yaliyopo katika mji wa Zanzibar na masoko yaliyopo katika kando ya mji.

Mhe. Naibu Spika, nililokuta kwa jumla kwa masoko ya Malindi, Darajani na lile soko la kuku ambalo lilikuwa lote linaonekana ni hali mbaya ya mazingira masoko yetu ni machafu sana. Huu ni mji tuna watalii na kitoweo ni kitu cha lazima na ni muhimu na hakuna kinakopatikana isipokuwa masokoni, lakini kule masokoni wengine hawendi kwa sababu ya uchafu na ni kweli uchafu upo.

Katika kutafiti kwa nini kuwe na uchafu wote huu, tuliona kuwa wote wale wanaofanya biashara mle wanalipa ada kama kawaida lakini usafi haufanywi na bahati mbaya sehemu nyengine hata maji hayapatikani. Hii ni aibu kwa mji kama huu katika sehemu muhimu kama hizo kuona kuwa hali ndio hiyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa soko la Malindi kwa sababu ya ule uchafu ulivyokuwa unakithiri hata wale wachuuzi wa samaki wamelihama lile soko wanauzia nje na wachache ndio wanaobakia ndani. Hapo nje pia sasa imeshakuwa ni *parking* ya magari chungu nzima kwa hivyo inakuwa ni fujo tena kubwa sana.

Matatizo tuliyoyapata kwa wale waliokuwemo mle ndani ni kuwa hata wale viongozi wetu wengine wanapokwenda sokoni kule hawaingii ndani lakini wananunulia kule kule nje. Yale masoko yamejengwa kwa maana yake tunataka usafi na yamejengwa vizuri, lakini ikiwa hatukuweka utaratibu mpaka yakavutia zile shughuli zikafanywa ndani itakuwa tunaharibu mazingira tunaufuja mji.

Mhe. Naibu Spika, juzi tumepata taarifa hapa kunguru laki tatu wameuliwa kwa sababu ya kuleta uchafu wa mazingira. Itakuwaje sisi sasa badala ya ule uchafu wa mazingira wa kunguru tu tunauona ni mdogo kuliko machango ya samaki na kadhalika hata hatuyashughulikii. Kwa hivyo, kwa hili lazima tubadilike. Halafu kwa bahati mbaya hata uongozi wao hatukupita tukaona pahala kuwa pana uongozi uliotimia na unaofanya kazi ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, la kusikitisha kabisa nilikwenda katika soko la Mwanakwerekwe. Kwanza Mhe. Naibu Spika, niseme lile soko tayari limeshakuwa dogo na mahitaji ni makubwa kupita kiasi. Kwa hivyo, tutajitahidi kuielekeza jamii lakini ikiwa pahala hapana budi ndio lolote lile hutendwa mpaka hivi leo bado hali haijawa nzuri. Lakini nyuma ya lile soko kuna nafasi ya kutosha na wafanyabiashara wengi wao wanajitolea kwa kuchanga pesa zao na kujenga vibanda hata kutia bati ili waweze kujiendeshea maisha.

Mhe. Naibu Spika, kwa maslahi ya wananchi wetu ambao wamejiajiri na wanatusaidia sisi tuliokuwa hatuna vifaa vile ningeliomba ifanywe kila inavyowezekana lile soko la Mwanakwerekwe liimarishwe katika sehemu yake ya nyuma ili watu waweze kufanya biashara zao ipasavyo na hapa barabarani watu waweze kupita kwa sababu sasa ni hatari tupu hapapitiki kwa magari na bidhaa ziliopo.

Mhe. Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa soko la Mombasa limehamwa, ni soko kubwa zuri lakini lina watu wachache kweli kweli wamelihama kwa sababu ya huduma ni mbovu. Mle hamna maji, hakuna uongozi, hakuna utaratibu wowote, isipokuwa watu wachache badala ya kuuza mboga mboga niliwakuta wanauza nyama ya ng'ombe. Mhe. Naibu Spika, naiomba serikali na wizara inayohusika na hili ifanye utafiti wa kina na *inshaallah* mabadiliko yaonekane.

Mhe. Naibu Spika, jengine tunayo Idara yetu hii ya Uratibu Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa ufupi ni Idara ya Vikosi. Mhe. Naibu Spika, kwanza naMshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia tukawa na vikosi vingi kabisa vya Muungano na vya Zanzibar katika nchi hii.

Lakini Mhe. Naibu Spika, kwa ufupi tu sisi hali yenyewe tumeiona tumepiga kura ya maoni, tumefanya uchaguzi mkuu, hata yule mtu muhimu sheha hakuwepo, askari hawakuonekana na tumefanya kazi kwa salama na amani. Panapotokea mabadiliko sitaki kuzungumza ya nyuma tulisema tuyasahau na sisi vile vile ni lazima tubadilike.

Hebu tuangalieni vikosi vyote tulivyonavyo na kazi wanazozifanya na kwa pesa wanayotiliwa hatuwezi tukafanya namna nyengine hawa watu tukawapatia pahala pengine hizi pesa zikatumika kwa wizara nyengine wakati tunajua kuwa katika bajeti hii wizara nyingi zinapata pesa katika asilimia ndogo sana.

Mhe. Naibu Spika, hivi vikosi vyetu kuwekwa katika mipango mingine haina maana kwamba ule ujuzi wao utatoweka. Kwa nini hatutafuti njia nyengine wakawa wanafanya kazi ya kuzalisha zaidi kuliko kutumia fedha hii nyingi mali ya wananchi. Hapa sitaki nifafanue lakini kwa sababu naamini Mwenyezi Mungu katujaalia muundo wetu wa serikali yetu hii Rais wetu Mwenyezi Mungu ampe maisha, Mwenyezi Mungu amzidishie elimu na kama mnavyofahamu amepata washauri wakubwa sana wenye uwezo na naamini anawasikiliza.

Tunae Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais ambaye Katiba inasema ni Mshauri Mkuu wa Rais na tunaye Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ambaye Katiba inasema ndie Mshauri Mkuu wa Rais. Tukaeni tuyajadili haya na hivi vikosi wakati hii ni nchi ya amani na utulivu tujue namna bila ya kutumia *formula* itakayokera ya kufanya mabadiliko. Kwa maslahi yetu hapa na kwa hivi

tunavyokwenda na kwa sababu maamuzi ya kuunda katika serikali kwa mujibu wa Katiba hayawezi kuondoka tena mpaka kura ya maoni, *inshaallah* tutakwenda safari nzuri na wenzetu waje waige.

Mhe. Naibu Spika, katika vikosi tuna kikosi cha KMKM ambacho ni Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo pamoja na doria baharini, uokozi na kadhalika. Mhe. Naibu Spika, kikosi hichi kinafanya kazi kubwa sana ya kupambana na magendo na kikosi hichi katika magendo tumefanikiwa kukamata karafuu nyingi sana za magendo, karafuu hizi zinauziwa zikishauziwa kuna wale wanaohusika wanapata *share* yao.

Mhe. Naibu Spika, hizi pesa zinagaiwa lakini katika kugaiwa kuna pesa zinaingia katika serikali kwa kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Lakini siku zote katika bajeti mapesa yote haya yanayokamatwa kwa magendo hatujayaona kupelekwa Wizara ya Fedha. Kwa kuwa hakuna wakati nauliza pesa hizi zilihalalishwa vipi mpaka zikakamatwa karafuu zikauziwa lakini pesa zile hazijulikani zilipo kwa kupelekwa kwenye wizara husika zinakapangiwa matumizi. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru, ahsante.

Abdi Mosi Kombo: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa ukarimu wako kwa kunipa nafasi hii kwa jioni ya leo. Mhe. Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake kutuleta hapa na akatuhuisha mpaka sasa hivi tunachangia.

Mhe. Naibu Spika, pia sina budi kumpongeza Mhe. Rais Dk. Ali Mohamed Shein kwa kutuongoza vizuri na kututia baraka hadi leo tunakwenda vizuri sana. Vile vile nampongeza Rais Mstaafu Mhe. Dk. Amani Abeid Karume pamoja na Maalim Seif Sharif Hamad kwa kukaa pamoja na wakati huu leo tuko katika umoja na tunafahamiana wala hatugombani.

Mhe. Naibu Spika, pia nampongeza Mhe. *Wiseman* Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa hotuba yake nzuri, yenye kupendeza na iliyopangika.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitachangia katika sehemu tatu tu. Kwanza nitaanzia katika Kikosi cha Zimamoto na Uokozi. Mhe. Naibu Spika, kikosi hichi hivi sasa nchi yetu ya Zanzibar imekuwa kubwa sana na imekua mara tatu kuliko huko tunakotoka.

Mhe. Naibu Spika, mchango wangu mkubwa mimi leo utakuwa ni ushauri tu, kuishauri serikali pamoja na wizara hii ya Mhe. Waziri. Mhe. Naibu Spika, ningelishauri kwamba vikosi vya Zimamoto vienezwe katika mikoa. Kwa sababu wazimamoto ikiwa wapo mjini tu na moto umetokea katika kijiji cha Matemwe ni sehemu ambayo inachukua meli si chini ya 39. Kwa kuwa hivi sasa magari yamekuwa mengi sijui itakwenda kwa *speed* gani mpaka zile nyumba ziwe bado ziko hai.

Mhe. Naibu Spika, ningeishauri wizara hii ijenge kituo mahsusi Matemwe cha Zimamoto. Maji yapo hayana wasi wasi pindipo yakipata mashine nzuri tu ambayo nzima na yenye nguvu, maji tunayo tunaweza tukazima moto Wilaya ya Kaskazini nzima. Kwa hivyo, ningeishauri wizara hii itujengee kituo cha Zimamoto Matemwe.

Mhe. Naibu Spika, nizungumzie Kikosi cha Valantia. Mhe. Naibu Spika, valantia ni wananchi waliokubali kuilinda nchi yetu kwa hiari yao. Mimi nakumbuka tokea uhai wa Afro Shirazi wapo valantia, lakini bado serikali haijawatazama kwa jicho la huruma. Naiomba wizara iwatazame valantia kwa jicho la huruma ili wapate motisha ya kulinda na kusaidiana na vikosi vya serikali.

Mhe. Naibu Spika, ndani ya nchi yetu hivi sasa kuna askari jamii ambao ni askari wa wananchi na wanalinda nchi yetu. Kwa hivyo,

kwa kushirikiana na valantia, polisi na hawa lazima wapewe motisha ya hali ya juu, wapewe mafunzo ya kiaskari kwa sababu nae analinda, anaweza akaambiwa sasa hivi nenda pahala kumeingia tifu hajui aende vipi. Kwa hivyo, naishauri wizara askari jamii iwape mafunzo ya kiaskari hasa.

Mhe. Naibu Spika, nizungumzie Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM). Mhe. Naibu Spika, magendo hasa yanayochukuliwa hapa ni magendo ya karafuu, lakini hata mgeni aliyekuwa anakuja hapa vibaya vile vile huwa magendo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri awape zana hawa kwa sababu wengine magendo yao wanaendea majini, anaweza mtu akaja na jahazi yake anaendea jini. Kwa hivyo, wapewe uwezo wa vyombo vinavyolingana hasa na *speed* ya majini.

Mhe. Naibu Spika, leo utastaajabu mchukua karafuu anakwenda kwa jahazi lakini hapatikani. Kwa hivyo, naomba kikosi chetu cha KMKM kitafutiwe zana za kikweli kweli hasa za kuweza kumfukuza mhalifu.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia nashauri tena, wakati majeshi yanapoandikwa, majeshi ya ulinzi ya serikali ya Tanzania yanapoandikwa, basi wizara naishauri iwatizame hasa hawa vijana wetu wa Valantia, kwa sababu hawa wanachukua muda mkubwa sana kutumikia taifa, lakini utakuta hawatizamwi hata kuchukuliwa katika vikosi vikubwa.

Kwa hivyo, naiomba serikali iwatizame sana vijana hawa wa Valangia na Askari Jamii, kwa sababu ndipo tutakapowapa nguvu wakisikia wenzao wamekwenda kule katika Jeshi la Tanzania basi na wao watapata moyo wa kuingia katika kulinda nchi yetu. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nisipoteze wakati wako, maana yake mimi nafikiri ndio karibu wa kitinda mimba.

Mhe. Naibu Spika, mimi nashukuru na ninapongeza serikali yetu ya Umoja wa Kitaifa, namuombea dua Mhe. Rais wetu Dk. Ali Mohammed Shein, awe na umri mzuri, awe na hekima ya kutuongoza. Mhe. Naibu Spika, nakuombea dua wewe nakupongeza kwa kupata wadhifa huo, Mwenyezi Mungu akujaalie utuongoze vizuri na ninaliombea dua Baraza letu hili la Wawakilishi na wao wajumbe wawe imara kuongoza majimbo, wawe na imani ya kuwaongoza wananchi wao. Vile vile nawaombe dua mawaziri wetu, tuwe pamoja, tushirikiane, tufahamiane na wawe na juhudi ili na sisi wakati tunapowaambia njooni majimboni kwetu, basi waje mara moja.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Matemwe naiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi).*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa na mimi fursa ya kuchangia bajeti hii ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nimpongeze Mhe. Rais wetu wa Zanzibar, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais na kuliongoza taifa letu la Zanzibar. Pia nimpongeze Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais kwa kushika hatamu hii ya kumsaidia Mhe. Rais. Vile vile nisisahau kumpongeza Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, Mhe. Seif Ali Iddi ambaye tunaye humu Baraza.

Mhe. Naibu Spika, naomba nianze katika ukurasa wa 44 kifungu cha 85.2, hii inazungumzia tawala za mikoa. Mhe. Naibu Spika, Waswahili wanasema ‘mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni’. Maana ya kusema hivyo ni nini, Mhe. Rais wa Zanzibar alipofanya ziara Pemba, alitembea na baada ya kwishakutembea Mkoa wa Kaskazini, katika majumuisho alisema maneno haya yafuatayo.

Kwa sababu ya kusema hivi nimeona hapa katika kitabu hiki cha bajeti kuna sehemu ambayo inazungumzia uchafuzi wa mazingira. Ni katika sehemu ya swahiba wangu Mhe. Hija Hassan pamoja na sehemu ile ya Mhe. Hamad Masoud Kangagani Ole pamoja na Micheweni kwamba sehemu hizo ndio zinazokidhiri kwa uchafuzi wa mazingira.

Lakini Mhe. Rais alipotembelea kule na katika majumuisho yake, aliisifu sana Micheweni na akatoa mfano akasema kwamba naomba mujifunze kutoka Micheweni, kwa sababu Micheweni pamoja na kuchimba matofali, lakini kwanza wanachimba kujua kwamba hapa panatosha hapaendi kwenye uchafuzi wa mazingira na halafu wanapanda miti.

Sasa Mhe. Waziri kwa nini hukutusifu Micheweni na hukutupa haki yetu, ukatuonea na ukasema hivi. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, naomba ‘mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni’. Kwa hivyo, mtusifu Micheweni tunajitahidi na Mhe. Rais ndivyo alivyosema na muheshimu ile kauli ya Rais na sisi mtusifu. Kuna mengi ambayo mnatulaumu, lakini lile ambalo tunafanya zuri basi mtuambie. Hilo ni moja.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo niende kwenye ukurasa wa 30 kuhusu usajili wa vitambulisho. Mhe. Naibu Spika, naomba nizungumze kidogo katika suala la vitambulisho. Nawasifu sana wenye kazi za vitambulisho, lakini nawalaumu sana.

Kwa nini niwalaumu, hivi Mhe. Naibu Spika, mzee kama Mhe. Makamo wetu wa Pili wa Rais, Mzee Seif Ali Iddi, anakuja basi ukiutizama tu ule umri wake hujajua tu kuwa huyu mtu anastahiki kupewa kitambulisho, unamwambia lete cheti cha kuzaliwa, mzee kama huyo unamwambia aje na cheti cha kuzaliwa atakipata wapi. Mnawajua wazee wetu zamani walikuwa hawana habari ya vyeti vya kuzaliwa.

Kwa hivyo, waheshimiwa nawaomba pamoja na sheria tuliyonayo, lakini tuangalie na wale wazee tuwape heshima zao, kwa sababu mzee ana heshima ya pekee. Lakini kuna wazee wametaabishwa wakitaabishwa, na sasa hivi vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi ni mali. Kwa sababu huwezi kupata pesa benki kama huna kitambulisho, huwezi kutambuliwa kupata hata kazi kama huna kitambulisho.

Leo wazee wetu wanaotulea, anakuja mzee kama baba yangu mimi anayenizaa, hajaondoka yuko pale pale ana miaka 80, kisha unamwambia kuwa hupati uje na cheti chako cha kuzaliwa. Mhe. Naibu Spika, naomba suala hili Mhe. Waziri uliangalie kwamba wazee wetu wafanyiwe utaratibu wa kupata haki zao, kwa sababu ni haki zao.

Mhe. Naibu Spika, nakwenda haraka haraka naondoka hapa. Naomba niingie katika ukurasa wa 76 kwenye idara na vikosi maalum. Mhe. Naibu Spika, wazee wanasema kwanza ukitaka upate sifa basi umuheshimu baba yako, ukishamuheshimu baba yako basi na mtu mwengine yeyote atamuheshimu, lakini kwanza uanze kumuheshimu wewe. Lakini ukianza kumkosea heshima baba yako wewe mwenyewe basi na mtu mwengine yeyote huko nyuma atakayekuja hatomuheshimu.

Mimi Mhe. Naibu Spika, nawalaumu sana vikosi vyetu vya idara maalum vya Zanzibar na ninawasifu sana askari polisi wetu, pamoja na kuwa wana muundo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini nawasifu. Kwa nini niwasifu wao.

Kwa sababu wanajua wajibu wao, mtu anapokuwa na cheo anachopewa na Mwenyezi Mungu basi ni dhamana, cheo ni dhamana. Leo unayo wewe na kesho anakua nayo mwenzio, pale yule mtu anayestahiki anapopewa cheo basi aheshimiwe. Leo kwa nini askari wa vikosi vyetu hawataki kutuheshimu.

Mhe. Naibu Spika, kwa masikitiko, mimi nimewahi kukamatwa tai hapa na askari wa Nevi, kanikamata tai mkoani ananiambia pamoja na uheshimiwa wako nataka kukutia adabu. Kwa nini iwe hivyo, yeye keshaambiwa huyu ni mheshimiwa, basi anasema pamoja na uheshimiwa wake nataka kumtia adabu.

Mhe. Naibu Spika, nasikitika sana kwa sababu unapokuwa mheshimiwa basi unaheshimiwa kweli na unatakiwa wewe mwenyewe ujiheshimu ili uheshimiwe. Kama ni hapo zamani nilipokuwa sio mheshimiwa tungekamatana tai pamoja, lakini niliheshimu uheshimiwa wangu. Kwa nini watudhalilishe vikosi maalum.

Namuomba Mhe. Waziri kwa hili azungumze na vikosi vyetu vya Zanzibar, kama cheo ni dhamana, leo ninayo mimi na kesho anayo mwenzangu watuheshimu bwana, kwa nini watuondolee heshima. Naamini kwamba haya ninayofanyiwa mimi na mwenzangu siku ya pili atafanyiwa. Kwa hivyo, unakuwa na dhamana na ikishakuondokea tu basi, lakini pale unapokuwa na dhamana basi heshima yako upewe.

Naomba Mhe. Naibu Spika, hili lionekane na namuomba Mhe. Waziri kwa kupitia Baraza letu la Wawakilishi wapewe orodha ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika maofisi yao wote, kama hawatujui basi watujuwe.

Lakini hata hivyo mimi nasema wanatujua, kwa sababu alisema pamoja na uheshimiwa wake na ilikuwa moja kwa moja mimi niko tayari kumchukulia hatua ya kumpeleka mbele, lakini nilinasihiwa sana, kama mwanadamu nikakubali. Lakini kwa nini watufanyie hivi, kwa masikitiko kabisa ni lazima waambiwe na wajuwe kuwa sisi ni viongozi wao kwa muda huu, kesho ikiwa nafasi sina basi ataheshimiwa mwenzangu aliyepo.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo nataka nilizungumze ni kuhusu majengo ya serikali katika sehemu za Ikulu. Nimeona katika kitabu hiki miradi inayokusudiwa kurekebishwa katika bajeti hii, lakini katika kuangalia sikuona Ikulu iliyoko Micheweni kama na hiyo imo katika mpango huu. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anieleze. Kwa nini na ile imejengwa ni Ikulu ya Mhe. Rais atakapokuja Micheweni ili apate sehemu, kwa nini imesahauliwa au haitaki kujengwa tena imeshaachwa moja kwa moja.

Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anieleze, kuna sababu ipo kwa sababu ilijengwa zamani ile, kwa nini isimalize ikatumika au tunaiweka kama ni kiyoo kile twende tukaiangalie tu. Sisi watu wa Micheweni tunataka ile iwe ni Ikulu itumike atakapokuja Mhe. Raia na viongozi wengine wafike na wapate wapumzike. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri anieleze kwa nini suala hili likawa limewekwa upande.

Jengine ambalo nataka nilizungumze Mhe. Naibu Spika, nataka niipongeze sana Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni, kwa nini nataka niipongeze sana halmashauri hii. Mhe. Naibu Spika, kama mnavyojua wote kwamba Micheweni ni Wilaya inayosifiwa kuwa ni wilaya ya watu wanyonge, kwa hivyo wilaya ikiwa na watu wanyonge basi na nyenzo zake zinakuwa vile vile ni nyonge. Sasa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ilipangiwa kukusanya milioni 20, lakini hadi kufikia mwezi wa Machi, imekusanya milioni 30 sawa na asilimia 150.

Mhe. Naibu Spika, kwa fununu niliyonayo katika kuzunguka zunguka na kuangalia katika maendeleo ya wilaya yangu, hadi kufikia mwezi huu wamekusanya milioni 40 ambayo ni sawa na asilimia 200. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, naipongeza sana, pamoja na unyonge tuliokuwa nao, naiopongeza kweli kweli Wilaya ya Micheweni. Naomba Mhe. Waziri na yeye aipongeze Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni.

Kwa nini Mhe. Naibu Spika, niseme hivi. Mhe. Naibu Spika, hazikukusanywa tu hizi pesa ovyo ovyo, lakini ni jitihada ya Katibu wa Halmashauri pamoja na madiwani waliopo kwenda sambamba ili kuzikusanya zile pesa na kuziweka. Kwa hivyo, nawapongeza sana.

Mhe. Naibu Spika, nataka kidogo kwa sababu wajumbe wameshalizunguza sana, niligusie kidogo suala la manispaa. Mhe. Naibu Spika, manispaa imezungumzwa sana na wenzangu wametoa ushahidi wote wa kutosha na kila kitu kimeonekana. Nataka nimuulize Mhe. Waziri, hivi kuna uzito gani mtu anapofanya kosa na likaonekana kwamba hili ni kosa tunamlinda, kwa nini tumlinde. Hivi serikali yetu kwa nini hatuna utamaduni mtu anapofanya kosa kama hili likionekana dhahiri tukamuwajibisha kwa nini, kuna uzito gani.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja atuambie kwamba huyu mtu tutamuwajibisha au atume maelezo mazuri zaidi. Mhe. Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi).*

Mhe. Asha Abdu Haji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema jioni hii. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii ili kuweza kutoa mchango wangu mdogo katika bajeti hii ya Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, naomba kumpongeza Mhe. Waziri kwa kuleta hotuba yake hii iliyojaa mambo mengi. Vile vile naomba kumpongeza Mkuu wa Mkoa wa Kusini kwa kujenga afisi yake pale ilipo. Kwa hakika amefikia kwenye kazi kubwa na kuweza kusaidiwa, jengo lile linahitaji asaidiwe, hivyo ningemuomba Mhe. Waziri alione jengo lile kwa pale lilipofikia.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amsaidie Mkuu wa Mkoa wa Kusini kwenye lile jengo kwa pale lilipofikia liweze kumalizika ili linapomalizika alitie vifaa kama meza, viti pamoja na vifaa vya afisini. Ni muhimu sana Mkuu wa Mkoa wa Kusini kusaidiwa kumaliza lile jengo ili afanikiwe, kwa vile pale lilipo hivi sasa lile jengo Koani afisi haina nafasi na ni duni.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuchangia kidogo kuhusu madiwani. Madiwani wanafanyakazi kubwa lakini serikali bado haijawaona. Kwa kuwa masheha wanalipwa mishahara na madiwani wanafanyakazi kama watoto yatima. Kwa kuwa madiwani wamechaguliwa kama sisi wawakilishi na wabunge, basi sioni haja ya kwa nini hawalipwi mshahara. Mhe. Naibu Spika, ningemuomba Mhe. Waziri alete mageuzi ya kuweza kuwasaidia madiwani walipwe mishahara kama wanavyolipwa wabunge na wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja, naipongeza kwa kuchangia mapato, kwani halmashauri hiyo ilijipangia yenyewe kuchangia mapato yake milioni 56.2, lakini mpaka sasa hivi imechanga milioni 64.

Mhe. Naibu Spika, ni juhudi nzuri iliyochukuliwa kwa halmashauri hii kwa mapato ili kuweza kuondoa umaskini hasa kwa wanawake wa Wilaya ya Kusini. Naupongeza sana uongozi wa Halmashauri hii ya Wilaya ya Kusini.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa mapato haya yatawaondolea wananchi katika kulipa kodi zao katika Wilaya ya Kusini.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii, naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia, mimi pamoja na wananchi wangu wa Wilaya ya Kusini, iwapo madiwani watalipwa mshahara kama tunavyopewa sisi.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi ya kuchangia jioni hii, ingawa wajumbe wameshachangia sana na mimi nitajitahidi kadiri ya uwezo wangu kutoa japo yale ambayo nimeyakusanya hapa.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri iliyojaa ufasaha. Pia nichukuwe nafasi hii kuwapongeza watendaji wa wizara yake kwa njia moja au nyengine wamemsaidia hotuba hii hadi kufanikiwa na kuweza kuisoma mbele ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Naibu Spika, nichukuwe nafasi hii tena kuwapongeza watendaji wote walioteuliwa na Mhe. Rais, naamini Rais hakufanya kosa, aliwateuwa kwa kuwa alijua wanaweza kumsaidia katika utendaji wao wa kazi.

Mhe. Naibu Spika, nianzie kwenye ukurasa 28 kwenye kitengo cha usalama kazini *GSO*. Mhe. Naibu Spika, dhana iliyokuwepo hapa ni nzuri sana ya kupata watendaji bora na ni watendaji ambao tutaweza kuamini kutekeleza majukumu yao bila ya kuwa na usumbufu wowote.

Kitengo hiki ni kitengo muhimu sana, lakini ni wizara moja tu ambayo mpaka sasa hivi ambayo ndio inayopita pale *GSO*. Hivi karibuni Wizara ya Habari, Utamaduni na Utalii na Michezo ndio imepeleka watu wake wa kupitia hoteli ya bwawani. Wizara ya Fedha imekuwa ndio muhimili mkubwa, lakini nayo ina mapungufu yake, ina waajiri kwanza wafanyakazi pale halafu ndio inawapeleka *GSO*. Wizara ya Fedha ndio macho yetu.

Kwa hivyo, ukenda tu pale kwa wale watendaji, ukawaambia tunawaajiri ambao bado hatujawapeleka *GSO*, basi tunaweza tukawaajiri pale wafanyakazi wakawa majambazi, tukawaajiri wafanyakazi ambao sio na pengine tukawaajiri wafanyakazi ambao sio raia wa nchi hii. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri

au namshauri ili watendaji wote wapitishwe katika *GSO* tuweze kupata watendaji waliokuwa bora zaidi.

Mhe. Naibu Spika, naomba nichangie kwenye ukurasa wa 45 kuhusu ujengaji wa mitaro ya maji ya mvua. Kwenye ukurasa huu umetajwa maeneo mengi ikiwemo Magomeni, Mpendae kwa Biti Amrani pamoja na Jang'ombe, dhana ni nzuri na itatuondoshea usumbufu mkubwa. Kama mimi katika Jimbo langu la Mpendae kwa Biti Amrani lile ni bwawa la siku nyingi sana. Wananchi wengi zikija mvua za masika basi wanapata mafuriko makubwa. Naipongeza sana serikali kwa kutekeleza zile ahadi zake ilizotoa katika kampeni. Hii inaonesha wazi ni kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, kuna dogo ambalo liko katika sehemu ya Migombani, katika Jimbo la Mpendae na Jimbo la Mhe. Mahmoud Muhammed swahiba wangu wa Jimbo la Kikwajuni. Msingi ule umekuwa ni kero na umekuwa ni kadhia kubwa. Pale waliwekwa wafanyakazi wa Baraza la Mji ambao sasa wamestaafu na hawakuwekwa tena. Tulichukua hatua ya dharura mimi na Mhe. Mahmoud angalau basi kuweka watu wa majirani na tukaweza kuwalipa ili ule msingi uende vizuri.

Sasa nakuomba Mhe. Waziri utakapokuja hapa katika majumuisho yako uweze kuniambia ni lini utaweka wafanyakazi wa kudumu pale au mimi Jimbo langu la Mpendae litakuwa gumu kidogo kwenye kupitisha bajeti yako.

Mhe. Naibu Spika, nakuja katika Mkoa wa Kusini Unguja, tunamshukuru sana kwa dhana nzima na nzuri Mhe. Mkuu wa Mkoa kwa kujenga jengo lile lililokuwepo Tunguu. Lakini tunataka tumwambie kuwa viwanja vimekuwa mali au ardhi imekuwa mali, huu mpango wa kujenga nyumba za chini kwa umaarufu mabanda umepitwa na wakati. Tujaribu kutumia sehemu zile tunazopewa tujenga nyumba za ghorofa, hata ikiwa

bado basi tuanze msingi imara wa kujenga nyumba za ghorofa na hatimaye kunyanyua juu. Tunampongeza sana kwa dhana yake hii na tunamuomba aendelee kama dhamira yake ilivyokuwa.

Mhe. Naibu Spika, nakuja kwenye KVZ. KVZ ni vikosi vyetu ambavyo mimi navipongeza sana, hata jana tu kiasi cha saa 5:00 za usiku katika Jimbo langu la Mpendae ulitokea moto mkubwa sana, lakini nawapongeza waliwahi kwa wakati, wakaleta gari mbili na kuuwahi moto wenyewe. Nawapongeza sana na ninamwambia Mhe. Waziri watu hawa wapewe kipaumbele na wapewe dhana tosha ili waweze kutuhudumia kama walivyonihudumia mimi jana katika jimbo langu.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye JKU, dhana ya JKU ni Jeshi la Kujenga Uchumi na sasa hivi Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili anasema yeye amekuja na mapinduzi ya kilimo, ametuletea mbegu bora ya nerika, tunaikubali.

Pia ningeona tufanye mapinduzi ya kilimo katika JKU, tuweze kuwapa dhana bora ili waweze kulima mboga mboga, ambapo mboga hizo tayari walaji wapo, soko la kutosha lipo, mahitaji yapo. Tuweze kuleta mapinduzi ya kilimo hadi kuhakikisha tunatimiza lile lengo ambalo tumelikusudia. Hiki ni kikosi muhimu sana na kama tutaweza kukihudumia basi tutaleta kweli mapinduzi ya kilimo katika jeshi hili la JKU.

Mhe. Naibu Spika, mimi kidogo nigusie kwenye masoko. Masoko yote yaliyokuwepo katika mji wa Unguja ni dhana nzima na nzuri kabisa ya Rais wetu Aman Karume aliyeyadumisha, kuanzia soko la Mwanakwerekwe, soko la Malindi na soko la Darajani. Lakini haya yote yamegubikwa na uchafu mnene uliokuwepo pale, kuna sehemu hata utaona tabu kwenda kama unakwenda kuuza kitu halafu wakenda kutumia walaji.

Mhe. Naibu Spika, kiingilio cha pale kwa wale wafanyabiashara, mwanzo tulikuwa tukiambiwa wanakata Shs. 500/= ile kodi ya kila siku. Lakini baada ya muda kidogo tukaona risiti nyengine zina kodi ya Shs. 1,000/= tulishangaa sana tulipopita pale. Inaelekea kodi zile ni nzuri, azma ni nzuri ya pale, lakini bado mapato hayajulikani wapi yanapokwenda.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri atakapokuja hapa kwenye majumuisho yake, namuomba basi aweze kuniambia masoko yale yanakusanya shilingi ngapi kwa mwezi, maana yake bado pana ubabaishaji mwingi ambao unaweza kutokea.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye manispaa yetu ya Zanzibar. Kwenye Serikali Kuu tulitajiwa kuna bilioni 38, lakini kwenye kitabu chake Mhe. Waziri hakuweza kutueleza.

Sasa tunaanza kujiuliza pesa zile ni za nani, zimekwenda wapi au Manispaa itafanya nini. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja hapa aweze kunipa maelezo kuhusiana na suala hili. *(Makofi)*.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja hapa atueleze, yaani afanye *review* ya ile Manispaa nzima juu ya uendeshaji wake, kuchukua kodi, kwa sababu bado inaonekana ile hali ni tete.

Lakini tunaimani kubwa sana kwamba Mhe. Waziri ameshajipanga na hili na ataweza kuliweka katika hatua nzuri zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nisichukue muda mwingi sana, sasa nichukue nafasi hii mimi mwenyewe binafasi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Mpendae kuunga mkono hoja kwa asilimia 99. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi na kuweza kuchangia kuhusu hoja iliopo mbele yetu, pamoja na kwamba watu wengi wameshachangia lakini na mimi nitakuwa nikizunguka humo humo, ili niweze kutia nyalio. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha siku ya leo tukiwa hai na hatimaye kutupa nguvu za uwezo wa kuingia katika Baraza hili tukufu na kuweza kutoa michango yetu. Aidha nitumie fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi. *(Makofi)*

Vile vile nisisahau kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mhe. Waziri pamoja na wataalamu wake kwa kuweza kukitayarisha kitabu hiki, Mhe. Waziri kuweza kukiwasilisha kitabu hiki kwa muda wa masaa mawili na kidogo bila ya kuhema wala kumeza mate, kwa hili nampongeza sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza niende katika hii Idara ya Utaribu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kwanza niipongeze idara hii kwa kuweza kufanyakazi nzuri ya kutoa mafunzo kwa Masheha 332 wa Zanzibar nzima pamoja na Madiwani 141. Nadhani mafunzo haya yatawasaidia sana viongozi wetu hawa, kwa sababu huko tunakotoka kama kulikuwa na viongozi waghasi ambao hawasikii lolote ni hawa Mashesha.

Kwa kweli Masheha ilikuwa ni tatizo Mhe. Naibu Spika. Kwa hivyo, nadhani taaluma hii waliyoipata kwa kiasi fulani inaweza kuwasaidia. Lakini wasipewe taaluma tu katika mambo haya ya uongozi, nafikiri ni vyema Mhe. Waziri aendelee kutoa taaluma na dhamira halisi ya *Government of National Union (GNU).*

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu dhamira ya *GNU* ni kuwaunganisha Wazanzibari pahala pamoja bila ya kujali itikadi

zao za kisiasa. Kutokana na hali hiyo, nafikiri Masheha wanahitaji sana taaluma hii Mhe. Naibu Spika. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba aendelee kuwasaidia viongozi hawa, kwa sababu hawo wako katika *root*. Sasa wakeshaielewa wao dhana hii ya kwamba dhamira ya *GNU* ni kuwaunganisha wananchi na wao wako kwa wananchi, basi nadhani wataisadia sana serikali katika kuwaunganisha wananchi wa nchi hii na kuwa kitu kimoja, bila ya kujali tofauti zao za kisiasa au dini.

Hivyo, nampongeza sana Mhe. Waziri na ninaiomba serikali kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba iendelee kuwapa mafunzo viongozi wetu hawa, yaani Masheha pamoja na Madiwani wetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kama walivyoeleza wenzangu ambao tayari wameshachangia sana kwamba kama kuna watu ambao wenye kazi ngumu tena ya kupigiwa mfano ni Madiwani. Kwa kweli hawa Madiwani mpaka kuupata huo Udiwani basi kuna kazi kubwa sana. Kwa mfano, waende kwa wananchi na kupapatua ndio wapata Udiwani, baada ya kupata huo Udiwani aisaidie serikali katika kuleta maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, hivi ninavyozungumza ni kuwa kazi za Madiwani ni kubwa sana. Kuna sehemu nyengine watu wanakuwa sugu kwa ajili ya kulipa kodi mbali mbali, yaani watendaji wa Halmashauri wanashindwa kupata kodi inabidi lazima aingie Diwani. Kwa kweli wanapoingia Madiwani wanasaidia sana watendaji kuweza kukusanya kodi mbali mbali. Kwa mfano, hasa sehemu za Micheweni na Kojani ni tatizo watu kulipa kodi mpaka waingie Madiwani.

Kwa hivyo, kazi hii wanayofanya Madiwani ni kubwa nadhani Mhe. Naibu Spika, atakaposimama Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kojani anaweza kuelezea vizuri kuhusu Wakojani walivyo, yaani

kulipa kodi inakuwa ni tatizo kwa kumpeleka mtendaji wa Halmashauri inakuwa ni tatizo mpaka waingie Madiwani wetu. Sasa Madiwani wetu wanatembea bila ya viatu, nguo zimetiwa viraka.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa umefika wakati kwa viongozi wetu hawa serikali kuwaona kwa jicho la huruma kwa kuwalipa mishahara, kwa sababu ni viongozi wanaojitahidi sana katika kuchochea maendeleo katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Nikiendelea na idara hii sasa niingie kwa Wakuu wa Mikao na Wilaya. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mkuu wa Mkoa ni mwakilishi wa Rais wetu katika Mkoa huo, kwa hiyo ofisi yake pamoja na yeye mwenyewe wanatoa taaswira, yaani wanatakiwa watoe taaswira ya nchi yetu. Kwa kweli wanahitaji wawezeshe Makuu wa Mikoa kwa ajili ya kutoa taaswira ya nchi yetu, yaani kuanzia ofisi zao mpaka wao wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, Wakuu wetu wa Mikoa wanayo bidii, uwezo wa kufanyakazi, lakini inaonekana kwamba serikali mpaka hivi sasa bado hawajataka kutoa uwezo kwa Wakuu wa Mikoa yetu kuweza kumuwakilishi Rais wetu vilivyo pamoja na kutoa taaswira ya nchi yetu.

Kwa mfano, sisi kule Pemba Mhe. Naibu Spika, Rais wetu Makao Makuu yake ni huku, sasa huwa tunapata wageni wa ndani na nje ya nchi hii, kama vile wanaweza kuja Marais au Mawaziri wa nchi mbali mbali kuja kutembelea kisiwa kile, sasa wanapofika wanafikia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa au Mawaziri.

Vile vile kama juzi angekuja Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje wa Marekani angefika Pemba, basi angekwenda ku-*pay courtesy* kwa Mkuu wa Mkoa Kusini Pemba. Mhe. Naibu Spika, nadhani Wamarekani wasingekubali kuingia katika jengo analofanyiakazi Mkuu wa Mkoa.

Kwa kweli Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kusini Pemba nafikiri haifai hata kumpa Sheha ofisi ile. Sasa kama angekuja Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje wa Marekani na kusema aende ku-*pay courtesy* kwa Mkuu wa Mkoa Kusini Pemba, basi Wamarekani wangemzuia asiingie katika jengo lile.

Mhe. Naibu Spika, ni jengo ambalo ni la kurithi, uchochoro. Pamoja na hayo, nampongeza sana Mkuu wa Mkoa kwa kufanyakazi katika ofisi ile kwa bidii.

Kwa hivyo, naiomba serikali kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, itoe umuhimu sana katika kujenga ofisi za Wakuu wa Mikoa, kwa sababu wao ni Wawakilishi wa Rais katika mikoa na Viongozi wa Kimataifa wanafika katika ofisi zao na wala tusiidhalilishe nchi yetu, hivyo, ni vyema tuweke vipaumbele.

Mhe. Naibu Spika, tukienda katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake ananing'inia kwenye gofu, yaani ofisi yake ni gofu tena yuko juu ananing'inia na hii ni hatari Mhe. Naibu Spika. Kwa hivyo, nadhani tutoe vipaumbele kwa hizi Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya kusudi ziweze kutoa taswira halisi na wala sio masikini kiasi hicho sisi Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Kwa kweli juzi Mhe. Mjumbe mwenzangu alisema uchumi tunao lakini tunaukalia na wala sio masikini kiasi hicho Mhe. Naibu Spika. Sasa kumning'iniza Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake kwenye gofu lile hatuna umasikini kiasi hicho. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naomba Mhe. Naibu Spika, tutoe umuhimu katika mambo, yaani *Governor* lazima aonekane kama ni *Governor* na sisi tunaye pale tena anaiweza kweli rafiki yangu, ingawa mimi hanipendi Mkuu wa Mkoa wa Kusini, lakini kazi ya Ukuu wa Mkoa anaiweza sana, basi naomba apatiwe ofisi nzuri. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba niende Idara ya Uratibu wa Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Nianze na Kikosi cha JKU kwa kweli hawa vijana napenda niwapongeze sana, yaani wanabidi sana ingawa hawawezeshi, lakini wanabidi sana naamini wakiwezeshwa vijana hawa basi Nerika inaweza kuleta maendeleo katika nchi hii, tuwasaidie vijana wetuu wa JKU. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hivyo, ninachokiomba Mhe. Naibu Spika, ni kwamba Vikosi vya JKU, KVZ na KMKM hivi vyote ni Vikosi vya SMZ na ajira zake huko nyuma iliwa wanfanya *bias* katika kuwaajiri wananchi. Kwa kweli hawana wanapata mishahara yao kupitia kodi za wananchi, yaani wananchi ambao wanatoa kodi bila ya kujali wao ni wa chama hiki na wenye rangi hii.

Mhe. Naibu Spika, naomba uajiri wa vikosi hivi usijali huyu ni wa chama gani. Kwa mfano, sisi tumo kwenye Baraza na tunaishi kama ndugu, basi na hawa wasiwe na ubaguzi, hivyo wawaajiri vijana wetu bila ya kujali *political grounds*. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba niende Chuo cha Mafunzo. Mhe. Naibu Spika, hapa pia kuna tatizo vyuo vya Mafunzo vyetu vina matatizo, kwa sababu hapa ni katika maeneo hatarishi na juzi tulikuwa tukizungumzia maeneo hatarishi kuhusu masuala ya UKIMWI wakati tulipokuwa tukijadili hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, wale watu wanaopelekwa pale ni wanafunzi na wala sitaki niwaite wafungwa. Kwa kweli pale tunawapeleka wanafunzi kwa ajili ya ku-*change mindset* kutoka uhalifu na kuwa raia wema. Lakini mazingira ya Chuo cha Mafunzo hawawezi kubadilisha *mindset* zao na kuwa raia nyema, kwa sababu hulka na tabia za pale hazimfanyi mtu abadilike.

Mhe. Naibu Spika, mimi ni mzoefu katika magereza yetu kwa sababu nimeshakaa sana. Kwa mfano, kila wakati wa uchaguzi ndio lazima niende Chuo cha Mafunzo isipokuwa uchaguzi huu tu na ninaishukuru sana Serikali inayoongozwa na Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein pamoja na utendaji Mkuu wa Mhe. Balozi Seif Ali Iddi haikunipeleka kule. Kwa kweli wale wanaopelekwa ni raia tena wanazo haki zote za msingi za kiraia wanatakiwa wapate. *(Makofi)*

Kwa mfano, mtuhumiwa bado hajawa na makosa na wanasheria wanajua hivyo, sasa leo anachukuliwa mtuhumiwa na kupelekwa kwenye mtondoo na wenzake kiasi ya ishirini, yaani kwenye nyumba kimoja wanalala watu ishirini na pale kuna mtondoo unataka kufanya haja kubwa kwenye mtondoo, hivi kweli huyo ata-*change mindset* wakati atakapotoka. Mhe. Naibu Spika, kwani kinyesi utakuwa unakichukia mpaka utakipenda na hii ni aibu.

Kwa kweli kuna kipindi fulani mimi nilikaa muda wa mwezi mzima asijafanya haja pale, kwa sababu huwezi kufanya haja na huku watu ishirini wanakuangalia wewe, basi nilipata ugonjwa na ikabidi nifanyiwe *operation*. Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kuwa Hamabusu kujengwe vyoo na wala UKIMWI haumalizi, kwa sababu mtu atakapokwenda haja watapenda mambo ya kulawitiana wale. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, samahani lakini magereza zetu ni mbaya sana na tuzisaidie. Kwa hiyo, kwa sababu wale ni binadamu sasa wanapokwenda pale na kupewa maharage yakiwa na mafunza, nadhani ni vizuri tuwasaidie. *(Makofi)*

Sasa niende katika Kikosi cha KMKM. Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nikipitia Ripoti Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kipindi cha mwaka 2008/2009. Katika kupitia ripoti hii

ukurasa wa 39 kwa idhini yako Mhe. Naibu Spika, naomba uniruhusu ninukuu kidogo.

Ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali 2008/2009 ukurasa wa 39 unasema hivi:-

"Kamati ya Ukaguzi wa Kikosi cha KMKM (*Audit Committee*), kwa mujibu wa Kanuni za Fedha za Zanzibar mwaka 2005 kifungu Nam. 28 Kikosi cha KMKM kimeshindwa kuunda Kamati ya Ukaguzi na kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Kanuni za Fedha za Zanzibar ya mwaka 2005.

Vile vile kuna vyaraka za fedha ambazo zimepelekwa kwenye Kikosi hiki cha KMKM. Nyaraka za Uingizaji wa Fedha ambazo hazikupatikana kwa ukaguzi, yaani kuna Nyaraka za Fedha ambazo zilipelekwa KMKM hazikupatikana kwa ukaguzi nyaraka hizi zinathamani ya shilingi milioni mia saba thamanini, laki moja na sitini na mbili elfu na kumi na nne.

Mhe. Naibu Spika, kuna nyaraka ya tarehe 04/08/2008 yenye kumbukumbu Nam. MFEA/B10/07/15 hii ilikuwa nia shilingi milioni mia tatu na tisiini, thamanini na moja elfu na saba. Pia kuna nyengine ya tarehe 29/08 kumbukumbu yake ipi vile vile na wala sitaki niinukuu tena. Lakini ile ya zamani ya shilingi milioni mia tatu na tisiini, thamanini na moja elfu na saba, nyaraka hizi hazikuonekana kwa ajili ya ukaguzi.

Aidha kuna fedha za kazi za maendeleo kuna dhamana ya shilingi milioni 52,521,300/-. Ukaguzi

umebaini kwamba jumla ya shilingi 52,521,300/- zimetumika kwa ajili ya kazi za maendeleo, lakini uthibitisho wa matumizi hayo haukupatikana kwa ukaguzi".

Mhe. Naibu Spika, sisi Baraza la Wawakilishi ndio mchungaji wa fedha za walipa kodi, yaani hizi ni fedha za walipa kodi. Sasa leo anakuja Mhe. Waziri tumpe tena fedha kwa ajili ya kwenda kuwapa Kikosi cha KMKM bila ya kupata mahesabu haya hivi inakuwa vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa na unyenyekevu wa hali ya juu naomba Baraza hili lizuie bajeti hii mpaka pale tutakapopata hesabu hizi. Kwa kweli, wananchi hawataelewa kwamba sisi tutoa fedha zao na kutumika bila ya *accountability*, nadhani tutaonekana wapumbavu. *(Makofi)*

Nikiondoka hapo sasa niende kwenye Baraza la Manispaa na wala sitaki nizungumze sana. Lakini katika kudumisha usafi wa mji wetu kunguru laki tatu waliuliwa. Mhe. Naibu Spika, hao wataalamu wamefanya *analysis* ya hali ya juu, kwa sababu kuondosha kunguru laki tatu ndio kuondoa tatizo au kuzidisha tatizo.

Kwa hivyo, kwa sisi ambao kidogo tunajua taaluma ya biolojia na viumbe, tunasema kwamba *there is a balance of nature* katika *ecosystem or biological equilibrium*, kwa sababu *there is interdependence of food between living organisms*. *(Makofi)*

Kwa kweli kuna mnyororo wa kutegemeana chakula, sasa unapoondosha kunguru laki tatu na unawaweka wapi panzi na nzige watakuwa hawana *natural enemy*. Kwa hiyo, itakosekana *balance of nature* na hiyo Nerika tukija kuipanda itakapovamiwa na nzige basi itakuwa nzige hwana maadui na hiyo ni *scientific analysis* ninayoitoa Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Sasa ikiwa Nerika tumeshaipanda sisi na wakaingia nzige na hawa maadui wao ni kunguru na tayari umeshawaua laki tatu na mpunga utaliwa na nzige. Kwa hivyo, nadhani ni vyema wakakae wataalamu na kuona utaratibu gani katika haya mambo ya *biological equilibrium or balance of nature*. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa ni tatizo, kwa sababu ni mbaguzi wa hali ya juu. Kwa kweli huyu bwana anawabagua wafanyabiashara pale Juakali na hapa ninayo barua ambayo amepelekewa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi hawa jamaa wanajiita JUWAMADA, wamempeleka malalamiko yao kwa jinsi anavyowabagua yule jamaa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hawa jamaa kama ningekuwa na muda ningeelezea jinsi wanavyolipa kodi, kwa sababu hawa kila mwaka wanalipa karibu shilingi milioni 76 na zaidi. Sasa hiki kipindi yale maduka yalipozuiliwa basi zaidi ya shilingi milioni 40 zimekosekana katika kipindi hiki. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, ametumia kiasi gani kwa ajili ya kuwalipa walinzi wa KMKM pamoja na JKU katika kipindi kizima kile walipowazuia wafanyabiashara wasifanye biashara pale.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo kwa heshima na taadhima pamoja na unyenyekevu wa hali ya juu baada ya kupata maelezo ndipo nitakapounga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa jioni hii na mimi kuweza kutoa mchango wangu kwa hotuba hii nzuri ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ambayo bila ya shaka ni kwa niaba ya Mhe. Rais wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nitoe pongezi maalum kwa vyombo vya habari hususan TV na Redio. Kwa kweli vyombo hivi tokea tuanze mkutano huu wameamua kuonesha Wawakilishi wao *live*. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa mtaji huu tunaweza kumbe nia ilikuwa haipo. Hivyo, hapa tulipo basi Wazanzibari wanatupelekea message kwamba hili ndilo Baraza. Nadhani nimuombe Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, aongeze mfumo huu pamoja na kuwalipa posho zuri wale waandishi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, niwaambie Waheshimiwa Wajumbe kwamba Wazanzibari wanafuatilia michango yetu. Kwa hivyo, lazima tuwatetee na tujenge hoja kwa Serikali yetu ya Umoja wa Kitaifa, kwa sababu kazi ndio kipimo cha utu wa binadamu. *(Makofi)*

Nianze mchango wangu kuzungumzia kuhusu suala la Ushirikiano wa Kikanda. Mhe. Waziri katika hotuba hii ameeleza kwamba Zanzibar pamoja na Tanzania itaingia kwenye Ushirikiano wa Kikanda kuanzia Nchi za Afrika ya Mashariki. Sasa ninachopenda kulifahamisha Baraza hili pamoja na wananchi wa Zanzibar ni kuwa zamani Afrika ya Mashariki ilikuwa ni Kenya, Tanzania na Uganda, lakini sasa kwenye ushirikiano tumeongeza Burundi pamoja na Rwanda.

Mhe. Naibu Spika, kuelekea kwenye Shirikisho la Afrika ya Mashariki nchi tano hizi tayari zimeshasaini itifaki mbali mbali ikiwemo Itifaki ya Soko la Pamoja, Sarafu na Shirikisho la Afrika ya Mashariki. Mhe. Naibu Spika, Soko la Pamoja tayari limeshaanza tokea mwezi wa Julai tokea mwaka 2010 na wala sina hakika Wazanzibari wameshirikishwa vipi, lakini ninahakika Tanzania kwa maana ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walishiriki.

Vile vile mwaka 2013 Mhe. Naibu Spika, nchi hizi tano zitaingia kwenye Shirikisho la Sarafu moja na sisi tukiwa chini ya *BoT*. Kwa kweli hivi ninavyozungumza Maafisa wakubwa wa *BoT* wa ngazi za juu ni 80 na Mzanzibari mmoja ni Tanzania kwa maana ya Zanzibar na Tanganyika 80 kwa 1 na wala bado hatujaingia Sarafu Moja ya Afrika ya Mashariki. Mhe. Naibu Spika, ni dhahiri kwamba tukiingia huko basi Zanzibar itakuwa na *negative zero*, kwa sababu nchi moja 80 kwa 1. Je, nchi tano kwa ngapi? *(Makofi)*

Namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, aniambie kwamba nini hatima ya Zanzibar kwa uchumi wetu. Sasa ikiwa bado hatujaingia kwenye Shirikisho tayari kuna migogoro au kero na mimi nasema ni migogoro zaidi ya 40 na tukiingia tutakuwa na mingapi. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba Zanzibar itakuwa imemezwa na wala hatuna sauti tena kwenye Afrika ya Mashariki.

Mhe. Naibu Spika, msemaji wa Tanzania kwa mikataba hii ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hivyo, naomba sana Zanzibar chini ya Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein waandae utaratibu wa Baraza la Wawakilishi kuridhia mikataba hii kwa mambo ambayo si ya muungano. *(Makofi)*

Kwa kweli si haki wala busara kuwa masuala ya Zanzibar kuamuliwa na Watanganyika, haipendezi na hili ni jukumu kubwa na kila mtu humu ameapa kwa kutumia Msahafu. Kwa maana hiyo, Wazanzibari wanataka walindwe na watetewe kwa mujibu wa Katiba yetu ya Zanzibar. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, anieleze maslahi ya Zanzibar kwenye shirikisho hili vipi yatalindwa kwa ustawi wan chi hii pamoja na watu wake. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kama hilo halitoshi mwezi Febuari, 2011 Kituo cha Katiba cha Afrika ya Mashariki kiliandaa Kongamano juu ya Utafiti wa Nafasi ya Zanzibar kwenye Afrika ya Mashariki. Jambo la kusikitisha hakuna Mtanzania ambaye aliyetetea maslahi ya Zanzibar, lakini nashukuru Burundi na Rwanda walitutetea. Sasa ikiwa Mtanzania hatetei maslahi ya Zanzibar anatokea Mnyaruwanda ndio anatutetea sisi Wazanzibari kwa kweli ni mtihani mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa hakika kwa mtazamo wa haraka Zanzibar imekwisha na niungane na Mhe. Mohammed Ibrahim Sanya Mbunge wa Jimbo la Mji Mkongwe, kwamba kweli Zanzibar kweli Mfakiridhia, maana yake bwana *hewallah*. Mhe. Naibu Spika, haya mpaka lini, kwa sababu Katiba inasema Zanzibar ni nchi, kwa nini hatuwezi kuamua hata kwa yale ambayo si ya Muungano na wao ndio watuamulie. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nadhani Mhe. Waziri atazingatia. Ingawa msitu mkubwa wa SMZ ni kero za Muungano, sasa kero ambayo haina suluhi si kero ni ugomvi. Kwa kweli kero ambao haina suluhu si kero ni ugomvi. Kwa hivyo, naishauri serikali kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba hii *terminology* wangeibadilisha sasa wakasema ugomvi badala ya kero na vyenginevyo Mhe. Naibu Spika Wazanzibari wasikubali kutoa fedha kwa msitu wa kero inawezekana huu ni mtaji wa watu, nikisema hivyo mara moja nawaza kuambiwa niombe radhi.

Lakini dalili zinaonyesha kwamba nia nzuri hatunayo ya kuwatendea Wazanzibari mimi naona tabu sana. Mwaka juzi kulikuwa na mkiristo mmoja mwaka huu sote ni waislam na wengine ni Maalhaj, naomba sana Wazanzibari tuwatetee kwa maslahi yao tuwache yote tuliyokuwa nayo vyenginevyo kila mmoja ni mchunga na kila mmoja atakwenda kuulizwa alichokichunga.

Mhe. Naibu Spika, mimi niwapongeze Mafunzo kwa jinsi wanavyofanya kazi kubwa kwa kulima vilimo mbali mbali kama vile mboga, mpunga, mihogo na vyengine na naamini mpango wa kilimo hapa utapata majibu, lakini ningeshauri sasa kwa sababu serikali inaingia katika mpango huo kuna haja sasa serikali ikaamua kabisa kabisa kuondosha sera ya uwekezaji wa kiwanda cha sukari Mahonda na badala yake bonde lile wapewe Magereza walifanyie kazi, liwe bonde la mfano. Zanzibar Mhe. Naibu Spika, si nchi ya *sprit* wala ulevi, tubadilishe mkataba uvunjwe wapewe Magereza walime hii mbegu ya Irika nina hakika majibu ya chakula Zanzibar yatapatikana.

Mhe. Naibu Spika, Zimamoto niwapongeze vile vile lakini niwaombee sana kwamba wapewe mafunzo wanafanya kazi nzuri sana, kuna utafiti ambao sio rasmi kwamba vyombo vya zimamoto wanavyopewa havina kiwango wanapewa magari mengine hata tenki la maji hayana ni matatizo ya utaratibu wa ununuzi, mambo ya ununuzi kwenye vikosi vyetu ni mtihani. Usimamizi ni mdogo kwenye mambo ya fedha kwenye vikosi vyetu wafanyakazi hawa ikiwa hawana vitendea kazi daima watalaumiwa kwamba ni wazembe kumbe hatujawawezesha kufanya kazi. Mhe. Naibu Spika, ningesema tu kwamba vikosi hivi viongezewe nyenzo.

Mhe. Naibu Spika, wenzangu wamezungumza kwenye KMKM mimi niseme tu kwamba haiwezekani kwamba watu wapewe fedha baadae wasahau marejesho, wasahau stakabadhi, wasahau kumbu kumbu ni makusudi na watu wanafanya hivi kwa sababu wanajua hawaambiwi kitu, hayo Mhe. Naibu Spika sio ya leo mimi nimeingia humu mwaka wa sita lakini lakini nimekuta kumbu kumbu zaidi ha miaka ishirini nyuma haya yapo na yatakuwepo kwa nini kwa sababu hawaambiwi kitu.

Mtu anajua akiharibu kubwa atahamishwa tu atatoka Mkokotoni atakwenda Dunga, au Mkoani. Kwa hivyo kama serikali hii iko

makini kwenye nidhamu ya fedha basi taratibu za sheria za mwaka 2005 zifuatwe, nitashangaa sana Mhe. Waziri wa Fedha najua ni mtaalam akiachia uzembe huu, fedha inapotea milioni mia saba (700,000,000) eti mtu kasahau stakabadhi.

Siku moja nilikwenda mara moja risiti ni mpya anaitoa saa nne asubuhi mimi naingia pale saa nne na robo ni mpya kabisa risiti, miaka minne nyuma hajaipata anaipata siku ile ni tatizo, kwa hivyo Mzanzibari akisema kwamba Zanzibar kuna ufisadi hata serikali ikatae huo ni ukweli kwa sababu ushahidi wa mambo ni mazingira au uhalisia, kwa hivyo mazingira ya Zanzibar ni kweli kwamba yapo yanaandaliwa kwa wizi wa makusudi, haiwezekani leo ukisema hapa iundwe tume serikali inabadilika rangi kama kinyonga mimi ukinambia hapa nilipo njoo unisachi bangi sina wasi wasi nitavua nguo zote, kwa nini sina wasi wasi wa kusachiwa bangi.

Lakini sema basi tuunde tume wote watageuka kama jambo kuubwa ni dhahiri kwamba watu tunawalea kwa makusudi mtu aliyekuwa hana dhambi haogopi kusachiwa, mtu aliyekuwa hana kosa haogopi kusachiwa, lakini dereva wa gari barabarani akisimamishwa Taxi akipita mbio huyo maana yake naha leseni au watu wamezidi ndio maana yake. Mhe. Naibu Spika, nadhani serikali hii ibadilike na mimi namuamini sana Mhe. Waziri wa Fedha kwamba suala hili la fedha atalisimamia.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie hoja yangu kwa Baraza la Manispaa juzi nimeshangaa sana lakini sheria imetumika kuna Mzanzibari amefungwa mwezi mmoja au faini ya elfu hamsini kwa sababu amekojoa hadharani, amekwenda haja ndogo barabarani amefungwa mwezi mmoja, lakini baraza hili hili halichukui hatua kwa yule mwizi anayeiba dhahiri shahiri Wazanzibari wanashangaa, kwenda haja ndogo ni kosa kisheria anafungwa lakini aliyesababisha uchafu akageuza maduka vyoo hafungwi wala haambiwi kitu. Watu wajisaidie wapi na bahati mbaya Mhe.

Naibu Spika, tumetoa mwanya kwa Wazanzibari Mkaazi watu wanaingia tu ukifika hapa wiki mbili ni Mzanzibari Mkaazi, watu wanakwenda haja kubwa ovyo, lakini huyu aliyesababisha vyoo vifungwe haulizwi.

Leo pale mjini ukiwa Malindi basi utapata choo Asha Fatuma Mwanakwerekwe tatizo nini usimamizi wa halmashauri, mimi nashangaa sana kuna mapato hapa Baraza hili la Manispaa limeona kwamba ni busara kusamehe milioni 762 za wafanya biashara kwa kupanda Pemba grass, maana yake Pemba grass ni muhimu zaidi kuliko mapato kwa wafanya biashara hawa. Nina utafiti niliofanya hapa Baraza la Manispaa wanakusanya shilingi milioni 762 kwa mwaka lakini tuwazuiye tupande Pemba grass ndio muhimu, mimi nataka niambiwe Pemba grass ile ninayoijua mimi ya Mwambe na Kangagani itatia shilingi ngapi hapa Zanzibar.

Mwisho Mhe. Spika, niseme kwamba vyovyote vile alivyo mimi niko radhi apelekwe Ikulu maana mtu mzuri apelekwe Ikulu lakini Mkurugenzi ni tatizo, juzi tulikuwa na semina *ocean view* nyote mlikuwepo niliwashuhudia watu anasema madiwani wanataka nikitumia wanione mimi bosi bwana, mimi nitaendekeza wanasiasa wapumbavu wale wee nani yakhe.

Diwani kachaguliwa na wananchi wewe umewekwa tu , kwa hivyo mtu mzuri nashauri apelekwe Ikulu akafanye kazi lakini pale aondoshwe kwa sababu ni tatizo sasa hivi Zanzibar nzima sura yake inaharibiwa na mtu mmoja kama kwamba kuna wizi mkubwa, kumbe ni taratibu za kisheria hazifuatwi ubabe leo Jamhuri garden imekodishwa kwa shilingi milioni moja, lakini serikali inapata laki moja.

Mhe. Naibu Spika, mimi nasema mbili mara moja nne hata kwenda hesabu hiyo hapa tumefeli. Kampuni ya Tigo wanakwambia mbili mara moja nne kumbe ni Zantel, mimi

nasema kwamba Waziri tunakuheshimu tumeelewa busara za Mhe. Makamo wa Pili wa Rais lakini tunataka majibu Baraza la Manispaa kwa usalama wa nchi yetu na maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya hapo nikiridhishwa nitaunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mahamoud Mohammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi kupata fursa ya kuchangia katika hotuba ya Mhe. Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Ikulu, kwa kuanza kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima salama na uhai, lakini pia nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Ikulu pamoja na watendaji wake wote kwa ujumla kwa kutayarisha hotuba hii safi na nzuri ambayo ina mwelekeo wa kusaidia taifa letu.

Lakini pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, hapo kwa kuweza kukilinda vizuri kiti chako na kuendelea kutuongoza vizuri katika Baraza letu hili tukufu ambalo linajadili na kupitisha bajeti ya serikali, baada ya shukurani hizo nianze kwa kuachangia kwenye ukurasa wa 45.

Mhe. Naibu Spika kwa kweli nimefarijika sana kuona kwamba baada ya kilio cha muda mrefu serikali imeweza kuona umuhimu wa msingi mkuu ule ambao umetokea maeneo ya Magomeni mpaka kuelekea Kilimani chini kule ambao uko tayari sasa kutafutiwa ufumbuzi wa suala lile, lakini kama hiyo haitoshi napenda pia kutoa pongezi zangu za dhati kabisa kwa mtaro mwengine ambao umetokea Kidongo Chekundu na kuelekea maeneo ya chini ya Kizingo nayo pia nashukuru sana kwamba kutokana na kazia tuliyokuwa nayo kwa muda mrefu serikali imeona kwamba maeneo yale sasa yafanyiwe kazi na yamepewa kipaumbele katika bajeti ya mwaka huu.

Lakini pia nakuja katika ukurasa wa 58 ambapo kunazungumziwa kazi za Manispaa, naomba kunukuu kidogo hapa.

"*Baraza la manispaa limeundwa kwa sheria namba tatu ya mwaka 1995 kwa ajili ya kufanikisha majukumu ya kusimamia kazi mbali mbali za maendeleo katika mji wa Zanzibar pamoja na utoaji wa huduma za uzoaji wa taka, usafishaji wa michirizi na maji machafu ya mvua, usafi wa barabara, ukarabati wa barabara pamoja na taa, utunzaji wa bustani na maeneo yaliyo wazi"*

Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atuelezee kwa kina mpango mzima unaohusu bustani ya Botanic kule, kwa sababu eneo lile naona limekwisha kuchafuka sana na imekuwa ni kimbilio la kutupa taka taka, kwa hivyo atueleze mpango gani utatumika katika serikali ili kuhakikisha kwamba eneo lile linatunzwa na kurejea katika haiba yake ile ya zamani.

Jengine katika ukurasa wa 59 Mhe. Waziri pamoja na kwamba kuna mipango ya kusaidia hii michirizi ambayo omo katika mji huu wa Zanzibar, lakini maeneo mengi sana ambayo michirizi hii imepita imekuwa sasa tayari imekwisha kujengwa kuna nyumba nyengine zinakaa watu kabisa, sasa sijui serikali imejipanga vipi katika kuhakikisha kwamba michirizi hii inakuja kurejeshewa uwezo wake na maji yakaweza kupita bila ya matatizo ya aina yoyote, tusije tukafanya mpango kama ule ambao umetokezea zamani wa kuweza kutumia pesa nyingi sana katika mradi wa Mnazi Mmoja lakini badala yake tatizo likawepo pale pale.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuchangia katika ukurasa wa 60 ambapo tunazungumzia suala la soko la Mombasa, Mhe. Waziri wakati sasa umefika serikali iweze kutafuta njia mbadala wa kuhakikisha kwamba soko la Mombasa linatumika kwa ajili ya bidhaa za mboga mboga, si jambo la busara kuona kwamba wahisani wa maendeleo wanatusaidia kupata fedha nyingi na

wakaweza kutujengea masoko kama yale ya Mombasa, Dimani na mwengine na masoko yale wananchi wakawa hawayaatumii. Naiomba Wizara yako pamoja na wataalam uliokuwa nao tutumie uwezo tulionao tuhakikishe kwamba tunapanga jambo lolote la mbadala ili masoko haya yaweze kutumika na malengo yaweze kufikiwa.

Jengine Mhe. Waziri ni kwamba tunakuja katika suala la michirizi ambapo katika maeneo ya nyumba za maendeleo kwa mfano Kilimani michirizi ya kuchukua maji machafu imeharibika na uwezo wake umepotea na kupelekea maji machafu kutuwama chini ya majumba ya maendeleo, tunaomba pamoja na mipango endelevu ambayo imepangwa basi tuhakikishe kwamba tunafanya utaratibu wa kusaidia maeneo yale ili wananchi wasije kupata madhara zaidi katika maeneo yao yale.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni ukusanyaji wa kodi baina ya Baraza la Mji na ZRB kumekuwa na utitiri mkubwa sana na mkanganyiko juu ya ukusanyaji wa mapato ya leseni baina ya ZRB na Baraza la Mji, naona wakati umefika wa kutengenezwa utaratibu muafaka wa kuhakikisha kwamba kila taasisi ambayo ina majukumu kutimiza majukumu yake, lakini kuhakikisha kwamba mapato yanakusanywa sehemu moja tu katika nchi yetu.

Jengine ni ukamilishwaji wa njia za ndani. Mhe. Naibu Spika, katika maelezo hapa yaliyokuwa yakitolewa mara nyingi na Waziri wa Mawasiliano na Miungo mbinu tunapozungumzia suala la barabara za ndani yaani *feeder road* mara nyingi tumekuwa tukipata maelekezo kwamba mwenye majukumu ya kusimaia *feeder road* ni Baraza la Manispaa, sasa tunaomba Mhe. Waziri kupitia katika Wizara yako hii utusimamie katika suala hili, ili barabara zetu za ndani ziweze kuchukuliwa hatua na ziweze kukamilishwa.

Mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, napenda kuchangia katika sehemu za vikosi wakati umefika sasa kwa vikosi hivi vya SMZ pamoja na majukumu ambayo wanayo, tungelipenda kuwafahamisha kwamba yale mapinduzi ya kilimo ambayo yameasisiwa na kusimamiwa Rais wetu wa Zanzibar sasa yaelekezwe katika vikosi hivi na tuhakikishe kwamba vinafanya kazi za ziada katika kuhakikisha kilimo kinaendelezwa kama hiki cha mpunga pamoja na mihogo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo kwa heshima na taadhima naunga mkono hoja kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Kikwajuni ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Farida Amour Mohammed: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii jioni hii ya leo, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa hazina ya uzima na afya njema kusimama katika Baraza lako tukufu kwa wakati huu.

Pili naomba nimpongeze Mhe. Waziri katika Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi jinsi alivyofafanua kitabu chake hiki kwa ustadi mkubwa, naomba nilipongeze Baraza la Mji Wete kwa kuvuka malengo ya ukusanyaji wa mapato yao. Kwa mjibu walivyojipangia walitegemea watakusanya milioni 40 lakini katika hotuba yao wamefanikiwa kukusanya milioni 42.

Mhe. Spika, nije ukurasa wa 69 kwa mwaka ujao walipanga kuweka kifusi katika maegesho ya gari, ikiwa kituo hicho cha maegesho ya magari ni kituo cha *stand* ya magari ya Wete cha Mkoa sikubaliani na kuwekwa kifusi, eneo lililopangiwa kuwekwa kifusi wakati wa nyuma lilikuwa na lami sasa hivi iweje kwa wakati huu baada ya kutengeneza lami iliyopotoea kidogo tu pakatandikwa kifusi. Ushauri wangu nalishauri Baraza la Mji lishirikiane na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kuweka lami na kuirudisha hadhi yake ya zamani ya *stand* hiyo.

Mhe. Naibu Spika, katika hali kama hii juu ya kulisifu Baraza la Mji la Wete kwa kazi nzungi waliyoifanya ya ukusanyaji na malengo yao waliyokusudia, naomba niseme kitu kimoja Afisi ya Katiba wa Baraza la Mji Wete ni chafu, ni mbofu na hailingani na hadhi ya kukaa Katibu wa Baraza la Mji, ushauri wangu kwa Mhe. Waziri patafutwe eneo zuri parekebishwe watengewe sehemu nyengine ambayo inakwenda na hadhi ya Afisi ya Katibu wa Baraza la Mji.

Mhe. Naibu Spika, katika hali hiyo hiyo kuna maeneo muhimu ya Afisi ndani ya Wilaya yangu ya Wete ambazo kuwa haziridhishi ikiwemo Afisi ya Mkuu wa Wilaya ya Wete, Mhe. Naibu Spika, Afisi ya Mkuu wa Wilaya Wete nayo ni mbovu sana. Namshauri Mhe. Waziri aliangalie hili anaekaa mle ni Mkuu wa Wilaya ni kiongozi wetu mzuri na muhimu anapaswa kukaa eneo zuri lenye kuendana na hadhi yake.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba niendelee kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Wete pia niipongeze kwa kuvuka malengo ya ukusanyaji wao walitegemea kukusanya milioni 25 na bahati wamefanikiwa kukusanya zile zile milioni 25, lakini naomba niishauri Halmashauri ya Wilaya ya Wete itafute mbinu mbadala za ukusanyaji kwani kutokana na hali hiyo ukusanyaji wao bado ni mdogo mno.

Katika malengo yao ya mwaka 2011/2012 ukurasa wa 70 imepanga ujenzi wa msingi wa Afisi ya Halmashauri hapo naomba ufafanuzi. Je, halmashauri imekusudia kufanya nini, msingi wao umeharibika unataka kurekebishwa au Halmashauri ina ujenzi wa Afisi mpya ya Hamashauri ya Wilaya na sasa inataka kuanza *foundation* kwa sababu ofisi yao ni mbovu, je pana msingi wa maji karibu na eneo la Afisi ya Hamashauri ya Wilaya na inataka kuutengeneza.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 55 kwenye malengo waliyoyakusudia watu wa Halmashauri pamoja na kulenga kusaidia maeneo mengi ikiwemo Ustawi wa Jamii, Afya, Elimu, Uwezeshaji na mambo mengine, sasa katika hali hii naomba kusema neno moja wana kijiji wa mjini Kiuyu Jimbo la Ole Wilaya ya Wete wamefanikiwa kwa nguvu zao wenyewe pamoja na misaada kutoka sehemu nyengine na hata kwenye Halmashauri yao ya Wilaya ya Wete kujenga kituo cha Afya ambacho wameshafikia hatua ya kuezeka.

Sasa namuomba Mhe. Waziri katika hili awaonee huruma wanakijiji hao kwani kutokana na eneo wanaloishi na kwenye kituo cha afya ni mbali sana, kwa kuwasaidia wanawake kwenda kuheshimu zile nguvu zao naomba wafanyiwe utaratibu wa kumaliziwa kile kituo cha afya na kupatiwa huduma wananchi hao.

Kwa vile mambo mengi yameshachangiwa na wenzangu sitaki nipoteze muda lakini kabla sijamalizia kuunga mkono hoja hii, naomba niseme neno moja Serikali ilitumia pesa nyingi sana kufanya chaguzi tano ndani ya nchi yetu, uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania, Uchaguzi wa Rais wa Zaznibar, Mbunge, Muwakilishi na madiwani. Cha kusikitisha madiwani hawa hawaonekani kusaidiwa chochote ndani ya nchi yao, hawana maslahi ndani ya nchi hii na kuthamini ule uchaguzi wao waliochaguliwa.

Kwa hivyo naomba tukumbuke maneno ya hekima ya muasisi wetu wa serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Marehemu Abeid Amani Karume yaliyosema.

“*Bora tuwe na chakula kidogo tugawane kidogo kidogo kuliko kuwa na chakula kingi tukaanza kukigombea”.*

Kwa hali hii naomba Mhe. Waziri, Madiwani wetu tuwaone kwa hicho hicho kidogo tulichokuwa nacho, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuweza kunipatia nafasi hii ya kuchangia bajeti hii ya Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa leo sina mchango mkubwa wa kuchangia isipokuwa ni kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia kufika hapa na kuweza kuchangia bajeti hii kwa pamoja.

Kwa leo nitachangia zaidi ukurasa wa 79 kifungu cha 163 kuhusu vikosi vya SMZ. Kwanza naanza kuchangia kwa ndugu zetu wa JKU wao bajeti yao waliyopewa ni ndogo sana kutokana na hadhi ya nchi yetu ilivyo na utendaji wao wa kazi, JKU ilianzishwa mapema tangu Rais wa Kwanza wa Zanzibar Marehemu Mzee Abeid Amani Karume kwa ajili ya kazi na sasa hivi inaitwa JKU vijana hawa walitunzwa kwa muda mrefu na vijana wa kwanza kwa Zanzibar kuweza kupewa nyumba za Michenzani kwa vile ni vijana ambao walikuwa wanajenga taifa na wanatekeleza vizuri majukumu yao kwa ajili ya taifa letu la Zanzibar.

Hivi sasa vijana hao wa JKU unakuta mambo yao yamekuwa magumu zaidi kwa sababu wajibu wa kuwatunza umepungua sana na kukosa malipo kwa JKU sas vijana hao wanapita kwa muda mrefu lakini sasa hivi wamebadilishwa na kuishia JKT.

Kwa muda mrefu sasa hivi vijana hawa wanaelekea JKT na tunapunguza nguvu kubwa hapa Zanzibar kwa vijana wetu kwenda JKT kwa ajili ya kutafuta ajira baada ya JKU kukosa ajira maalum ya kuwasaidia vijana wetu, hivi karibuni kuna vijana sio chini ya 300 na zaidi wameelekea JKT badala ya kushindwa kuwajibika hapa Zanzibar kwamba hatuwapi malipo ambayo yanategemewa, wanakwenda JKT kwa ajili ya kutafuta ajira wakati vijana hao walikuwepo hapa Zanzibar wanapatiwa ajira

moja kwa moja kama walivyozoea na hasa ajira zao zilikuwa zinakwenda kwenye nafasi za ulinzi. Sasa utakuta vijana hao nafasi hizo za ulinzi zimeondoka na utakuta hawapati nafasi zozote za ajira ambazo walitegemea kuzipata na matokeo yao wanaelekea JKT na JKT wakifika vijana hao nafasi walizozitegemea hawazipati isipokuwa wanakwenda kutoa nguvu kubwa kwa kikosi cha JKT badala ya kutoa nguvu zile kwa JKU.

Vijana hao sasa hivi wanakwenda JKT wanapata malipo zaidi ya Sh. 60,000 kuna sababu gani Waziri angalikuwa amewatunza hapa Zanzibar wasichukuliwe na JKT angalau bajeti yao ikapanda kuweza kulipwa vijana hao si chini ya Shs. 50,000 kama walivyozoea wakati wa mwanzo kilipoanzishwa kikosi hiki cha JKU na Marehemu Mzee Abeid Amani Karume alikuwa anawalipa sio chini ya shilingi 50,000. Kwa hivi sasa nguvu kubwa ambazo tumezitoa JKU kuzipeleka JKT. Iko haja Waziri bajeti hii aiongeze ili fedha ile iende kwa JKU ili vijana hawa wabakie kutoa msaada kwa taifa letu liweze kuimarika zaidi na lieleweke kwamba Zanzibar pana vikosi vya ujenzi wa taifa ambavyo vinaitwa JKU.

Vijana wetu wa JKU ilikuwa ndio wanaokwenda katika vikosi vya ulinzi kama jeshi la JWTZ, jeshi la Polisi na Usalama. Utakuta sasa nafasi hizo JKU zote hazipatikani matokeo vijana wanakaa kule JKU kufanya kazi za amali na wakitoka hawapati ajira zozote. Hapo zamani tulizoea kwamba vijana wakimaliza skuli tu wanakwenda JKU kujenga taifa na vijana hao wanaanzia darasa la 7,8 la 10 hadi la 12, kule ndiko wanapongoja ajira zao za kuweza kupata ajira za ulinzi.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na hali hiyo hivi sasa utakuta kwamba vijana wengi hawapati nafasi za ulinzi na utakuta Zanzibar mwisho itakuwa halipo jeshi la ulinzi isipokuwa lipo jeshi la JKU, KVZ, na KMKM. Kusema hivyo ni kusema kwamba mwisho wake Zanzibar tutakuwa hatuna hata maafisa wa

majeshi ya ulinzi hata kufikia cheo cha Jeneral au Brigedia au Canal. Vijana wengi wanakwenda JKT na huko hawapati kazi kama tulivyotegemea hapo mwanzo kupata ajira kutoka JKU.

Tulikuwa tuna fungu maalum hapa Zanzibar la askari wa ujenzi wa taifa, wanatoka askari si chini ya 500 au 1000 kwenda katika majeshi yetu. Sasa hivi utakuta si chini ya mwaka wa pili au wa tatu vijana wa JKU hakuna ambaye anaajiriwa katika jeshi la ulinzi.

Hii sasa utakuta jeshi la ulinzi limeshaajiri wapiganaji kutoka JKT lakini hakuna hata Mzanzibari mmoja ambaye ameajiriwa pale. Utakwenda Mafinga utakuta kuna kozi ya jeshi la Wananchi wa Tanzania au unakwenda Tanga utakuta mafunzo ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania lakini hukuti vijana ambao wametoka Zanzibar kutoka JKU ambao wapo kule kwenye ajira.

Hilo ni kosa kubwa ambalo vikosi vyetu vinapoteza muda wao na vijana wanakosa kupata ajira kama tulivyotegemea. Bajeti hii iliyopangwa kwenda JKU ni ndogo kwa kuzuia vijana wetu wasiondoke Zanzibar kuelekea JKT huko Tanzania Bara. Ni afadhali waongezewe bajeti ili vijana hawa waweze kupata ajira angalau walipwe shilingi 40 mapaka 50 waweze kubakia hapa na sio kuondoka kuelekea JKT ambapo tunapoteza nguvu kubwa ya vijana wetu kwenda kule badala ya kubakia Zanzibar.

Nikirejea vikosi hivyo hivyo vya SMZ nazungumzia kikosi cha KMKM. Hiki ni kikosi tegemezi tunachokitegemea kwa ulinzi wa baharini. Utakuta kikosi hicho cha baharini tumekiweka kwa ajili ya kuzuia magendo tu wakati tulijua kikosi cha KMKM ni kikosi cha mapigano kama vikosi vyengine vya baharini. Vikosi hivyo iko haja ya kupata boti za kisasa ambazo zina silaha za kisasa kwa ajilli ya ulinzi, sio kwa ajili ya kukamata karafuu na nazi tu. Hiyo sio kazi inategemea Zanzibar kama ni nchi, lazima kiwe na ulinzi ambao unatambulika na dunia nzima. Isiwe vikosi vyetu vimekaa

kwa ajili ya magendo kama ilivyo hivi sasa. Vile vile vikosi vyetu vya Magereza ambavyo sasa hivi vinaitwa Chuo cha Mafunzo. Chuo cha Mafunzo ni kikosi ambacho kina wapiganaji ambao tunawategemea sana kwa ulinzi na kwa ajili ya kuwatunza watu wa mafunzo.

Hichi chombo hivi sasa kinatakiwa kiwe cha kisasa kama tunavyotegemea tuondokane na wakati uliopita. Chuo cha Mafunzo kina hatua mbaya ambayo kinatumia *mtondoo* kama wakati hatujajitawala. Nafasi hiyo ilikuwa iondeke hivi sasa iwe ni sehemu ya kawaida ambayo hizi sasa iwe na vyoo kama kawaida ya nchi nyengine. Magereza ambayo hivi sasa ni Chuo cha Mafunzo inahitaji zaidi kuondoa mtondoo na kutumia mambo ya kisasa ambayo ni lazima kuwe na vyoo. (*Makofi*)

Tulipita kwenye kamati yetu kutembelea sehemu hizo, tulikuta sehemu moja tu ambayo sasa inajitayarisha na mambo ya kisasa, Chuo cha Mafunzo cha Ubago ndicho hivi sasa kinaanza kuwa na vyoo. Ukienda Chuo cha Mafunzo cha Hanyegwa ndio peke yake tulipokuta choo cha kisasa ambacho kimeanza kujengwa. Mhe. Naibu Spika, napenda twenda na wakati ili tuondokana na mambo ya kizamani ambayo yamepitwa na wakati.

Nikienda upande wa Manispaa. Manispaa yetu hivi sasa haitekelezi wajibu wake wa usafi. Usafi unatakiwa ufanywe muda wote wa nchi. Usafi ule ungelikuwa ni bora kufanyika wakati wa usiku.

Mchana ikawa ni masawazisho tu, lakini usafiri wote unafanyika usiku kwa vile Idara hii ina watu wengi ni afadhali kugawana nusu. Nusu wakaenda usiku na nusu wakenda mchana kwa kufanya masawazisho ambapo usiku kazi ile imefanyika. Utakuta kazi yote inafanywa asubuhi na hakuna chochote kinachofanyika katika Manispaa ile.

UTARATIBU

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ibara ya 88(3) kinasema kwamba "Mjumbe yeyote anapokuwa akisema Barazani atawajibika kuwa na sababu za msingi kwamba maelezo anayoyatoa ni sahihi na sio mambo ya kubuni au ya kubahatisha. Spika, au mjumbe mwengine yeyote anaweza kumtaka mjumbe huyo anayesema atoe uthibitisho wa usemi wake unaohusika".

Mjumbe aliyekuwa anazungumza sasa hivi alisema kwamba enzi ya Mzee Karume JKU walikuwa wakilipwa shilingi elfu 50. Katika kuweka kumbukumbu sawa Mheshimiwa enzi ya Marehemu Mzee Abeid Amani Karume muasisi wa taifa hili ilikuwa hakuna JKU na badala yake kulikuwa kuna Valantia. Walikuwa wanajitolea Mavalantia hao, walikuwa wanapewa posho dogo tu. Kwa kuweka kumbukumbu sawa hakukuwa na malipo ya sh. 50,000 wala hakukuwa na JKU badala yake kulikuwa na Valantia.

Namuomba Mjumbe afute hoja yake hii na maneno yake hayo.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mheshimiwa Mjumbe kwa maelekezo, Mjumbe unayechangia, urekebishe maelezo yako kwamba kipindi hicho kulikuwa hakuna JKU, kulikuwa na Valantia na walikuwa hawalipwi kiasi hicho. Kwa hivyo weka sawa hotuba yako halafu umalizie.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Ahsante Mhe. Naibu Spika, wakati wa marehemu Mzee Karume JKU walikuwa wanapata posho na malipo ambapo sio zaidi ya shilingi elfu 50 ilikuwa haifiki lakini walikuwa wakipata posho, pamoja na nyumba za Michenzani.

Mhe. Naibu Spika, sasa hivi nazungumzia Baraza la Manispaa. Baraza la Manispaa lingeliendelea kufanya usafi usiku badala ya mchana.

Mhe. Naibu Spika: Dakika tano imebaki umalizie.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Ingeliweza kufanya shughuli zake za usafi usiku badala ya kufanya shughuli hizo mchana. Vile vile nachangia kuhusu vijana wetu ambao hupatiwa ajira katika sehemu mbali mbali za Manispaa.

Hivi sasa kuna vijana wengi wanatarisha usafi mjini kwa ajili ya Manispaa vile wapatiwe ajira zaidi katika Manispaa hivyo na sio kujenga taifa kama walivyo sasa. Kwa hoja hii nachangia mimi na Jimbo langu la Koani tunaunga mkono hoja mia kwa mia.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwanza napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mhe. Mwenyekiti, wa Baraza la Mapinduzi, Waziri kwa hotuba yake ya Bajeti aliyotuletea ambayo imejaa ufanisi.

Mhe. Naibu Spika, mimi sitaki niende mbali sana kwa sababu mambo mengi yameshachangiwa na mengi yameshapata ufafanuzi, ila na mimi nilikuwa nataka nigusie tu kwa sababu **"***kila anayelia hushika kishikiole***".**

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nizungumzie kuhusu vitambulisho. Vitambulisho bado ni kero katika Wilaya zetu. Kwa hiyo tunaomba Ofisi za Wilaya zituwekee utaratibu mzuri wa kupata vitambulisho. Kweli ni lazima uwe na cheti za kuzaliwa lakini tunatakiwa tuzingatie na ule umri wa mtu unaohitajika kipatikane kile chetu cha kuzaliwa.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nizungumzia Madiwani. Madiwani wanalalamika sana kutokana na kuwa hawapati hata posho. Madiwani hawa na wao wamechaguliwa kwa uchaguzi

Mkuu wa Zanzibar na kupiga kampeni, na kupoteza muda wao mrefu, lakini hatimaye wanashindwa hata kugaiwa Shilingi 50,000/ za mwezi.

Tunamuomba Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Mwenyekiti ya Baraza la Mapinduzi awaone madiwani na wao katika kero lao hili. Ingelikuwa madiwani wanapatiwa ruzuku yoyote katika kila mwezi basi wangilikuwa ni watu ambao kuwa wanakusanya mapato zao katika Wilaya zao. Lakini tatizo hawapewi katika serikali basin saa nyengine na wao watakuwa wanajichukulia mkono wao. Kwa hiyo naiyomba serikali wawaone madiwani kupitia suala hili.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 56, Mhe. Waziri ameomba kwa mwaka wa Fedha 2011/2012 anaomba Baraza hili tukufu liidhinishe shilingi milioni 700 kwa matumizi ya kawaida na shilingi milioni 250 kwa ruzuku kwa Baraza la Mji la Wete. Hapa miye katika Wilaya yangu sijui tunasaidia nini.

Kama tunavyojua Wilaya ya Micheweni ni Wilaya iliyokuwa ina misuko suko mengi. Humu sote tu mashahidi ni Wilaya ambayo kuwa umasikini umekithiri huko, majamgo hapo huko na mpaka juzi tunasikia kuwa katika hotuba ya Makamo wa Pili wa Rais ni kuwa hata tatizo la ukimwi ni Wilaya moja wapo inayoongoza. Sasa leo katika fungu hili naona Wilaya ya Micheweni japo kuwa ni Mkoa wa Kaskazini imo hiyo Wilaya ya Micheweni lakini naona angalau pengelikuwa pana fungu linaloingia la maendeleo katika Wilaya hii ya Micheweni.

Kwa hivyo Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri aliifikirie hii Wilaya sana katika mtizama wake ili kuondoa matatizo haya. Ni wilaya ambayo inahitaji kusaidia kwa kila hali na mali.

Usaidizi huo tunategea kusaidiwa katika serikali. hatutegemei kusaidiwa popote pale pengine isipokuwa tusaidiwe na Serikali

yetu hii ya Mapinduzi ya Zanzibar na ndio serikali ambayo kuwa wanaijua matatizo ya Wilaya hiyo. Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe, Waziri alione hilo na aifikirie hiyo Wilaya. Kwa hayo machache kwa niaba ya wananchi wangu wa Wilaya ya Micheweni naunga mkono hoja mia kwa mia.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nishukuru kwa kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia, hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri ambayo imejaa ufanisi na mambo yote ambayo tunayarajia katika serikali yetu.

Mimi nilikuwa naomba nichangia katika mambo kama matatu tu tena kwa mkato sana, kwa sababu mengi wenzangu wameshachangia, lengo na madhumuni ya kuyatia mkazo tu. Kwanza ni suala zima la Kikosi chetu cha JKU. Kwa kweli tukitaka tusitake kama tuna dhamira na nia njema ya kusaidia vijana wetu na kuisaidia serikali kuna haja ya jeshi letu la JKU na Jeshi la Kujenga Uchumi.

Jeshi hili la Kujenga Uchumi linaandaa vijana wetu na ndio vijana wa Taifa la kesho. Bahati nzuri ndugu zetu wa JKU wananyanja nyingi ambazo wameshajiandaa katika kuwasaidia vijana hawa, wana viwanda mbali mbali vya umeme, plamba, fanicha, pamoja na maeneo ya kilimo. Imani yangu kwamba kama serikali itatilia mkazo kutoa nguvu za kutosha basi itakuwa ni eneo tegemezi kwa vijana wetu katika kupata taaluma ya kuweza kujiajiri baadaye.

Nikitoka hapo nakuja katika suala zima ambalo wenzangu wengi wameliogelea tena kwa muda mrefu. Na mimi naomba nilitilie nguvu nalo ni sehemu ya Manispaa. Eneo hili kama kuna watu ambao inapozungumzwa wanakuwa makini au wanakuwa wanaumwa na Manispaa basi mimi nakuwa ni mmoja wapo. Mheshimiwa Taasisi hii mimi nimeitumikia kwa muda wa miaka 10 kuna kipindi wewe Mwenyewe Naibu Spika, ulikuwa Waziri

wangu wa Tawala za Mikoa na mimi nilikuwa Diwani. Mhe. Mwinyihaji alikuwa alikuwa Waziri wa Tawala za Mikoa wakati mimi nilikuwa Diwani. Mhe. Nyanga na yeye keshakuwa Waziri wangu wakati mimi nilikuwa Diwani. Nimesha *deal* na Makatibu wengi, nimesha deal na Mawaziri wengi na Mamea wengi.

Kweli taasisi ina matatizo mengi lakini naomba nalo pia tulifahamu jitihada na wao pia wanajitahidi kadiri ya uwezo wao. Tulipoanzia sipo tulipo.

Mhe. Naibu Spika, wakati naingia Baraza la Manispaa mwaka 2000 lilikuwa linakusanya shilingi milioni 400, lakini kwa miaka miwili kutoka mwaka 2000 – 2002 liliweza kujikomboa kutoka shilingi milioni 400 hadi shilingi bilioni moja. Hii ni jitihada tosha.

Haya nayo yalikuwa ni mabadiliko katika jitihada za kazi zao. Lakini kama tunavyosema kwamba mchungaji mzuri huanza na ng'ombe mmoja hadi wawili. lakini ng'ombe wakishakuwa wengi inakuwa ni tatizo kwa mchungaji, hata kama atakuwa mchungaji mzuri vipi. Kundi linakuwa kubwa, kulichunga inakuwa tabu, hatimaye yule wa nyuma ndiye anayeanza kupata mikwaju baada ya kuwapiga wale wa mbele.

Mhe. Naibu Spika, hili linajionesha baada ya jitihada za Manispaa kuboresha usafi, kuboresha mapato yameshakuwa mengi sasa hivi ndio inaoneka ni tatizo. Imani yangu kwa Waziri tuliyokuwa naye, Mhe. Makamo wa Pili wa Rais wote hawa wanaonesha jitihada kubwa. Kweli matatizo tumeyazungumza mengi, matatizo yamejitokeza mengi, lakini na serikali ni lazima tuipongeze inajitahidi.

Pamoja na vizingiti ambavyo vimetokezea Barazani lakini Baraza ambalo lina mamlaka kamili kwa mujibu wa sheria, tatizo wameliona. Waliunda Kamati na kamati tatizo limeonekana.

Naamini taarifa imefika kwa Makamo wa Pili wa Rais pamoja na Waziri anayehusika kwa mujibu wa Taratibu ya sheria. Makamo wa Pili wa Rais na yeye aliahidi ndani ya Baraza hili kwamba ataunda Kamati na Kamati ameiuda. Sasa nafikiri ni vyema matatizo ambayo yamejitokeza mimi nawaomba chonde chonde, namuomba Mhe. Waziri na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwamba yale ambayo mapungufu yataonekana baada ya kukusanya taarifa zote, wajitahidi kuzifanyia kazi kwa umakini ili warejeshe matumaini kwa wananchi na kwa Baraza kwa jumla.

Nina imani hakuna lisilowezekana hata siku moja. Hususan baada ya kuangalia upevu wa wazee wetu. Mhe. Rais kaona. Nilipoangalia taasisi zote za Makamo wa Pili wa Rais, Makamo wa Kwanza wa Rais, Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, nilikuwa naanza kujiuliza vichwa vyao vinamvi, hizi ni hekma Mhe. Rais kaona. Hekima na busara walizokuwa nazo ninaimani kwamba matatizo haya yatafanyiwa kazi. Naomba watupe ufafanuzi wa kutosha, wayachukue kwa makini.

Mhe. Naibu Spika, katika hekma ambazo naziona baada ya kuangalia vitabu vyote viwili nimeangalia kitabu vya bajeti nikaangalia kifungu cha Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais nilipoviangalia nikaona tayari Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais ameshapea na ameshaona. Katika kibabu cha bajeti unakuta kuna pesa ambazo zimeandaliwa za miradi ya Manispaa, miradi ya taa na miradi ya michirizi, huku hazikuja. Hili ameanza kuliona kwamba nikizipeleka huku litakuwa tatizo. Kwa hatua hiyo nampongeza sana.

Mhe. Naibu Spika, namalizia la mwisho ambalo zito sana. Wajumbe wengi hawajalizungumzia.

Mhe. Naibu Spika: Muda umekwisha, kaa kitako. Waheshimiwa wajumbe tunashukuru kwa michango mizuri tangu asubuhi mpaka sasa hivi. Tumebakiwa na wachangiaji wanne, Wajumbe watatu

na Waziri mmoja. Tunategemea asubuhi ya kesho tumalize mjadala huu baada ya masuali, saa 5:00 tumwite Waziri kwa majumuisho na kupitisha vifungu. Tunaomba tuje mapema ili tuweze kumaliza wizara yetu hii.

Kwa hayo machache naakhirisha kikao mpaka kesho saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 30/06/2011 saa 3:00 asubuhi)